ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini - Tarehe 3 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 71

Matengenezo ya Mtaro wa Eneo la Mnadani Darajani

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 187

Mfumo wa Kubadilisha Nyaraka kutoka "*Manual*" Kwenda katika Mfumo wa Elektroniki:

Mhe. Mohamed Said Mohamed - Aliuliza:

Tunaipongeza serikali kwa kuanzisha mradi wa kubadilisha nyaraka kutoka mfumo wa kutumia karatasi "*manual*" kwenda katika mfumo wa kielektroniki.

(a) Je, vifaa vilivyotumika vina uhakika gani wa kuacha nyaraka katika uhalisia wake.

(b) Je, kuna uhakika wa kuzitumia rekodi za elektroniki inavyotakiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 187 lenye kifungu (a) na **(**b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kimsingi kubadilisha nyaraka kwenda mfumo wa kieletroniki ni moja kati ya njia za kuhuisha nyaraka zilizochakaa (*fragile documents)* ili zisitoweke. Vifaa vinavyotumika katika kazi ya uhaulishaji wa nyaraka hizo zimependekezwa na kununuliwa kutokana na

ushauri wa kitaalamu uliotolewa na Mtaalamu. Vifaa hivyo ni "*scanners*" za aina ya *"Book Scanners", "Flat Back Scanners"* na *"Map Scanners"*. Kazi hii inafanywa chini ya uangalizi wa wataalamu wa Kitengo cha Uhuishaji wa Nyaraka (*Conservation Unit*), kilichopo katika Jengo la Nyaraka za Taifa. Hivyo, upo uhakika wa kutosha kuwa nyaraka hizo zinabaki katika uhalisia wake kwani wataalamu wetu wanafanya kazi hii kwa kuzingatia misingi ya uhaulishaji wa nyaraka.

(b) Mhe. Naibu Spika, kazi ya uhaulishaji wa nyaraka itakapokamilika utawekwa mfumo wa *"ICA Atom"* ambao utatumika kutoa huduma bora kwa watafiti wa ndani na wa nje ya nchi ikiwemo kupatikana huduma za nyaraka katika mfumo wa kieletroniki (*Virtual Archives*). Vile vile kuimarisha ulinzi, usalama na uhai wa nyaraka za taifa kwani watafiti watatumia nakala za nyaraka *(Digitized Archival Documents)* badala ya kuwapa nyaraka halisi (*Original Documents*).

Mhe Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya serikali naomba kuuliza maswali madogo ya nyongeza yenye (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri pamoja na kukiri kuwa kazi hiyo hiajakamilika lakini nataka kujua ni *documents* ngapi mpaka sasa ambazo zimefanyiwa kazi.

(b) Lakini vifaa hivyo vimegharimu shilingi ngapi mpaka kutika katika sehemu husika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, idadi ya *documents* ambazo hadi hivi sasa zimeshakuwa *scanned* na vile vile gharama za vifaa hivyo ambavyo tumevinunua kwa ajili ya kuzi-*scan* hizo *documents*, nimuombe Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae kwamba nitamjibu kwa njia ya maandishi.

Nam. 155

Uwekaji Mbovu wa Vitabu katika Ghala la Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi katika kuendeleza elimu na kufikia kiwango cha juu katika sekta hii kwa kuleta vitabu na vifaa vya kila aina vya kukuza elimu. Lakini bado Pemba katika ghala la elimu la kuhifadhia vitabu, Chake Chake hali imekuwa mbaya na kutothamini juhudi za serikali za kuleta vifaa hivyo na kuviweka katika eneo slisilostahiki.

(a) Je, serikali inalijua hilo.

(b) Ghala hilo la kutunza vitabu limekodiwa na serikali au tumesaidiwa.

(c) Hatuoni hali ile ya ghala ya vitabu kuharibika kwa vitabu ni kulitia hasara taifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 155 lenye sehemu (a), (b), na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi.

Ghala la kuhifadhia vitabu na vifaa vya elimu vya huko Pemba liko karibu na Msikiti wa Chachani. Jengo la ghala hilo ni bovu na halitoshelezi uhifadhi wa vifaa vya elimu vinavyopelekwa Pemba. Pia jengo hilo kwa muda mrefu limekuwa likidaiwa na waumini wa Dini ya Kiislamu wanaotumia Msikiti wa Chachani kuomba warejeshewe kwa ajili ya upanuzi wa Msikiti wa hapo. Baada ya maelezo hayo napenda kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Wizara inafahamu jengo la ghala la huko Pemba ni bovu na juhudi zimechukuliwa kutafuta eneo ujenzi wa ghala la kisasa katika Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro. Ujenzi huo haujaanza kutokana na ukosefu wa fedha.

(b) Vitabu na vifaa hivi sasa vimehifadhiwa katika ghala la muda ambalo lipo mkabala na ghala la sasa limekodiwa na Kamati ya Msikiti wa Chachani kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyetu kwa muda hadi hapo tutakapopata ghala jengine.

(c) Baadhi ya vitabu vilivyoko katika ghala hilo vimesambazwa katika skuli mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya walimu na wanafunzi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe Naibu Spika, nashukuru na nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nipate majibu mawili ya nyongeza ya (a) na (b).

(a) Nataka nimuulize Mheshimiwa ina maana jengo hilo tayari limeshapewa waumini wa Msikiti wa Chachani.

(b) Kama serikali ilikuwa inajua jengo lile ni bovu na kwamba waliamua sasa kulitoa, kwa nini serikali ilikaa muda wote huo bila ya kutatua suala lile na kuendelea kwenda kukodiwa sehemu ambayo haikidhi haja ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Jengo hili ambalo lilikuwa linaombwa na waumini wa Msikiti, limeombwa kwa muda mrefu kidogo na katika kuombwa huko sisi Wizara ya Elimu tukaona kwamba jengo hili tulirejeshe katika wizara inayohusika na nyumba. Kwa miaka iliyopita ilikuwa Wizara ya Ardhi na wizara iliyopo sasa. Kwa hivyo sisi Wizara ya Elimu tumelikabidhi kwa Wizara inayohusika na Ujenzi. Sasa wao wana hatua zao za kuchukua, baada ya kujiridhisha wao wataweza kufanya lolote ama kulikabidhi Msikiti au laa. Lakini pia tumekuwa tukipata ushauri kutoka Ofisi ya Mufti ya kuwapatia watu wa Msikiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye (a) na (b).

Kutokana na uwekaji usioridhisha wa kumbukumbu za vitabu kumejitokeza na tatizo la wizi wa vitabu katika sehemu mbali mbali, tayari kuna kesi za wizi zimeripotiwa Mahkamani. Nataka kuuliza swali langu dogo tu lenye (a) na (b).

(a) Je, ni watuhumiwa wangapi ambao wamefikishwa katika vyombo vya kisheria hadi sasa.

(b) Ni hatua gani ambazo zimechukuliwa katika utaratibu wa kutafuta haki ya urejeshwaji wa vitabu hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake kama ifuatavyo:-

a) Ni kwamba baada ya wizi kutokea uliripotiwa katika Vituo vya Polisi, Polisi wakafanya kazi zao za uchunguzi na upelelezi, wakapeleka jalada katika Ofisi ya *DPP* baadae baada ya kuchunguzwa zaidi ikaonekana kwamba hakuna ushahidi wowote.

b) Kwa hivyo, hakuna mtuhumiwa aliyepelekwa isipokuwa vile vitabu ambavyo vilichukuliwa kama ushahidi vimesharejeshwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa Wizara ya Elimu ina majengo mengi ambayo hayatumiki na mfano hai Skuli ya Birikau ina madarasa matano ambayo mawili kati ya hayo yamezibwa vizuri na yanaweza kuhifadhi vitabu hivyo. Kuna shida gani vitabu hivyo kwenda kuhifadhiwa katika jengo lao kule Skuli ya Birikau na kuepukana na kukodi hapo na vitabu hivyo kuharibika na kuibiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa idhini yako napenda kumjibu Mheshimiwa swali lake kama ifuatavyo:

Hakuna tatizo lolote Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhifadhi au kutumia jengo lolote katika kuhifadhi na tumeshafanya kuhifadhi vitabu katika Skuli ya Mohamed Juma Pindua. Kwa hivyo wakati utapofika wa kutumia skuli hiyo tutaitumia hakuna tatizo lolote.

Nam. 16

Utaratibu wa Kuwasaidia Wakulima wa Kilimo cha Umwagiliaji

Mhe. Hidaya Ali Makame - Alijibu:-

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo kwa maendeleo ya mwanadamu na ili kukiendeleza kilimo. Wizara ya Kilimo inasisitiza zaidi juu ya kilimo cha umwagiliaji ambapo wananchi wanatekeleza wajibu wao kwa kufuata maelekezo ya wizara na wahusika wake (mabwana shamba).

(a) Je, wananchi ambao wanaolima kilimo hicho cha umwagiliaji na kukiacha kilimo cha asili cha kufuata miongo ya mwaka wanapopatwa na

maafa mbali mbali, kama vile mabonde kujaa maji wakati wa masika na mazao kufukiwa na maji na kupotea, wizara huwasaidia vipi.

(b) Je, wananchi hawa ambao wanapatwa na maafa hayo kila mwaka hususan mabonde ya Kizimbani, Mkanyageni, Bubwisudi na Miwani watakuwa na imani gani na kilimo cha umwagiliaji pamoja na kufuata ushauri wa wizara endapo watakuwa hawasaidiwi wanapopatwa na maafa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango (Kny. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi) - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 16 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Wizara ya Kilimo, Maliasli, Mifugo na Uvuvi inatilia mkazo sana kilimo cha umwagiliaji maji na hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba kilimo hicho ndio chenye tija na pia ni mkombozi wa wakulima baada ya kugundua kwamba kilimo cha kutegemea miongo ya mwaka hususan katika wakati ambapo mvua hazipatikani kwa wingi na kwa wakati. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanaathiri sana upatikanaji wa mvua na kusababisha vipindi virefu vya jua kali, pamoja na unyeshaji wa mvua nyingi kwa kipindi kifupi na baadhi ya wakati husababisha mafuriko. Hivyo ni dhahiri kwamba uamuzi wa serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji ni sahihi na wenye maslahi kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Wakulima wote wanaolima katika mabonde ya umwagiliaji maji wanasaidiwa kupatiwa pembejeo kupitia mpango maalum wa ruzuku. Ruzuku hiyo inatolewa kwa mbegu na mbolea na sio tu kwa wakati mabonde yanapoingia maji, bali hutolewa kila mwaka ambapo mkulima hulipa asiliamia 25 tu ya bei ya thamani ya pembejeo na serikali inalipa asilimia 75 ya bei za pembejeo hizo. Katika jitihada hizo za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji aji, serikali kupitia Wizara ya Kilimo inafanya jitihada za makusudi kwa kuwapa vipaumbele wakulima wa umwagiliaji maji kwa kuwapatia pembejeo kwa wakati ikiwa ni mikakati ya kuongeza uzalishaji katika maeneo hayo ambayo yana fursa nzuri ya uzalishaji wa kilimo cha mpunga.

(b) Mhe. Naibu Spika, naomba nimjuilishe Mhe. Mwakilishi kwamba mabonde ya Kizimbani, Miwani na Mkanyageni bado hayajaanza kutumika kwa umwagiliaji na kilimo kinachoendelea katika mabonde hayo ni kilimo cha kutegemea mvua. Aidha, bonde la Bumbwisudi ni miongoni mwa mabonde yanayolimwa kilimo cha umwagiliaji maji.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba sehemu ya bonde hili hutokezea kujaa maji wakati wa mvua kubwa, lakini maji hayo hupungua kwa haraka kutokana na uimarishwaji wa mitaro ya kutolea maji na kuwafanya wakulima kuendelea na kilimo chao. Wizara inawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kusaidia katika kazi za kuwashajihisha wakulima kupitia jumuia zao katika mabonde ili kusaidia usimamizi bora wa miundombinu ya umwagiliaji maji ikiwemo mitaro ya kutolea maji ambayo kwa upande mwengine ndiyo sababu kuu ya kujaa maji katika mabonde hayo.

Mhe. Hidaya Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu lakini pia ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

(a) Mhe Naibu Spika, kweli tunafahamu kwamba hali ya tabia ya nchi ndio inayosababisha mabonde kujaa maji na mitaro kufurika maji kipindi cha mvua kubwa, lakini kama wizara ina jitihada gani ya kukutana na wakulima au wananchi wa mabonde haya ya Kizimbani, Miwani pamoja na Mkanyageni kuwashajihisha kuhusu kilimo hiki cha umwagiliaji maji kwa vile wao bado hawajakuwa na kilimo hicho cha umwagiliaji ili waepukane na hizi hasara wanazozipata kipindi hiki cha mvua kubwa za masika.

(b) Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hawa katika kipindi kama kile cha jua kali endapo mabonde haya yanakuwa yanakauka maji mpaka hata kile kilimo kidogo kidogo ambacho kinahusu labda unyevunyevu tu ule wa maji ndani ya mabonde kukosekana katika kipindi kile cha jua kali. Wizara ina mpango gani wa kuweza kuwasaidia wakulima hawa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Serikali kama nilivyosema wakati natoa jibu la swali mama kupitia Wizara ya Kilimo inajitahidi kujenga katika kila eneo la umwagiliaji maji, mbali ya mitaro ya umwagiliaji maji kunakuwepo na mitaro maalum ya kutolea maji na kazi hizo zote zinafanywa kwa mashirikiano na wakulima wenyewe

kupitia Kamati zao za Kilimo. Lakini Wizara ya Kilimo inafanya juhudi kubwa ya kukutana na wakulima kupitia utaratibu wa elimu kwa wakulima elimu ya ugani lakini kwa kushirikiana na Kamati za Kilimo kama nilivyosema pale awali.

b) Lakini pia Wizara ya Kilimo ina mpango hivi sasa unaandaliwa kutokana na msaada ya wa *Bank Exim* ya Korea ya Kusini ya kutengeneza miundo mbinu yenye hekta elfu moja na mia mbili ambayo italimwa kilimo cha umwagiliaji maji na hatua hiyo itaendelea kadri hali itakavyoruhusu, ili baadae hatimae uwezo wetu ukiruhusu basi eneo lote la hekta elfu nane mia saba hamsini na moja ambazo zinaweza kulimwa kilimo cha umwagiliaji maji ziendelezwe kwa kilimo hicho. Na wakati wa jua kali suala la msingi ni mabadiliko ya tabia ya nchi na kama nilivyosema serikali ina mpango wa kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji kwa kuendeleza mabonde ili yaweze kulima kilimo cha umwangiliaji maji.

Lakini pamoja na hayo kupitia Wizara ya Kilimo ina mbinu nyengine mbadala ya kwanza kushajihisha wakulima, kutumia mbegu zenye kustahamili au mazao yenye kustahamili ukame katika maeneo mbali mbali. Lakini zipo pia taratibu za *drips irrigation* hasa kwa wakulima wa mboga mboga na mazao ya matunda.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii ya leo. Naomba nimuulize Mhe. Waziri wa Fedha lakini sasa hivi kaa kama Waziri wa Kilimo hapo suala (a) na (b).

(a) Kwa sasa hivi wakulima wa umwagiliaji maji kwenye robo moja anatakiwa atoe thalathini elfu kwa ajili ya kulipia umeme. Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hawa wanyonge kupunguziwa angalau bei kama wanavyofidiwa kwenye mbolea.

(b) Ardhi sasa hivi kwa wakulima umwagiliaji kulima Vuli na Masika ardhi imechoka kidogo, lazima tuhakikishe inapa mbolea kwa kile kiwango ambacho kinatakiwa kipatikane. Lakini kwa bahati mbaya kile kiwango au kilo ambazo zinatakiwa zipatikane kwa upungufu inatakiwa haipatikani, polo moja lenye kilo hamsini, unaambiwa mgawane watu wanne na ardhi sasa hivi imechoka. Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mbolea inapatikana kukidhi mahitaji ya wakulima wa umwagiliaji maji.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe.

Masoud Abrahman Masoud swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kama nilivyojibu katika swali mama ni kwamba mkulima anatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano ya bei, na serikali inachangia ruzuku ya asilimia sabini na tano kwa pembejeo zote ikiwemo huduma za matrekta, ikiwemo mbolea na ikiwemo mbegu. Sasa inategemeana na bei ya ile pembejeo yenyewe. Lakini ni asilimia ishirini na tano ndio anayolipa mkulima na hicho ni kiwango kikubwa sana cha ruzuku na naamini mimi nchi chache kama zipo ambazo zinatoa ruzuku ya namna hiyo. Na serikali imefanya hivyo kwa makusudi mazima ya kuwasaidia wakulima wake kwa kuelewa kwamba wakulima ni wanyonge na wanahitaji kusaidiwa ili kuongeza uzalishaji. Kwa hivyo ningemuomba sana Mhe. Masoud Abrahman Masoud akajua kwamba hii zuruku ni zuruku kubwa na serikali imechukua jitihada kubwa ya kuhakikisha kwamba kilimo kinaendelea lakini vile vile na wananchi wetu wakulima ambao ni wanyonge wananufaika kutokana na kilimo hicho.

Lakini ni kweli nikubaliane nae kwamba ardhi yetu imechoka hasa katika baadhi ya maeneo mengine na ndio maana kuna mambo ambayo serikali kupitia Wizara ya Kilimo inawahimiza wakulima ikiwemo maswala ya kutumia mbolea zenyewe lakini pia si mbolea hizi za viwandani tu lakini pia mbolea za samadi, mbolea za asili. Lakini pia kuzungusha mazao ni njia moja ya kusaidia kurutubisha ardhi, mtu analima mbunga akivuna mbunga apande kunde kwa sababu kunde zina uwezo wa ku-*fix nitrogen* katika udongo. Kwa hivyo hilo linafanyika na kadri hali itakavyowezekana basi serikali itaongeza idadi ya upatikanaji mbolea kwa wananchi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kwanza nimpongeze kwa majibu mazuri katika wizara hii na hasa pale alipoonesha sehemu na mpango wa serikali katika eneo hili la umwagiliaji. Lakini kwa kuwa Mhe. Waziri pia alikiri katika majibu yake usahihi wa ubora wa kutumia kilimo hichi cha umwagiliaji.

Naomba nimuulize maswali kama hivi ifufatavyo lakini katika kutumia mpango wa serikali kwa fedha za ndani sio zile ambazo tunasubiri, kwa sababu ule mpango tumeuona miaka mitatu ya bajeti haujakalika.

(a) Je, kwa kupitia hizi fedha za ndani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuna mkakati gani wa serikali kusaidia miundo mbinu ya umwagiliaji kwa wakulima wetu.

(b) Ni sehemu gani za mashamba au mashamba mangapi ambayo hadi sasa serikali imesaidia miundo mbinu, lakini na imesaidia zile mbinu kwa wakulima wetu katika kurejesha hali ya uchumi Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango (Kny: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi): Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Miraji Khamis Mussa swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Kila mwaka Waheshimiwa Wajumbe tunapitisha na katika bajeti na zinakuwepo fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuhudumia miundombinu ya umwagiliaji maji na hata katika bajeti hii tumeshapitisha zipo fedha ambazo zinawekwa maalum kwa ajili ya kuhudumia miundombinu ya umwagiliaji maji. Kwa sasa kwa uwezo wetu zipo takriban hekta baina ya mia saba na mia nane ambazo zinalimwa kilimo cha umwagiliaji maji ambazo zinaendeelezwa miundombinu yake. Sasa hiyo fedha inatengwa kwa ajili ya kuhudumia miundombinu hiyo.

Lakini kama nilivyosema kwamba serikali tayari imetafuta ufadhili kupita Benki ya *Exim* ya Korea ya Kusini na fedha hizi zitapatikana, kwa sababu tuko ndani ya mchakato sasa wa kupata mkandarasi pamoja na mshauri elekezi kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa miundo mbinu ya hekta elfu moja na mia mbili ambayo itakuwa ni hatua kubwa sana ambayo serikali yetu imepiga ya kusaidia wakulima wetu. Kwa sasa tuna hekta baina ya mia saba na mia nane. Lakini tukipata na elfu moja na mbili tutakuwa tumepiga hatua kubwa sana. Kwa hivyo bado tuamini kwamba na hizo fedha ambazo zinapatikana kutoka kwa wafadhili ni fedha za serikali kwa sababu ni mkopo nafuu ambao serikali yetu utaulipa. Kwa hivyo ni fedha zetu.

b) Lakini pia katika suala lake jengine tuna mabonde mengi ambayo hivi sasa yanalimwa kama nilivyosema kwa mfano Kibokwa kuna miundombinu ya umwagiliaji maji Bumbwisudi, Cheju, Mtwango, Kibonde Mzungu na kwa upande wa Pemba vile vile sehemu za Mangwena, Mgelema nako pia kutaendelezwa katika kilimo cha umwagiliaji maji. Kwa hivyo kazi hiyo inafanywa na serikali itachukua hatua zaidi ya kuhakikisha kilimo hichi kinaimarika nchini kadri hali ya uchumi utakavyoimarika.

Nam. 113

Uhaba wa Maji

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Serikali ya Zanzibar inajitahidi kuimarisha suala la maji lakini mpaka leo maji hayo hayatoshelezi kwa matumizi na hayana ubora wa kunywa hali inayosababisha viwanda vya maji kuongezeka.

(a) Je, ni lini sekta ya maji itatosheleza matumizi ya maji Zanzibar.

(b) Je, ni lini maji hayo yatakuwa salama kwa kiwango kinachokubalika kwa matumizi ya kunywa bila matatizo ya afya.

(c) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kuvilinda vyanzo vya maji ambavyo kwa muonekano wa wazi vyanzo hivyo vinapotea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 113 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba bado maji yanayozalishwa hayajaweza kufikia kiwango kinachohitajika kuwatosheleza wananchi wa Zanzibar. Hata hivyo ili kuweza kufanikisha hilo serikali kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na juhudi mbali mbali za kuwapatia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi inayoendelea na kutafutia ufadhili miradi mipya ya maendeleo ambayo itawezesha kutatua matatizo ya maji nchini. Miongoni mwa miradi inayoendelea ni pamoja na mradi wa usambazaji maji na usafi wa mazingira wa Mjini Magharibi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, mradi wa uchimbaji wa visima unaofadhiliwa na Ubalozi wa China (Vijijini), mradi wa uchimbaji wa visima ambao unafadhiliwa na mtawala wa Ras-el –Khaimah wa mijini na vijijini na kwa upande wa miradi mipya ni miradi wa uimarishaji miundo mbinu ya maji Mjini Magharibi unaofadhiliwa na *Exim Bank* ya India pamoja miradi mengine midogo midogo inayotekelezwa kwa nguvu za wananchi na uongozi wa majimbo na kadhalika. Kukamilika kwa miradi hiyo kunatarajiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa kama si kuondosha kabisa upungufu wa maji uliopo.

(b) Naomba kutoa ufafanuzi maji yanayozalishwa na serikali kupitia Mamlaka ya Maji yana ubora na ni salama kwa matumizi ya wanadamu kutokana na uasili wake. Aidha Mamlaka ya Maji ina utaratibu wa kuyapima maji hayo kwa kuangalia wingi na ubora wake na kutibu kwa kuhakikisha usalama wa maji kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

(c) Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na jitihada za kuvilinda vyanzo vya maji kwa kuendelea na uainishaji na upimaji wa maeneo hayo kwa nia ya kuyawekea mipaka maalum na hatimae kuyapatia hati miliki za ardhi, upandaji wa miti, ujenzi wa uzio kwa kadri ya hali ya uwezo inavyoruhusu, sambamba na utoaji wa taaluma kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na mikutano ya wananchi Kishehia juu ya ulinzi na utunzaji wa vyanzo vya maji kwa lengo la kulinda raslimali maji kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina maswali ya nyongeza (a) na (b).

Nimuulize Mheshimiwa kwamba amejibu humu katika hoja yake kwamba maji ambayo yanatoka katika bomba la serikali ni maji safi yana ubora, salama na yana viwango vya *WHO*.

(a) Lakini inakuwaje Wizara ya Afya kutoa tamko kwamba watu wachemshe maji wakati maji yale yana viwango.

(b) Katika barabara ya Fuoni wakati wa ujenzi mabomba mengi yalikatwa sijui kama anafahamu na kama yalikatwa lini atarudisha miundo mbinu hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Tunafahamu kwamba kinga ni bora kulikom tiba, lakini ukweli ni kwamba maji ya kwetu katika uasili wake ni salama, lakini hata hivyo, pia tunatia dawa kwa kiwango ambacho kinasitahiki kwa sababu kutoka katika chanzo hadi kufikia mlaji hapa kati lolote linaweza likawa linatokea na ndio maana tunaweka stahiki cha dawa kusudi wananchi wetu wawe salama kwa maji yale.

Lakini pia inawezekana huko nyumbani baada ya kuyachota yakachafuliwa ndio maana Wizara ya Afya inasisitiza kwamba maji tuyachemsheni.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wananchi wengi wa Zanzibar wanalalamika sana upatikanaji wa maji safi na salama na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetumia fedha nyingi sana katika mradi wa kuendeleza maji Zanzibar, suala langu liko hapa.

(a) Je, serikali haioni kwamba wakati umefika sasa wa kupeleka shughuli za maji katika ugatuzi kama ilivyo suala la elimu na afya ili Halmashauri ziweze kushughulika huko pamoja na Serikali Kuu.

(b) Je, Mhe. Waziri anaweza kulieleza Baraza hili la Wawakilishi ni kiasi gani cha fedha za wafadhili na Serikali za Mapinduzi ya Zanzibar zilizotumika kuanzia mwaka 2000 mpaka 2015 katika maendeleo ya maji na hatua ya mafanikio ya maji.

(c) Ni lini mradi kupitia fedha za India utaanza Zanzibar utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Nataka kujua ni lini ama kwa nini maji yasipelekwe kufanyiwa ugatuzi. Lakini naomba kwamba tukumbuke tulisema wengine tukawa tuna hofu ya kupeka ugatuzi chini kwa hofu ya kwamba ndio kwanza wapya. Sasa serikali imefikia maamuzi ya wizara hizi tatu kupeleka kule tuone mafanikio yake, *inshaallah* baada ya mafanikio mazuri ambayo tunayategemea kidogo kidogo tutakwenda kote katika wizara zote.

(b) Kwamba kiasi gani toka mwaka 2000-2015 ni suala ambalo linataka takwimu basi naomba tu nilichukuwe nitakujibu, lakini niombe zaidi ya siku tatu kusudi tuweke hesabu vizuri na ukizingatia kesho ni Jumapili nitaleta hilo jawabu.

(c) Lakini ni lini miradi itamalizika. Miradi kama nilivyokuwa nimesema kuna mingi lakini zaidi ya ule mkubwa hatua ambazo zimebakia sasa ni

ukusanyaji wa taarifa na uitishaji wa zabuni na kuendeleza. Sasa kila mradi unajitegemea. Kwa hivyo kwa pamoja hatuwezi kusema lini lakini pia tuseme kwamba jitihada za upatikanaji ni endelevu, kwa hivyo haziwezi kukoma siku gani, siku zote serikali itahakikisha kwamba inafanya jitihada za kuwapelekea wananchi wake maji.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kabisa naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwanza nimpongeze kwa maelezo mazuri ya mahitaji ambayo tunayagemea kupata huko mbele tunakokwenda kuondoa tatizo la maji katika mji wetu na nchi yetu kwa jumla.

Lakini kwa kuwa kuna visima mbavyo vimechimbwa katika maeneo mbali mbali kimoja wapo kisima cha Tomondo kinatumika kwa upande wa Tomondo ambao watu wanapata maji na Kwarara maduka sita hawapati maji, wakati zamani walikuwa wanapata.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kulitatua tatizo hili.

(b) Kwa kuwa kuna mfanyakazi ambaye alalamikiwa sana analeta matatizo hayo katika maeneo hayo kuyafunga maji kwa makusudi. Wizara kushirikiana na mimi Mwakilishi itakuwa tayari kwenda kumuondoa mtu huyo ili aondoshwe aletwe mwengine kwa kuondoa tatizo hili la maji na kuwa wanapatikana pande zote. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

a) Ni kwamba wizara iko tayari kufuatana naye kwenda kubaini tatizo ni nini kinasababisha kwamba wananchi hawa hawapati maji ili hali kisima kipo.

b) Pia tupo tayari kubaini kuona nani anafanya hivyo na kwa sababu gani, inawezekana ikawa ni shutuma au kuna ukweli. Sasa cha kwanza tutafute ukweli kabla hatujamuonea mtu. Lakini pia tukisema kwamba kama hapa ulivyokuwa umelizungumza inawezekana akajirekebisha. Lakini niombe sasa kwa maeneo yale ambayo kuna watu wenye tabia kama hiyo, basi tuambizane siri kusudi tutafute ukweli siri tukichukua hatua basi tuchukuwe hatua kwa mujibu wa ukweli ambao tumeubaini. Inawezekana wakati mwengine kuna

stofahamu kati ya watu na watu, kila mmoja binadamu inawezekana ukweli na inawezekana sio kweli.

Lakini watu wanasema lisemwalo lipo kama halipo linakuja. Sasa sisi tusilingoje mpaka likafika, tayari wizara yetu itashirikiana na Mwakilishi na mwanamke yeyote raia mwema ili kuona kwamba tunaondoa vile vipingamizi vya aina yoyote ambavyo vinatupelekea tusiyapate maji kwa uhakika.

Nam. 44

Utaratibu wa Upasishwaji wa Vyombo vya Moto

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuanzisha Idara ya Usafirishaji na Ukaguzi wa Magari na Vyombo vyengine vya Moto, Hata hivyo, kumekuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaohitaji huduma katika Idara hiyo pale Karakana ambapo mtaka huduma hulazimika kwenda Karakana na kwenda kufanya malipo benki na kisha kurejea tena Karakana.

(a) Je, hatuoni kama tunaongeza usumbufu katika utoaji wa huduma hizo

(b) Ni sababu zipi zilizofanya ishindikane kuweka mfanyakazi wa *PBZ* pale Karakana kwa kukusanya mapato ya huduma hizo ili kuondoa usumbufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 lenye
kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuanzia tarehe 1 Machi 2017 Wizara yangu ilitakiwa kuwataka wananchi walipe malipo
yao ya huduma hizo kwa kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*).

(a) Faida inayopatikana ni kubwa zaidi kuliko usumbufu unaopatikana.

(b) Utaratibu umeanza na changamoto tunakubali na kila zinapoendelea kujitokeza na sisi huwa tunakabiliana na changamoto hizo ili tuhakikishe kwamba usumbufu huo unaondoka.

Kwa hivyo usumbufu huo tutakuwa tunaendelea kuuondosha mmoja baada ya mmoja kwa wale wote wanaopata kutumia hiyo benki. Vile vile tutaangalia uwezekano wa kulipia kwa kutumia simu za mkononi hapo baadae.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza
swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Ni kweli utaratibu wa kulipa benki ni mzuri kuweza kudhibiti mapato ya serikali. Tumeona taasisi kama *TRA* kwamba wamewaweka watu wa benki pale ili kukusanya mapato yao.

Je, wizara yako kwa kupitia idara yako ina mpango gani wa kuweka ki-*sub bank* pale cha kukusanya mapato yale ili kuondoa usumbufu, ukiangalia masafa kutoka Karakani kuja benki mbali mbali ya Mwanakwerekwe na sehemu nyengine.

b) Kama utaratibu wa simu utaanza bila ya majibu ya kisiasa, ni lini utaratibu huu utaanza ili kuweza watu kuwaondoshea usumbufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kama tunavyojua kuanzisha huduma hizi za benki zina taratibu zake na sio taratibu ndogo na ni karibuni tu Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alitoa maelezo alipoulizwa kuhusu kwa nini Wilaya nyengine hazina matawi ya benki.

Kwa hivyo, ni mchakato ambao unahitaji muda na iwapo ingekuwa inawezekana kufanya kwa kipindi hiki ningefanya. Ndio maana nasema kwamba tumeamua kuangalia huu mchakato wa kutumia simu kulipia baada ya kufanya mawasiliano na Wizara ya Fedha na Mipango na kusema lini tutaanza. Kama nilivyosema mwanzo, sisi tunatoa majibu ya uhakika kwamba huu ni utaratibu unataka uangalifu ili baadae usije ukaleta malalamiko kwa wananchi kwamba wanaibiwa pesa zao au pesa zao hazifiki sehemu husika.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza.

Kwa sababu mfumo wa *e-payment* umeenea duniani na hapa kwetu Zanzibar tayari umeshafanyakazi. Je, ni sababu zipi zinazoifanya wizara isiweze ku-*motivate e-payment* na kuweka kwenye vituo ili wananchi iwe rahisi kupata huduma ile badala ya kwenda kuweka msongo mkubwa na usio na manufaa katika idara yake ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumuarifu kwamba kama nilivyosema hapo mwanzo, kwamba taratibu hizi zinafuata taratibu maalum za kifedha.

Kwa hivyo ili kujihakikishia kwamba mapato yanayopatikana hayapotei bora tuanze na usumbufu lakini tuna utaratibu huo na utakapokuwa tayari huo utaratibu, sisi tuko tayari kuwaondolea wananchi wetu usumbufu. Kwa hivyo tunawaomba watustahamilie, kwa sababu hata hayo mambo ya e-*payment* yana umuhimu wake kama tunavyosema na sisi ndio wahusika wakuu, lakini atupe muda ikiwa tayari tutasema. Lakini siwezi kusema kama lini na kwa haraka gani tutafanya, lakini tuko katika huo mchakato.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye kipengele (a) na (b).

Kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini naipongeza pia serikali kwa kupitia idara hii kwa hatua ya mabadiliko ya mfumo huu wa malipo ya benki. Inasemekana kabla ya mchakato huu wa kubadilisha mfumo huu kulikuwa kunakadhia ya upotevu wa mapato.

a) Je, ni kweli kulikuwa na tatizo hilo.

b) Kama ni kweli wahusika walioshiriki kupoteza mapato ya serikali wamechukuliwa hatua gani hadi hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ni kweli kama ulivyosema mwanzo watu walikuwa wanatumia njia za panya hata wengine wakawa wanatumia leseni *fake* na baadhi ya zile taratibu kama Bima *fake*. Kwa hivyo kusema ukweli hapo ndipo yalipokuwa mapato yanapotea. Lakini kwa sasa hivi kwa kushirikiana vizuri na Jeshi la polisi na watu wa *ZRB* tumehakikisha kwamba malipo yanapokwenda benki,

tunamjua nani ana leseni sahihi na nani amelipia vifungu vyote vile vinavyohusiana na mapato yetu kwa kupitia benki. Kwa hivyo hii imesaidia sana.

b) Kuhusu hawa watu waliokuwa wamehusika katika mambo hayo. Kwa taarifa ya Jeshi la Polisi lilitoa ufafanuzi na hao watu wamechukuliwa kadhia kwa kupelekwa katika vyombo vinavyohusika vya Mahakama. Kwa hivyo nina imani kubwa sana utaratibu wa kesi inavyoendelea upo Mahakamani.

Nam. 143

Kutotumika Barabara za Ndani

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini - Aliuliza:-

Kwa miaka mingi ya nyuma barabara kuanzia Forodhani kupitia jengo la Wizara ya Kilimo la zamani kwendea Kiponda na kutokezea Darajani kwa Muzamil ilikuwa inatumika kwa gari ndogo. Pia barabara itokayo Msikiti wa Ijumaa Malindi kupitia jengo lililokuwa la Wizara ya Mawasiliano Jamatini hadi Darajani ilikuwa nayo ikitumika.

(a) Ni sababu zipi za msingi zilizopelekea barabara hizo kutotumika hivi sasa.

(b) Je, Wizara haioni kama barabara hizo zikitumika baada ya matengenezo zitatanzua tatizo la msongomano wa gari liliopo hivi sasa hapo Malindi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 143 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba barabara hizo zilikuwa zikitumika. Hata hivyo, wizara ilichukua uwamuzi wa kuzifunga barabara hizo kutokana na kupunguza wimbi la magari katika eneo la Hifadhi ya Mji Mkongwe na kuzifanya *one way*.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuziruhusu njia hizo kutumika kutaweza kuongezeka idadi ya magari katika maeneo hayo ya Hifadhi ya Mji Mkongwe ambayo kwa kiasi kikubwa yamekuwa yakichangia kuharibu haiba ya mji huo.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, naomba nimuulize swali langu la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, utafiti mdogo nilioufanya nimebaini kwamba kiukweli moja ya ile njia hivi sasa kutoka Msikiti wa Ijumaa Malindi kupitia Wizara ya Mawasiliano ya zamani Jamatini mpaka Darajani hivi sasa inatumika, tena gari zinapita *two way*, zamani ilikuwa *one way* unateremka tu. Lakini sasa unakwenda *both way*. Kwa hivyo imesababisha magari mengi zaidi kupita katika Mji Mkongwe.

a) Je, hiyo dhana aliyosema Mhe. Naibu Waziri ya kuzuwia gari zisipite, ile haiba ya Mji Mkongwe iwepo, bado *concept* hiyo ipo.

b) Lini wizara yake itasimamia ukarabati wa mashimo mengi yalioko njia hiyo ili hayo magari yaweze kupita vizuri zaidi ku-*reduce* msongamano ulioko njia ya Malindi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, kama tunavyosema kazi ya kuchukua sheria ni kazi ya Jeshi letu la Polisi. Kwa hivyo sisi tutaendelea kuwahimiza Jeshi la Polisi waendelee kusimamia hizi sheria tulizoziweka.

Kweli mimi ninakiri kwamba kuna baadhi ya wakati watu huamua kukwepa hizi sheria. Lakini kama nilivyosema sheria zitachukua mkondo wake na wale wote watakaoonekana wanavunja sheria hizi, basi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

b) Mhe. Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa zile barabara, kama nilivyosema tulipokuwa tukijibu masuala yetu ya bajeti hivi juzi, ni kwamba sisi tumeweka mpango wa kufanya ukarabati maeneo tofauti na nina imani kubwa sana katika huo ukarabati tutakaofanya basi na Mji Mkongwe vile vile tutauangalia ili kuendelea kuipa haiba mji ule.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kwa Mhe. Naibu Waziri.

a) Kwa kuwa wananchi wengi wa Mji Mkongwe wana magari mengi na sehemu za ku-*park* gari ni ngumu sana kwao na ni tabu kutafuta sehemu za ku-*park* gari na usalama wao. Je, wizara yako imejipanga vipi kujenga eneo katika eneo lolote la Mji Mkongwe *parking* maalum za ghorofa kwa ajili ya wananchi wa Mji Mkongwe na wakaweza kulipa kwa mwezi.

b) Kwa kuwa mna lengo la kupunguza magari Mji Mkongwe. Je, ni lini sasa wizara yako itapiga marufuku magari yote, halafu wakaruhusu baadhi ya gari maalum kwa vibali na kuweka nyinyi wenyewe wizara basi maalum ambazo kama wanazoweka nchi za wenzetu za Ulaya ambazo zitaweza kupita Mji Mkongwe na watu kulipia kama dala dala, lakini zikawa basi nzuri na za kisasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Ni kweli tunajua kwamba tuna msongamano na nina imani kubwa sana mradi wa Darajani *Corridor* utakapomalizika basi tatizo la *parking* litaondoka sana. Vile vile tutataka kufanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba Mji Mkongwe kunaingia gari maalum. Hivi sasa tumeshaanza utaratibu gari tunazoziruhusu kuingia ndani ya Mji Mkongwe zisizidi tani mbili. Sasa kama kuna watu wanaruhusika kupitisha gari nyengine ni kwa kazi maalum.

Kwa mfano, gari za fire na gari ambazo zinaomba kibali maalum kupitia kwetu. Kwa hivyo sisi tutaendelea kusimamia hili ili kuhakikisha kwamba Mji wetu Mkongwe unaendelea kuwa katika Uhifadhi na Uendelezaji wa Miji ya historia duniani.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Waziri kwa vile wewe ni Mwakilishi kutoka Jimbo la Malindi na Jimbo la Malindi liko Mji Mkongwe, na gari nyingi ni za wanyonge zinazokwenda katika bandari ya Zanzibar na zinapakia mbatata, ma-*cabbages*, pilipili na kadhalika, na kule ndio kunako maisha yao.

Je, huu utaratibu wa kuwapa vibali hamuoni kama mtawasumbua watu. Ni lini mtatoa elimu ili kuwaelimisha wananchi wenye magari yale, ukizingatia bandari iko katika eneo la Mji Mkongwe kama kuna mpango huo.

Lakini vile vile kama wewe ni Mwakilishi wao umechukua hatua gani ya kuwatetea ili wananchi hao wanyonge wasijekupata usumbufu huo, ikiwa kama wapiga kura wako.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema hapo mwanzo tumetoa vibali maalum kwa kupitia Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kwa wananchi wanaoishi katika Jimbo la Mji Mkongwe, hata kuweka magari yao na vile vile kuingiza gari zao.

Lakini kama ulivyosema pale ambapo wanakuwa na mizigo basi sisi huwa tunatoa vibali maalum. Nina imani kwamba wenyewe baada ya kukaa nao wamechukulia kwamba na ule mji wao ni mji ambao uko katika uridhi wa kihistoria. Kwa hivyo na wao wanataka uhifadhi, kwa hivyo wamekuwa tayari kuzifuata zile taratibu. Sisi kupitia Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe tutaendelea kutoa elimu kwa wananchi wetu ili wao watuelewe nini nia yetu, na kwamba sisi hatukusudii kuwakomoa wananchi, bali tunataka waendelee zaidi na vile vile ule mji uendelee kutuingizia pesa nyingi kwa kupitia kwa watalii.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, nasimama kwa heshima kabisa katika Baraza lako tukufu kwa kutumia Kanuni ya 63, lakini pia naiunganisha na Kanuni ya 37(3)(vii) ambayo inasema:

37(3)(vii)

"Swali linalohusu jambo lolote katika yafuatayo halitoulizwa au kujibiwa katika Baraza:-"

kama inahitaji habari ambazo zinapatikana katika hati ambazo Mjumbe anaweza kujisomea, kama vile nakala za sheria au maandishi ya kumbukumbu za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakubali kwamba muhusika mwenye swali hili kwanza simuoni katika Baraza. Lakini napata hofu sana katika swali hili juu ya maswali ya nyongeza ambayo yatakayofuata.

Mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwa kutumia busara na hekma swali hili lirudi likakarabatiwe zaidi na ikiwezekana au kama litakupendeza basi utumie Kanuni zako ambazo zinakuruhusu ili kuleta umoja wetu na swali hili uliondowe katika Orodha ya Shughuli za Leo. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe nafahamu sana *concern* yako lakini swali limeshafika katika *Order Paper*.

Nataka tukubali na nafikiria kuna majibu yake mazuri ya kulijibu swali hili. Kwa hivyo tutamuachia Waziri atalijibu swali hilo ingawa mwenyewe hayupo hapa simuoni ambaye ameuliza na ambaye atajibu kwa niaba. Kwa hivyo naomba tuendelee. Nimesikia *concern* yako lakini naomba tuendelee suala hili.

Nam. 119

Utaratibu wa Ajira Kwa Unguja na Pemba

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondosha)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante mheshimiwa umeomba litolewe. Haya kwa hivyo tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2017/2018 - Wizara ya Afya

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Nimepata vikaratasi vingi kila mtu anataka kuchangia mwanzo, lakini mimi nitafuata utaratibu uliokuwepo hapa na kila mmoja wenu ana sababu nzito tu. Kwa hivyo ningemuomba sasa hivi aanze na Mhe. Abdalla Maulid Diwani, akimaliza atafuata Mhe. Suleiman Sarahan Said. Karibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kusimamia utaratibu katika hilo nakupongeza sana.

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima tukaweza kukutana Jumamosi ya leo katika kazi zetu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo niende moja kwa moja kwenye harakati zangu za uchangiaji hotuba ya Wizara ya Afya. Awali ya yote napenda sana kumpongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa azma kamili ya kuona kwamba Wizara ya Afya ni kweli kimbilio la Wazanzibari wanyonge na wakulima wa nchi hii, kwa kusimamia ujenzi wa vituo, kusimamia huduma za afya katika nchi hii. Ninampongeza sana Mhe. Rais.

Lakini vile vile kwa dhati kabisa katika ukumbi huu napenda kuipongeza Hospitali ya *Global* ni juzi tu iliweza kupima wagonjwa wapato 100 matatizo ya kipimo cha *echo* ili watu wale waende wakapate matibabu nchini India. Cha kusikitisha Mhe. Waziri kasoma hotuba yake mpaka kamaliza alishindwa kuwapongeza, mfanya biashara yule mwenye hospitali kasamehe zaidi ya milioni kumi kwa sababu kila kimo pale ni laki moja. Kwa hivyo alithubutu kusamehe shilingi milioni 10 kuwapima vijana wale bure ili kuisaidia Serikali yake ili iwe mchango katika Serikali hii.

Vile vile nikiendelea mbele naingia katika kitabu changu nachangia ukurasa wa 15 "Huduma za Afya ya Uzazi na Watoto". Ninakwenda katika ubeti wa 35 naomba ninukuu Mhe. Naibu Spika.

"Mhe. Spika, vifo vya mama wajawazoto bado ni tatizo katika jamii yetu ambayo jumla ya vifo 27 vimeripotiwa katika hospitali yaUnguja 12 na Pemba 15 katika kipindi cha mwaka 2016/2017, hata hivyo idadi hiyo inaonekana pungufu ukilinganisha kipindi kifupi….

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe naona kelele zimezidi ili tumsikie mchangiaji na Waziri aweze kumsikia naomba sana tuwe watulivu, ahsante endelea Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: ukilinganisha kipindi hichi kinaonekana idadi pungufu ukilinganisha na kipindi kama hichi kwa mwaka wa fedha 2015/2016".

Ni kweli tupongeze katika hicho lakini bado hatujamaliza ile robo ya mwisho tukajua ni idadi gani. Lakini katika humu hamna vifo vya watoto. Je, tumekuwa sasa hivi *alhamdulillahi* tumeweza kudhibiti vifo vya watoto wachanga, kwa sababu ilitakiwa kama vifo vya akinamama wajawazito wanapojifungua wanapata matatizo, basi mategemeo yangu mimi sio daktari lakini navisikia au tunaviona vifo vya watoto vinavyotokezea lakini katika kitabu hichi hamna. Ningeomba sana Mhe. Waziri atakapokuja pengine amepitikiwa au namna gani

atueleze. Je, tumeweza kuokoa vifo vingapi vya watoto kutoka ngapi mwanzo tulikuwa tunapata 2015/2016 na 2016/2017 tunapata vifo vingapi, nilitaka niseme hilo.

Lakini vile vile niende katika Kitengo cha Damu Salama. Kwanza nimpongeze sana…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Abdalla Maulid Diwani naomba kidogo ukae ninamwachia sasa Mwenyekiti aje kwa ajili ya kuendelea na shughuli hizi.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tuendele Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu katika huduma ya mpango damu salama ubeti wa 99. Ni kweli nipongeze kabisa kwa dhati ya moyo wangu Idara hii ya mpango wa damu salama kwa juhudi zao za dhati kabisa kupambana ili kuona upungufu wa damu katika visiwa vyetu hivi inakuwa historia. Nathubutu kutamka mbele ya Baraza lako tukufu mimi ni mmoja wa mabalozi waliochangia damu Zanzibar. Nafasi hii nimeipata kutoka kwa Mhe. Mahamoud kuona mchango wangu jinsi namna gani ninavyopambana katika suali hili.

Hivi juzi tu tulikuwa na mpango wa kukusanya damu katika Mikoa yote ya Unguja na tumefanikiwa, lakini kuna malalamiko ya wafanyakazi katika Kitengo kile hawatoshi, ni tatizo kubwa sana imepelekea hadi kuazima wanafunzi wa Chuo cha Afya Mbweni ili waweze kusaidiana nao angalau kuweza kukidhi mahitaji ya wakati ule, watu wako tayari kujitolea damu lakini kuna uhaba wa wafanyakazi katika Kitengo kile. Ningeomba sana Mhe. Waziri katika hilo uliangalie kwa dhati kabisa kama unavyofahamu kwamba damu ni muhimu, asiyekuwa na damu sawa sawa na sanamu, damu haina kiwanda duniani. Kiwanda cha damu ni mwanadamu. Ningekuomba sana kwa wale wananchi ambao walikwenda kujitolea kwenda kutoa damu wasisumbuke na hawatosumbuka ikiwa watakuwa na wafanyakazi wa kutosha katika kitengo kile.

Lakini vile vile nikiendelea hapo hapo kuna tatizo jengine la upatikanaji wa vifaa, vitenganishi vya damu hata vya kuhifadhia damu ni tatizo, imekuwa mpaka vinamalizika kabisa inakuwa ziro tena tunahangaika tukaazime wapi sio lengo. Ninajua serikali yangu sikivu sana katika hilo inafahamu dhima kamili ya Wizara ya Afya kwa kuweka Kitengo kile cha Damu Salama. Tunaweza

kuokoa maisha ya watu kila mara hususan mama wajawazito kwa upande wa kujifungua na ajali zinazotokea mara kwa mara watu wanahitaji damu, na kama itafika wakati tuzikosa vile vitenganishi vya damu na vifaa vya kuwekea damu, nafikiri sijui kama tutawatendea haki kwa Wazanzibari. Ningekuomba sana Mheshimiwa katika hilo ulingalie kwa dhati kabisa ili kuona kwamba tatizo la vifaa na vitenganishi vya damu vinaondoka kuweza kufanya kazi hiyo.

Lakini sio hiyo tu vile vile hata yale mahitaji yao wale wafanyakazi kule yanachelewa kupata ndani ya muda, inakuwa ni shida. Ninafikiri hata posho yao wanayopewa pale milioni mbili kwa mwezi ni pesa kidogo na watendaji wanashindwa hata kupata mafuta kwenda kuzifuata hizo damu katika sehemu nyengine. Ningekuomba sana Mheshimiwa katika hicho tulifanya kikao na wewe ulikuwa shahidi pale na ukaahidi kwamba utalivalia njuga suala lile ili kuona kwamba Kitengo kile kinafanya kazi zake salama. Bado kuna changamoto ya upatikanaji wa fedha katika shughuli nzima za kukusanya damu ili uweze kutia gari mafuta kwenda katika sehemu zao husika.

Lakini vile vile nikiendelea mbele katika suala hilo hilo la damu nikupongeze sana Mhe. Waziri kwa dhati ya moyo wangu kwamba tulipiga kelele kuwa gari bovu. Lakini kwa taarifa yako gari nimeliona lipo gereji sasa hivi linaanza ukarabati hongera kwa hilo, mnyonge mnyongeni na haki yake mpeni. Mhe. Waziri umefanya kazi kubwa sana kuona lile gari la Benki ya Damu leo hii lipo gereji pale kwa Buda linaanza utaratibu wa kutengenezwa, hongera Mheshimiwa, ijapokuwa una changamoto nyingi lakini nikupe hongera kwa sababu nilikwambia tukaelezana ikafika wakati kwamba umetekeleza, huo ndio uongozi, nakusifu sana Mhe. Waziri nakupa pongezi sana katika hilo kutekeleza kwa wajibu wako ipasavyo.(*Makofi*).

Nikiendelea mbele vile vile nakwenda katika suala zima la Bodi ya Madawa, Chakula na Vipodozi. Niipongeze sana taasisi hii inafanya kazi vizuri na hata hivi karibuni sote tulikuwa mashahidi, lilitokea zoezi zima la kuziratibu machinjio zetu hapa Zanzibar, ikawa kuna tatizo kubwa sana lakini watu wakaweza kuelimishwa wakakaa mpaka wakaelimika kuona kwamba lile tatizo sasa hivi limeondoka mpaka dakika hii kuna machinjio matatu yanafanya kazi Zanzibar, mazuri kabisa, masafi kila mtu anaridhika, hata uchukuaji wa nyama, magari yale yako vizuri, tumeondoa lile tatizo la kuchukua nyama kwenye vespa ambayo hata ile *hygienically system* haikubali. Nashukuru sana Mheshimiwa kwa hilo umesimamia na nampongeza sana Mkurugenzi wa pale wa Bodi ya Madawa, Chakula na Vipodozi.

Lakini vile vile kuna changamoto nyengine ambayo nakuomba sana Mheshimiwa uiangalie. Kuna uhaba wa usafiri pale kama unavyofahamu kwamba wana kitengo chao kimoja kipo bandarini, wanasumbuka sana katika harakati za kukusanya *sample* kupeleka kwenye taasisi yao kuzifanyia vipimo na kurudisha *sample* na kuwaruhusu wafanya biashara kupata bidhaa zao ndani ya muda. Ningekuomba sana Mheshimiwa uangalie, wale mpaka dakika hii wana gari mbili. Gari mbili ni kidogo kwa taasisi kama ile ambayo tumeipa meno makubwa sana sasa hivi kukamata kila pahali. Ningekuomba uwaangalie kwa moyo mkunjufu kabisa kuweza kuwapatia magari ili kuona wanafanya shughuli zao vizuri.

Vile vile kuna tatizo la utoaji wa leseni ya duka la madawa. Duka la madawa linakuwa na leseni mbili. Leseni moja ya Manispaa au Halmshauri husika na leseni ya pili kutoka *ZSTB,* kulikoni kuna leseni mbili pale katika duka moja ambayo mfanya biashara anatakiwa alipe laki na nusu kwenye Manispaa, alipe laki na nusu kwenye Bodi ya Dawa, Chakula na Vipodozi. Ningekuomba sana Mheshimiwa hilo uliweke sawa ili kuondoa sitofahamu ya wafanyabiashara kuona kwamba wananyonyeka zaidi kuliko wafanya biashara wengine ambao wao lengo lao kubwa pamoja na biashara, lakini kuwatunzia mahitaji ya wananchi katika suala zima la kupata dawa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikienda mbele vile vile katik hiyo Bodi ya Madawa, sasa hivi kumejitokeza madaktari wengi na sijui ni madaktari au waganga wa asilia ni wengi ambao wana vituo unakwenda kwake anakukamatatisha kifaa tu mkononi kwenye kompyuta yake anasoma anakuagulia maradhi. Je. Mhe. Waziri hichi kifaa kama wewe kwa upande wa sekta ya afya kinakubalika. Mimi najua maradhi kwa kukamata kile kifaa, mimi akili yangu ndogo au elimu yangu ndogo sidhani kama unaweza kuona maradhi, lakini pale panaandikwa maradhi mengi. Najua maradhi yanaangaliwa kwenye choo kikubwa, choo kidogo kwenye damu utapigwa *E-ray* na *CT scan,* kukamata kile kifaa tu mkononi, halafu mtu ukaambiwa maradhi kidogo mimi napata shaka katika hilo. Ningeomba Mhe. Waziri katika hilo ulisemee ili watu wetu wanaotusikiliza wajue ile ni *official* imekubalika kabisa na Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya shughuli zile.

Sio hilo tu sasa hivi kumetokea wauzaji wa dawa wasio rasmi katika Misikiti yetu kila siku ya Sala ya Ijumaa, utakuta kila siku pale dawa zinauzwa, mpaka kuna dawa unaambiwa ya kuweka heshima nyumbani, tena watu wanamiminika kununua zile dawa. Je, zile dawa zina ubora gani, zina viwango vilivyokubalika. Ninajua Bodi ya Madawa kazi yao ni hiyo na wanakutana nazo dawa mbali mbali za kunywa, kujipaka na kukorogea kwenye kwenye uji.

Ningeomba sana Mhe. Waziri katika hili uje kunipa ufafanuzi ili kuweza kuwaokoa watu wetu wasiendelee tu kupewa madawa ambayo hayana viwango au nini.

Nikiendelea mbele katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri sijaona katika kitabu chako chote nilichopitia humu juu ya suala zima la uboreshaji wa kituo cha Umbuji. Kituo hichi Mhe. Mohammedraza alikipigia zogo sana katika bajeti iliyopita na hadi hii leo bado hakijatengenezwa.Tatizo nini. Ningekuomba sana Mheshimiwa suala la kituo cha Afya cha Umbuji ambacho kimekuwa kibovu kinavuja, hakina hadhi kuwa kituo cha afya ambayo Mwakilishi mwenyewe alijitolea kwamba akijenge, lakini mkasema kwamba mna mradi mtakijenga hadi hii leo bado muda umeshakuwa mwingi. Ningeomba katika hilo Mhe. Waziri uje unipe maelekezo kulikoni. Bajeti iliyopita tulikiombea lakini hakijakuwa lakini mkasema hichi kituo ipo program inakuja ya kuboresha hivi vituo kitakwenda kushughulikiwa. Ningeomba sana katika hilo.

Nikiendelea mbele vile vile nitoe shukurani nimekuta hapa kitu kimoja ambacho kimenifurahisha, juu ya utayarishaji wa huduma za bima ya afya kwa wananchi wa Zanzibar. Nikupongeze sana, mimi ni muumini mkubwa sana wa taasisi hii kwa sababu hata jimboni kwangu mimi nimefanya na sasa hivi nakuja kwenye mpango mzima wa Serikali, hongera sana na inshaallah nia njema siku zote basi inakuwa na baraka ndani yake.

Sasa niende moja kwa moja katika kadhia ya Wazanzibari, niende katika program ya HP02 kwa "Hospitali ya Mnazi Mmoja". Mhe. Mwenyekiti, nimesema hayo kwa sababu nina imani kwamba kila Mwakilishi atakayesimama hapa nina imani kwa namna moja au nyengine kwa uzuri au kwa ubaya ataizungumzia Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini mengi ni kwa ubaya si kwa uzuri. Mhe. Waziri najua unajitahidi sana katika hilo lakini nasikitika kwamba natamka kwa dhati ya moyo wangu kwamba wasaidizi wako wa Hospitali ya Mnazi Mmoja wanakuangusha. Nina imani hiyo kwa sababu ninaona jitihada zako na mimi ni mdau kila mara kwenda kupekura pekura kule Hospitali ya Mnazi Mmoja, nakuta changamoto mbali mbali lakini majibu naambiwa lishamalizika hilo bado halijafanywa.

Kuna masikitiko kuna jenereta pale tumepewa na *UNWFPA,* hii leo kufika pale jenereta ni miezi minne na siku kumi na saba, linahitaji dola 5,000 au 6,000 hivi ili waweze kulitumia jenereta lile pale. Juzi wamekufa watu kwa kukosa umeme ghafla tu Hospitali ya Mnazi Mmoja jenereta limekaa pale eti kwa Dola elfu saba. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba hata hiyo *guarantee*

warrant itaishia pale pale, haiwezekani jenereta lile limeweza kukaa pale leo hii miezi minne na siku kumi na saba halijafungwa, utwambie je, hakuna sehemu ya kufungia. Hospitali ya Mnazi Mmoja hakuna eneo lililowekwa kwa ajili ya kuweka jenereta na hakuna pesa hizo Dola elfu saba ni milioni kumi na nne *maximum* na kama halijafungwa kwa sababu gani. Mhe. Waziri najua kila siku unapishana mawinguni, leo Geneva, kesho wapi tunashindwaje …

UTARATIBU

Mhe. Mweyekiti: Kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 63

Mhe. Mwenyekiti: Kanuni ya 63 imekuruhusu wewe usimame kuhusu utaratibu taja kifungu abacho kanuni imekuruhusu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu kanuni ya 63 kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu utaratibu Kanuni ya 63 Mhe. Jaku imekuruhusu wewe useme unasimama kwa Kanuni ya 63 halafu utaje Kanuni iliyovunjwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kifungu cha 59(3) nisome au utaiangalia**.**

Mhe. Mwenyekiti: Isome.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani, atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu, na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika".

Nimuombe tu Ndugu yangu Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa nia njema, lile jenereta halihitaji hata Dola efu tano pale kazi iliyokuwepo, kama milioni tatu au milioni nne kujenga sakafu tu kuliweka. Kwa hivyo hizo pesa alizozitaja ni nyingi na tunapoteza wananchi wetu huko. Aseme tu milioni tatu au nne, hizo Dola efu tano milioni kumi na hazifiki gharama. Huu ni uzembe wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naendelea. Mhe. Waziri hakuna sehemu inayoitia doa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

kama Hospitali ya Mnazi Mmoja. Malalamiko mengi, najua wenzetu alhamdulillahi huko mbele mnapopata matatizo tu, ninajua mtakwenda India, China, mtakwenda wapi lakini mwisho wa siku, sisi sote basi "buno kusini". Lakini pamoja na hayo, tuwaonee huruma hao wenzetu wengine wanaotumia hospitali ile pale.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, utakwenda pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, leo hii imani yangu kwamba Serikali ni tajiri kuliko mtu binafsi, kuna vipimo Mnazi Mmoja unalazimishwa lazima ukapime Al-Rahma, ukapime Hospitali ya Global, tunashinwa vipimo na kama vipo kwa nini havipimwi pale na kama vilikuwepo vimeharibiwa kwa nini viharibiwe. Mhe. Mwenyekiti, imani yangu kwamba vipimo pale vipo lakini kwa *sabotage* za makusudi, ninavyoona mimi inapelekea vipimo vile kuharibiwa ili watu wapate kujinufaisha katika hospitali zao binafsi. Mhe. Waziri nakuomba sana katika hilo uwe mkali. Ninajua Hospitali ya Mnazi Mmoja ina Bodi yake, ina wakaguzi wake na kila kitu, lakini una haja na wewe kama msimamizi kulisemea, wanakuharibu Mhe. Waziri, ifike wakati hata uchafu basi iwe shida Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, tumekwenda na Wajumbe wanzangu karibuni 27 Hospitali ya Mnazi Mmoja utaona aibu. Jengo jipya Mhe. Rais kalifungua jengo lile halijafika hata mwaka mmoja na nusu. Leo hii kuna msitu unataka ufuge simba basi kusafisha tu mpaka tupate mtaalamu. Mhe. Waziri inasikitisha sana, Bodi yako ya Hositali ya Mnazi Mmoja au pengine uongozi wa Hospitali yako ya Mnazi Mmoja unasikitisha.

Mhe. Mwenyekiti, na pengine akili yangu inaniambia kwamba kuna watu hawaungi mkono hayo Mapinduzi ya Zanzibar wanatuharibia. Mhe. Waziri ningekuomba sana uwe na meno katika hilo kwa sababu Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kimbilio la Wazanzibari wa nchi hii hawana kwengine, hakuna hospitali nyengine yoyote hapa utakayokwenda katika kisiwa hichi kwa wanyonge wetu watakwenda pale, wenye uwezo kidogo Alhamdulillahi watakimbilia Hospitali ya Global, wengine Mawaziri mtakwenda India, China, Afrika ya Kusini, lakini sisi wanyonge tutakimbilia wapi. Tunaomba ile hospitali jamani tunasema angalau iwe katika hali kidogo ya kuridhisha.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, si hilo tu suala jengine la walinzi wa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja ni matatizo. Wezangu walizungumza hapa kwamba watafutwe basi vikosi wawekwe pale angalau wakikukosea unajua utakwenda kutoa ripoti nidhamu itachukuliwa kwa watu wale. Lakini leo kampuni iliyowekwa pale hawana mafunzo, wajeuri, wajuaji hawana lugha nzuri, hakuna mtu

anayekwenda kutembea Hospitali ya Mnazi Mmoja bura bure, kutembea mtu anakwenda Forodhani atatafuta *beach* atakwenda. Hata mtu akienda Hospitali ya Mnazi Mmoja ana matatizo, kama haumwi anauguliwa, pengine ana matatizo mengine lakini haendi kutembea, kwa kutembea tu pale si pahali pazuri. Nasema hivyo kwa sababu kila pahali na raha yake, unapokwenda kwenye hospitali kuna harufu zake unazipata, lakini hospitali yetu usije ukenda pale utasikia harufu ya vidonda na mikojo ni tatizo, hatutegemei kwamba mtu atoke huko akatembee akasikie harufu ya mikojo na vidondo si kweli.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana wale walinzi waliopo pale wafundishwe angalau heshima. Nilikuwa shahidi kwa macho yangu katika kipindi kilichopita Baraza hili hili tuliloanza nimewakuta Waheshimiwa watatu kwenye mlango mkubwa wa kuingilia Mnazi Mmoja, wanasulubiwa na mlinzi eti Wawakilishi wa CCM. Sasa tunakwenda wapi Mhe. Waziri, tunafanya kazi kisiasa imekuwa haramu kwa CCM, kwa CCM, eti mlinzi tu awa-*harass* Wawakilishi na bahati nzuri nikatoka nikaja kutatua tatizo lile, Wawakilishi wale wakapita, wamo humu ndani ya Baraza na mashahidi wa hayo, hata ukitaka nikutajie nitakutajia. Ningekuomba sana katika hicho Mheshimiwa ujitahidi na suala la pale. *(Makofi)*

Lakini vile vile nije katika suala jengine la kinga Mhe. Mwenyekiti, najua unaumwa sana na sekta ya afya, kama anavyoumia Rais wetu wa Zanzibar katika sekta hii. Kwa sababu macho yake yote anayaweka pale mpaka ukaja ukathubutu kila mwezi kukupeni pesa sio chini ya shilingi milioni mia moja na kitu kwa ajili ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini hili suala la kinga haliko pale isipokuwa ninataka nizungumze tu kwamba kuna upungufu wa kinga hizi na malalamiko yako mengi, hakuna kinga ya *TT* imekuwa tatizo, hii zaidi ya miezi mitatu *PCV* tatizo, kama imekuja jana na leo au juzi, kuna Penta tatizo ilikaribia ku-*expire* walipewa UM yake iko ndogo, kuna polio ni tatizo na hata rota, tuone hizi kinga ambazo ndizo zinazosaidia akina mama na watoto, lazima wapate chanjo hizi. Kwa sasa hivi Zanzibar imekuwa tatizo. kulikoni wapi tunakwenda. Tunakumbuka nyuma ilikuwa kila muda ilikuwa hivi vitu tunavipata ndani ya muda watu wote wanafaidika navyo. Sasa hivi imekuwa tatizo katika suala hili. Ningekuomba sana Mhe. Waziri katika hili uje unisaidie angalau tuone watu wetu pale wanapokimbilia pana kilio chao kinasikizwa na masuala mengine ambayo yanaweza kuhitajika yanafanyika sana katika suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Maulid Diwani naomba umalizie una dakika mbili.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana vile vile, nikizungumza mbele narudi tena Hospitali ya Mnazi Mmoja suala *mortuary. Mortuary* yetu haikidhi na wewe ni shahidi uliweza kuthubutu kuhamisha mwili wa mzungu kutoka pale kuupeleka Hospitali ya Bububu kwa kuogopa kutafunwa na panya, kwa sababu kunikuwa na maiti moja mule ishatafunwa na panya kwenye pua na wewe ulikuwa shahidi. Mna panya mle mna mende, kwa maana hiyo hamna baridi ya kutosha kwenye *mortuary* yetu ya Mnazi Mmoja. Ni hilo hilo jipu la Hospitali ya Mnazi Mmoja Mhe. Waziri nakuamini sana na kupenda sana kaka yangu, lakini katika suala la Hospitali ya Mnazi Mmoja mtupunguzie kutuuwa. Mnatuuwa siku zetu hazijafika Mnazi Mmoja kwa kukosa gas tu oxygen.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana lazima uombe *mandate* na wewe ya kufanya kazi katika hospitali ile au kama kuna watu wengine wana agenda siri na wewe hawakutaki, hakupi mashirikiano ni suala jengine lakini mtu mzima akili za kuambiwa changanya na zako, uangalie jinsi gani utaweza kulitatua suala lile. Mhe. Mwenyekiti, zogo limekuwa jingi Mhe. Waziri. Waswahili wanasema, "Mtemewa mate na wengi mwisho huroa", nakuomba usije ukaroa katika suala la Mnazi Mmoja, inauma sana inasikitisha sana, natamani kulia kwa uchungu wa suala la Mnazi Mmoja mnatuuwa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nina mengi ya kuzungumza katika suala hilo lakini muda sio rafiki. Siungi mkono hoja ya Wizara hii mpaka nipate majibu mazuri sana kuhusu kadhia ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, baada ya hapo nitakuwa sina matatizo katika kupitisha. Lakini kwa sasa hivi siungi mkono hoja.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said akifuatiwa Mhe. Zulfa Mmaka Omar na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Sarahan Saidi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kuniona na kunipa fursa kwa kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi napenda nimpongeze Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein katika jitihada zake za dhati katika Wizara ya Afya kwenye kututoa kule tulipotoka mpaka kutufikisha hapa katika hatua kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, lazima na yeye nimpongeze hasa kwa kutujengea hospitali yetu ile ya Mkoani ambayo kama ni kwa Pemba au Zanzibar dira la kuonesha kwamba kweli tuna muelekeo wa hali ya juu, hapo lazima nimpongeze Dkt. Ali

Mohamed Shein pamoja na jitihada nyengine ambazo anazitekeleza. Pia nimpongeze Waziri katika jitihada zake pamoja na watendaji wake.(*Makofi*).

Lakini Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze katika sehemu hii wanayoita Bodi ya Chakula, Vipodozi na Madawa pamoja na mambo mengine. Sawa Mhe. Mwenyekiti, katika Wizara ya Afya imeunga kila sehemu. Mhe. Wizara ya Afya ndio kila kitu, binadamu yeyote ambaye akifikwa na matatizo au akikaribia kurudi kwa Mwenyezi Mungu basi afya ndio kitu cha kwanza lakini hata kama yuko katika maisha inabidi ajichangie sana na afya. Mheshimiwa malalamiko bado kukwambia kweli katika Wizara ya Afya pamoja na kwamba kuna mambo mengi ambayo yanakuwa kama hayakuhusu, hayakuhusu lakini yanakuhusu. Mheshimiwa masuala ya chakula katika mambo kama mabucha au katika sehemu ambazo kuna machinjio au katika sehemu zile za bahari ambazo samaki wanaburuzwa. Mheshimiwa pamoja na kwamba inawezekana labda sekta zile katika ugatuzi zikawa ni sehemu ambazo zina watu wasimamizi lakini afya wewe baadae ndio dharura pamoja na utafiti wa maradhi yanakufika wewe.

Mhe. Mwenyekiti, samaki akitolewa kwenye maji anaweza kuburuzwa katika matope labda kama mita ishirini anaburuzwa ndani ya matope. Sasa sijui hata utaratibu huu umekuwaje. Zamani watu wakitoa kwenye jahazi wanaweka mzega mzega anakwenda kwenye soko anauweka. Leo nenda Malindi pale anatolewa pale anaburuzwa ndani ya zile tope za makaro na nina uhakika kuna maradhi mengine ambayo wewe unayajua, kwamba hata ukiyachemsha watu wanakwambia si atapikwa, hata akipikwa hafi. Matokeo yake tunapata maradhi samaki anaburuzwa kwenye makaro yanayotoka kwenye mabomba wanayotumia watu, ile mzenga mzenga umeondoka haupo tena, watu wanafanya mambo kama haya. Lakini hata nyama ya ng'ombe inaburuzwa inakokotwa ile nyama kama si chakula ambacho kitaliwa, mwengine unaweza kukiona kinyesi hata usile tena.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana watu wako wa afya pamoja sijui katika sekta hizi za sasa kama zinahusu watu wa kilimo au watu wapi lakini ni afya. Mheshimiwa kukwambia kweli tungekuwa wakali katika kuangalia suala kama hili ambalo lina matatizo. Lakini pia katika sekta hiyo hiyo ya chakula tuna vijidude vidogo vidogo kama peremende ambazo zinaingia nchini na huwa watoto wanakula, kwa kweli zile peremende havina hadhi ya kuliwa, vinafanywa ovyo ovyo, watoto wanakula hawajui wanakula kitu gani na tumevitupa tupa hatujui hata kama kitu gani.

Mheshimiwa hizi peremende nazo zingekuwa na *grade*. Hebu ungeamua peremende inauzwa shilingi moja, shilingi mbili sijui hata peremende za aina gani. Matokeo yake watoto wale ndio tunaowategemea lakini watakufa siku si zao na kupata maradhi hata siku si zao. Mimi ningeomba sana hata vitu vile vidogo vidogo si lazma vitu vikubwa lakini viangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la pili ni suala la madaktari na sehemu zile ambazo tuseme kama hospitali ndogo ndogo katika kuwajibika. Mimi nataka nizungumze kitu kimoja kwamba kwanza pamoja na yote daktari ukiachia kusomea, lakini lazima na Mwenyezi Mungu amuweke mbele na dini yake aiweke mbele katika kuhudumikia, sio kusoma tu na kuamua kufanya kazi na kulipwa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, zamani tulipokuwa watu wakifanyiwa *interview* ilikuwa sekta ya afya na nyengine zote zilikuwa hazitizamwi kama mtu anakuwa na *credit* gani katika cheti chake, wakati mwengine hata roho yake uitizame, wakati mwengine uso wake utizame. Mheshimiwa unaweza utakuta mgonjwa anakaribia kufa lakini ukampelekea daktari mzuri ana sura ya kuchekesha ana sura nzuri akapona, na lakini unaweza kuwa mtu yuko katika sakaratul mauti au sehemu ambayo hana tatizo, ukampelekea daktari ambaye kukwambia kweli roho yake mbaya pamoja na kila kitu chake hakiko hadhi yake ya mtu yule ikamfikia. Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana katika kuajiri sekta ya afya ukawatizama watu na roho zao, usitizame cheti zaidi. Kwa sababu kuna watu hawaoni kwamba huyu ni binadamu mwenzangu, yeye anaamua mimi serikali haikunilipa, sijui mimi sijalipwa mafao, mimi wacha nimuuwe, wache afe kitu gani, wakati kitu kile ukiachia malipo daktari ukiachia na mwalimu ni mtu sawa na yai na kuku ni kwamba wewe hata ukalipwa na serikali haijakulipa kitu, utakwenda kulipwa na Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo madaktari na walimu lakini ningesema sana kwamba Mheshimiwa hii ni ajira katika ajira tizama sana watu ukiona watu roho zao mbaya usiwaajiri, wanakwenda kuzimaliza. Jana tu nimeona katika mtandao mmoja kuna mama mmoja anauwa wazee ati katumwa na Mungu toka mwaka sijui mwaka 2006 – 2015 juzi kishauwa watu ati katumwa na Mungu. Sasa nimeona anawachomwa shindano yaliyokuwa *over dose* sijui kitu gani mpaka anauwa ambazo ni *poison* kabisa. Ningekuomba sana Mhe. Mwenyekiti, katika ajira usitizame cheti tu, tizama na hali halisi ya kumpima mtu, tena muulizie hata kwao kama ana roho mbaya hata usimuajiri, kwa sababu anakwenda kutumaliza kule. *(Makofi)*

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusu suala la ukaguzi. Mheshimiwa ningeomba tena na wewe ukaacha sekta kidogo ya magari, madaktari wako wale wa ukaguzi ukawapa vespa, wakenda katika vijiji na katika sehemu katika maeneo huko kukusaidia wapate vespa za haraka haraka ni pesa ndogo ambayo atatumia kwa shughuli zake lakini na kazi atakufanyia. Kwa hivyo ningeomba mafuta yake ya 2,000 atia mwenyewe najua ukimpa vespa mpya na mafuta ataweka mwenyewe, lakini watakusaidia anaingia katika kituo anaangalia hali halisi, sio lazima mpaka gari itoke ya Wizara ya Afya kwenda kukagua wanajipanga wale, na huko kukwambia kweli kuna mashaka Mheshimiwa. Kwa hivyo ningeomba sana wakaguzi nao ukawatafutia vespa wakawa wepesi wa kwenda katika shughuli zao.

Lakini chegine nije katika Hospitali ya Chake Chake. Mheshimiwa mimi najua kama tuna hospitali kubwa sana na nzuri sana ya Mkoani, lakini katika hospitali kwa Pemba inayohudumikia watu wengi kama ya Chake Chake hakuna. Lakini pia ndio kioo cha Chake Chake kwa wageni, watu wa kila aina wanakaa Chake Chake, kimahoteli na kila jambo. Kwa hivyo ningekuomba sana Mhe. Waziri Hospitali ya Chake Chake ukaichukulia kwamba ni hospitali kubwa kutokana na wingi wa watu wake ambao wanahudumia. Watu pale kwenye Uwanja wa Ndege, ndio kwenye kiwanja cha watoto na kila kitu kipo pale. Kwa hivyo ningekuomba kwanza tulipanga sana pale Mhe. Waziri kwamba utengeneze sehemu moja ambayo itakuwa na vyumba vya kulala Waheshimiwa, wageni au watu watakaopata na dharura sio unamkuta mtu mkubwa, mtu mgeni rasmi ana pesa yake akakae kwenye *corridor* na wagonjwa wa kawaida.

Kwa hivyo tungesaidia kwa sababu pale Chake Chake hakuna hospitali za binafsi ambazo zina uwezo huo. Sasa bora hiyo hospitali yetu ya Chake Chake tukaipanua ikawekwa katika nafasi nzuri. Lakini pia hospitali yetu Mhe. Waziri inavuja, unaburuta kitanda mvua hizi zote ilikuwa watu wanapigana shambi, njoo kwako, njoo kwangu. Mheshimiwa hii hospitali ningeomba utizame kweli kweli kwa sababu *population* ya watu wanaohudumikiwa zaidi ya laki moja ile nafasi ni kubwa sana wengine wanaokuja kutembea wanapelekwa hospitali kabisa. Kwa hivyo hii hospitali ningekuomba sana Mheshimiwa ukaitizama sana, lakini hospitali ile hata lile *washing machine* haina. Mheshimiwa ningeomba ukaitafutia *washing machine* za nguvu zikaweza kusaidia. *(Makofi)*

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee kwamba bado nakutupia lawama katika masuala ya ukaguzi. Mhe. Mwenyekiti, matatizo yanaanza padogo yanaanza kwenye nyumba, yanaanza kwenye maeneo madogo madogo lakini kipindi cha nyuma wakati wa mvua kabla ya mvua wakati wa makaro,

Mheshimiwa nyumba inakaguliwa moja kwa moja na mtu kutoka afya. Sasa ningekuomba mimi sijui mambo ya ugatuzi yameanzia wapi lakini bado nasema ni afya. Mheshimiwa bado waruhusu watu kuingia kwenye majumba kwa ajili ya ukaguzi. Kuna nyumba zina makaro yako ndani, sasa yule akianza kipindupindu ina maana ndio kimeenea Zanzibar nzima. Sasa ningeomba kwamba nyumba nyengine zikaguliwe, kuna watu bado nyumba mpaka leo haziza vyoo, watu wanafanya mambo yao wanachimba mashimo wengine wanakwenda haja ovyo. Kwa hivyo ningeshauri bado nyumba zikaguliwe ili watu wasipate maradhi ya kuambukiza pamoja na maskuli bado inatakiwa zikakakaguliwe maskuli.

Kwa sababu elimu wanatazama watu tu wanavyosoma tu lakini ukaguzi wa afya hautizamwi. Kwa hivyo ningekuomba bado maskuli ni jukumu lako ukapeleke watu wakayakague kama maskuli mengine hayako kiafya yafungwe, kama mengine yanahitaji kuboreshwa utowe muongozo wako. Hivyo ningekushauri sana Mhe. Waziri zaidi huo ni ushauri. Lakini nataka nizungumzie kwenye sekta ya vifaa vyako. Mheshimiwa bado nakwambia tena dawa zako unazoleta kwa jitihada zote zinaibiwa, dawa Mhe. Waziri kukwambia kweli unajitahidi, kwa kweli Serikali inajitahidi lakini kwa sababu kuna mvujo, lile neno halitojaa, lakini wewe hata ukajitahidi ukatwambia umeleta dawa za aina gani mimi nakwambia zinavuja na bado utapata matatizo kwamba dawa hazitoshi lakini dawa zinatosha zinazoletwa na Serikali. *(Makofi)*

Lakini kwa kweli mvujo umekuwa mkubwa bado na haya madawa ambayo yanasababisha kwamba chini ya mahospitali ndio kuna mafamasi, kuna mabalaa gani na dawa zetu hazina nembo. Kwa hivyo dawa ndio hiyo hiyo, Hivyo ningekuomba sana Mhe. Waziri sijui utafute mbinu nyengine ya kukusaidia. Maana yake najua unajitahidi lakini bado naweza kukwambia kwamba wanaokukabili wako wengi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nije kwenye uzazi wa mama na mtoto. Mhe. Waziri nimeona kwenye kitabu chako kwenye kifungu cha 34 kwamba kuna watu ambao wamejifungua lakini Unguja na Pemba katika mazingira tofauti ambayo ya ujauzito. Nimeona kama ripoti ya Pemba, watu katika mama na ujauzito wamepata wengine wamekufa zaidi kidogo kwa sababu kwenye vifo vya watu 27, lakini watu 12 wamekufa Unguja na Pemba 15. Hii nayo na pia katika idadi ambayo wemejifungua ni dogo lakini kasema Mheshimiwa haijakuwa mbaya, haya ni mambo ya Mwenyezi Mungu kufa lakini pia kuna sababu zake. mchunguze kidogo.

Kwa sababu mama akikosa maji na akikosa damu pamoja na ile kujifungua nyumbani na mtu anaweza kwenda hospitali akaambiwa sijui hafanyi, hebu chunguza kwa nini wafe ingawa siwezi kusema kwa sababu kufa ni lazima. Lakini bado kwenye afya tunataka tuchunguze.

Mhe. Waziri jengine utakapokuja hapa hebu njoo uwafahamishe watu kidogo katika hii watoto njiti, katika *style* hii ya kangaroo. Mhe. Waziri mimi nilikwenda Bara nikaiona mama katika watoto wale wanaozaliwa kabla ya umri basi hakuna haja ya kutiwa katika *incubator* na nini, mama anafungwa nayo katika *style* ya kangaroo, anapona yule mtoto anapata joto anakwenda lakini Pemba sijaiona hii kangaroo. Nimeangalia angalia kila nikitizama naweza kwenda amepigwa pumzi kwenye *incubator*, lakini *style* ya kangaroo bado, sijui kwamba tayari au vipi lakini ningeomba hii *style* ya kangaroo inayosifiwa sasa hivi kwamba ni nzuri na zaidi ina afya.

Kwa hivyo ningeshauri katika mambo yako ukaweza kuifanya, lakini Mhe. Waziri nimeona katika kitabu chako pia umeangalia katika suala la unyonyeshaji katika miezi 6 ambayo mama mzazi anatakiwa amnyonyeshe mtoto bila ya kumlisha chakula chochote. Mheshimiwa hii bado ni ngumu, sijui katika utaratibu maana yake mama mwenyewe chakula anachokula sicho. Sasa ningeomba kitu kimoja wale mama ambao unawahisi kwamba afya zao hazitoshi ukapata ushauri nasaha nzuri sana kwamba yule mtoto anamnyonyesha vipi. Mwengine ukimwambia mama kifua chenyewe hichi, hilo ziwa halikuvimba limekaa kama soksi ya jeshi. Maana yake halina maziwa ya kutosha. Sasa huyu akimnyonyesha miezi 6 hafiki mtoto atalia usiku wa kucha ana njaa hamna *vitamin* vya kumtosheleza, ukija Mhe. Waziri uje utufahamishe kidogo hii hali inakuwaje. *(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka niseme Waziri pia atakapokuja umeelezea katika habari ya watoto ambao wamefikwa na utapia mlo ambao wanatakiwa *vitamin A*. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja kwa manufaa ya watu wote uwafahamishe *vitamin A* ni nini, kwa sababu wengine wanamuona mtoto wanampikia sijuii mpikie kigali, sijui nimpikie kidude gani, anampikia wali na anamtilia mchuzi kidogo, sio *vitamin A*, bora apate kitu kidogo kama ni kipande cha yai au kitu kidogo ufahamishe *vitamin A* ni nini, sio kila siku utumie matone tu ya *vitamin A*, umfahamishe yule mama anaweza kuwa *vitamin A* anavyo, lakini hajui vya kumpa. Kwa hivyo ningeomba hilo kidogo tulitizame ili uweze kutusaidia, unatusaidia sana lakini uzidi kutufafanua.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka niangalie kwenye ukurasa wa 22 katika kifungu cha 55 habari ya shingo hii, habari ya *goitre*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahani Said naomba umalizie una dakika 2.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naam Mhe. Mwenyekiti, dakika mbili. Dakika mbili hee! mama.

Haya ngoja niende upesi upesi Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Waziri basi atakapokuja niliona katika takwimu zako kwamba kuna Kaskazini kuhusu habari ya chumvi. Hii chumvi ambayo ina madini inasaidia. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, *goitre* Pemba ni nyingi, zinakuja kwa kasi sana. Nafikiri hili suala kwa sababu utafiti wako umeshajieleza kwamba wale watengenezaji chumvi wapate haya madini joto ambayo yanasaidia sana kuondoa hili tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa sababu wakati hamna ngoja niende katika ukurasa wa 63 ambao kuna maradhi na mienendo ya mambo chungu mzima. Nimeona humu katika ukurasa wa 63 kuna watu waliotafunwa na mbwa. Juzi Mhe. Nadir Abdul-latif alisema hapa kama hawa mbwa kama wameshakuwa kero, kwa nini hatuwauzii wanaokula. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri angetoa agizo, mbwa wameshakuwa wengi. Kwa hivyo ungetoa agizo kwamba mbwa wote wakamatwe, wakusanywe tukawauze lakini wasitafune watu, umesema kwenye kitabu chako watu wengi karibu sitini na ngapi wametafunwa na mbwa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikupe pongezi pamoja na Waziri wako ambaye mlikwenda juzi Geneva lakini haitokuwa mbaya ukaja ukatupa mafanikio uliyoyapata Geneva katika Zanzibar yetu, ningekushauri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikwambie kwamba umejitahidi katika afya za kawaida, ninachokuomba kule Pemba hebu tutafutie madaktari *specialist* hata watatu kama daktari wa moyo, daktari wa sukari, daktari wa *cancer* utakuwa umemaliza kazi. Madaktari wa maradhi madogo madogo, madaktari tunao utakuwa umetupunguzia sana safari za kwenda Dar-es-Salaam na kwengine. Ukitutafutia madaktari watatu hata wakiwa wana *appointment* za mtu katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la Hospitali ya Mikunguni katika hospitali ya macho. Kama umeamua hospitali ya macho ya kitaifa iwepo pale Mikunguni basi vile vitengo vyengine viondoe. Mhe. Mwenyekiti, ile hospitali haitoshi inakuwa na tabu kubwa. Kwa hivyo unaweza ukawaondoa wale wengine wakawekwa wale watu wa macho wakapata nafasi ya kutosha. Siku

utakapokwenda siku ya *clinic* pale watu mpaka barabarani watu. Ningeliomba hilo litekelezwe.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kitu kidogo utueleze hivyo hapa Zanzibar nimeona katika kifungu chako kuna uzazi wa mpangilio. Juzi ulitusifia sana kwamba siku moja wanazaliwa watoto 100. Hivyo huu ndiyo mpangilio au tumezidi nguvu.

Chengine utueleze Zanzibar ina mpango gani wa kueleza watu katika familia mwisho mtu azae watoto wangapi, maana kwa vile hujatoa kauli hii, tunazaa sana. Ningeomba utakapokuja utwambie kwamba Zanzibar inampango gani. Maana ukituachia basi ndiyo ngoma unaiona baada ya kuzaa watoto 100, tutazaa watoto 200, sasa hivi wanazaliwa wanne wanne, uje utwambie hapa kwamba familia izae watoto wangapi.

Jengine nataka niseme la mwisho kabisa kwa sababu ya muda. Mhe. Waziri katika sekta yako ya afya mambo mengi unajitahidi katika kila kitu lakini bado usafi unahitajika sana. Ningekushauri bado wale watu wanaojitolea (*day paid),* ukatoa nafasi wakatusaidia katika sekta za usafi. Mahospitali kwa wale *orderly* tu wakusafisha hawatoshi pamoja na mle ndani ambamo mnasafishwa, lakini kama utatoa nafasi hii wanaweza watu wengine wakatusaidia kwa mishahara, lakini tukapata usafi wa ziada. Mhe. Mwenyekiti, niwape nafasi na wenzangu.

Nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahani wa Jimbo la Chake Chake. Sasa nilimwita Mhe. Zulfa Mmaka Omar, naona hayupo, nakuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub akifuatiwa na Mhe. Mtumwa Suleiman Makame na Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei) ajitayarishe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa Bismillahi Rahmani Rrahim, Ramashani ya 9 leo. Mhe. Mwenyekiti, niruhusu kidogo nikaze suruwali yangu kuivuta juu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, wengi huko walifikiri kwamba sitozungumza kwenye Wizara hii ya Afya. Wizara nyeti, Wizara inayemgusa kila kiumbe hai, anahitaji afya na bila ya afya sisi sote humu tusingekuwepo. Afya ndiyo uhai wa mtu na ndiyo utajiri wake mtu kuliko kitu chochote duniani, utakuwa na pesa zako ngapi lakini afya ukawa huwezi kuipata.

Mhe. Mwenyekiti, hii Wizara huko nyuma rikodi yangu mara nyingi huwa naichangia mwanzo na kuitoa makosa mengi. Hii bajeti ina makosa makubwa na kipindi cha huko nyuma tulifanya marekebisho Naibu Spika alikuwa shahidi tukairejesha Wizara hii ikafanya marekebisho. Unajua ukisema utoe na sababu zake kwa nini ina makosa. Tumepitisha sheria juzi juzi hapa Nam. 3 2016 na tukapiga kelele humu humu ndani Hospitali hii ipewe dhamana labda nikinukuu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria Nam. 3 tulipitisha humu ndani tukasema hospitali hii iwe na maamuzi, Wizara ikaeleza kwenye hotuba yake hata Mhe. Waziri kwenye kitabu chake alieleza kina makosa katika hicho kitabu. Waziri kaeleza kuna makosa ambayo katika ukurasa wa paragrafu ya 114 ukurasa wa 49 naomba kunukuu.

"Mheshimiwa Baraza lako lilipitisha Sheria Nam. 3 ya Mwaka 2016 ya kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe inajitegemea", mwisho wa kunukuu.

Maelezo hayo bora yasiwemo kwenye hotuba, siyo kweli kwa Sheria hii kuwa imefanya Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe inajitegemea. Mwanasheria Mkuu kama yupo angetusaidia kuwa hichi kitabu kina makosa tele kikarekebishwe. Tumepitisha sheria sisi wenyewe humu ndani lakini tunajisahau, mchana tunazungumza vyengine na jioni tunazungumza vyengine. Sheria hii imefanya Hospitali ya Mnazi Mmoja bado tegemezi kwa kuwa bado ni Wakala wa Serikali na Wakala sio chombo kinachojitegemea, tuangalie wenzetu Hospitali ya Muhimbili. Mhe. Mwenyekiti, huo ni utangulizi naomba dakika zangu uzilinde. Maana yake tukifanya jambo tuwe na uhakika na *confidence* ya kwamba nini tunachokifanya, haya ndiyo masikitiko yangu. Mhe. Waziri hotuba yake kaeleza vile vile, hata Kamati nayo imefanya makosa. Nataka kuilaumu Kamati. Huu ndiyo ukweli ulivyo, "Mnyonge mnyongeni". Hii bajeti kwanza irekebishwe, haya maneno yasiingie kwenye *hansard*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo sasa nianze kwenye mchango wangu. Nikubaliane na Mhe. Waziri katika utangulizi wake na haya siku zote nasema hata saa sita za usiku nikiamshwa usingizi mkali katika sekta ya afya basi nitasema kwamba Dkt. Ali Mohamed Shain kafanya kazi kubwa sana. Sisi sote humu ndani ni mashahidi. Kila Rais kaondoka na alichokifanya lakini kwa hili Dkt. Shein kafanya kazi kubwa sekta ya afya ni lazima tumpongeze. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nilipiga kelele sana humu kuhusu huduma za wazazi humu ikawa tunasokotana humu ndani, akaliona ukweli wake ikaondoshwa ada ya

shilingi 40,000. Wazee wetu walikuwa wakilipishwa shilingi 40,000 ni jambo la kutia moyo. Rais yupo makini kwa wananchi wake na sisi sote ni mashahidi. Nimepiga makelele *ICU* humu ndani palikuwa hapana, palikuwa pana gereji mle ndani. Mhe. Juma Duni kipindi kile alitaka kujiuzulu humu ndani. Mhe. Mahmoud ulikuwa ni mgeni wakati huo, imejengwa *ICU* ya kimataifa Agakhan alikuwa hana. Kelele za Mwakilishi wa Jimbo la Paje, wakati huo wa Jimbo la Muyuni, walikuwemo akina Mhe. Mwanaidi wanakumbuka Mhe. Bhaa anakumbuka kipindi hicho nikaonekana mimi ni mbaya. Leo tumeiona *ICU* ile. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, tumeliona jengo la Hospitali ya Abdalla Mzee. Nimpongeze sana Mhe. Rais kwa jitihada hizo, lakini nitakuwa sijamfanyia haki Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa ziara zake za kushtukiza katika jengo la Hospitali ya Mnazi Mmoja, ingawa siku hizi kazikata Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, amefanya ziara mbili za kushtukiza na akaona machafu yaliyokuwepo pale. Nikupongeze sana Mhe. Balozi na hilo jaribu kulifuatilia, bado kuna matatizo makubwa na nitakueleza Mheshimiwa kama Kiongozi Mkuu wa Serikali humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikubaliane na maneno ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein aliyozungumza Mkoani Pemba saa 5:45 alipofungua Hospitali ya Abdalla Mzee, akasema maneno haya naomba ninukuu.

"Niungane na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa marafiki waliokuwa wakubwa kama sio watu wa China".

Katika sekta ya afya hawa ndio marafiki kwa asilimia 97 wametusaidia wao. Kwa hivyo mimi nimpongeze sana na Mhe. Balozi tupelekee salamu kwa Balozi wa China kwa kazi kubwa, kuweza kutusaidia katika sekta ya afya, tunampongeza kwa dhati kabisa. "Mnyonge mnyongeni", lakini wamefanya kazi kubwa hawa watu kutusaidia. Haya kayazungumza siku ile ya nyinyi nyote mlikuwepo na akatoa hadithi Mhe. Rais. Nafikiri mnakumbuka Mawaziri, Wawakilishi wengi miongoni mwetu hatukwenda. Alitoa hadithi pale akasema "Hata wewe".

Mhe. Mwenyekiti, unajua tusiwaonee Wizara ya Afya, wamefanya mengine mazuri na wao haki yao kupongezwa. Wizara ya Afya imefanya mengine mazuri siyo tunawaonea tu. "Hoi hoi nacho kilindo". Kelele za Wawakilishi sio za Jaku tu peke yake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nitaje mafanikio yaliyopatikana. Dawa ambalo ndiyo jambo lililokuwa zito, wamefanya kazi Wizara ya Afya dawa sasa hivi zinaridhisha kwa kiasi fulani. "Mnyonge mnyongeni haki yake apewe", dawa zipo kwa kiasi fulani, sio zote. Ukitoka kwenye dawa vituo vya afya na dhana zake. Wizara imejitahidi kwa kiasi fulani ni lazima tuwapongeze. La tatu kubwa zaidi naomba hapa nisikilizwe kwa makini wasije watu wakafika mbali.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imesomesha madaktari bingwa hamsini. Jambo la kupongezwa sana, wamefanya kazi kubwa sana madaktari bingwa 50 kwenda kuwasomesha ni kazi kubwa, lakini nataka kurudia tena Mhe. Issa Gavu hayupo hapa kidogo ningemgusa yeye. Lakini wanaporudi tusije tukawabagua jamani hawa, serikali imepoteza pesa zake nyingi isije yakawa mambo ya kisiasa, tusamehane jamani, tunawasomesha kwa pesa zetu, siasa isijekuwemo ndani tena humu. Kama upekuzi ufanyike mapema kabla ya kwenda kuwasomesha, tufahamiane vizuri jamani. Siasa na afya tusije tukachanganya ni vitu viwili tofauti, *(it is two things words of different concept).*

Mhe. Mwenyekiti, watu tumeshawasomesha, pesa zimeshapotea tunakuja kutia siasa, tuwachunguze kabla ya kuwasomesha hawa watu. Wizara ya Afya imefanya kazi kubwa kwa hilo niwapongeze. Sasa hivi *oxygen* kwa kiasi fulani ipo inaridhisha. Kwa hivyo Wizara haya tukupongezeni, sio ninalaumu tu lakini panapo ukweli tuseme ukweli.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye mchango wangu katika Wizara ya Afya. Kitengo cha *ICU* kina mapungufu makubwa hivi sasa. *Air condition* mbili zinahitaji shilingi ngapi kwani, wagonjwa wanaumia kwa joto, wengine wanakufa kabla ya wakati wake na kwa joto liliomo ndani yake. Kuna dawa za *oframax* hamna ndani katika *ICU* iliyojengwa juzi na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. Hichi kitengo ni muhimu ICU *(Intensive Care Unit),* hivi mkiangalia hichi kitengo leo ule pale ndio ubinadamu gani ule unaoufanyika. *ICU* imejengwa na Mhe. Rais kwa gharama kubwa hakuna kinachoendelea, kuna vitu chungu mzima pungufu.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye Kitengo cha Watoto wanaoungua moto, ukenda pale utawaonea huruma, wamejengewa kibanda kama kuku mle ndani. Kitanda kimoja watu wawili na mle ndani mwisho watu watano. Sasa hivi ukenda hii leo kuna wagonjwa 7 na dawa zenyewe hazipo, kuna dawa zinahitajika kama *meblow* ni *cream* hii inauzwa karibu Shs.18,000 au nyengine inaitwa *Mupitesam. H*izi *cream* mgonjwa hawezi kuzinunua na kitengo kile cha moto kina umuhimu wake, mtafute pahali pa kukiweka sawa. Chumba ni kidogo hakiridhishi kilichokuwepo pale. Doctor Jamala andika vitu ndugu yangu huko,

najua huko juu unafuatilia sana. Mhe. Mwenyekiti, pia kuna madirisha nayo yanavuja mle ndani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikitoka hapo nije kwenye *theatre*, mazingira yake hairidhishi. Kuna wimbo wa bendi ya Sikinde Ngoma uliimba kwamba, "usiache chungu kipya kwa chungu cha zamani". Kwa hivyo mmepata chungu kipya lile jengo la zamani mkalidharau. Mle ndani *theatre* aibu viti vya kuchukulia pale sijui kama gongo lake halijaoza lile moja, *lift* hazifanyi kazi tokea wakati huo. Lakini cha kushangaza hapa hapa *goose* nazo sasa hivi zimepungua hazipo, jiko la kupitikia lina mashaka mle ndani, kiwembe nacho nobe kikatafutwe.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri haya maneno ninayoyazungumza kuhusu *theatre* yaandike vizuri, kuna *povidone iodine* zote hazipo. Haya mambo ni ya kusikitisha sana. Hichi kitengo cha upasuaji uhaba wa vifaa nacho, kuna *canular* hapa mkiulizwa mnasema zipo kumbe hazipo, *urinarybag* za mikojo hizi hazipo. Sasa mnazungumza mambo ambayo hata mengine hayaelekei.

La mwisho kwa jengo lile kuna mambo mawili hetu yafikirieni, lile jengo hamlioni kama linavuja miaka mingapi tunapiga kelele kwenye ghorofa ya tatu kule. Juzi wagonjwa waliteremka chini walipoa bila ya muda wao kufika, kulitokea *shoot* ya umeme iliyosababishwa na maji na aje mtu abishe kana nasema uwongo maneno haya hapa, wameondoka kwa moto uliotokea kule na yote ni kwa kuvuja kwa jengo. Haya yote ndiyo atoke Rais Ikulu akafanye yeye jamani. Haya mambo madogo madogo Dkt. Shein sekta hii kaipa uwezo mkubwa sana, sijui kwa kuwa katokea kule au vipi. Nafikiri na mwenyewe anafuatilia mjadala huu unavyoendelea. Mhe. Mwenyekiti, hichi kitu cha ajabu (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika ripoti ya Kamati. Sasa hapa kidogo Mhe. Waziri anza, kuchukua buku tufungue pamoja. Nataka kujua Kamati na Wizara ipi yenye nguvu, hapa nataka nitumie lugha ya kiswahili kidogo kidogo. Kamati ya Ustawi imeidhinisha bilioni 21.4 "Programu ya Kinga ya Elimu ya Afya", ndiyo hotuba ya Kamati ilivyosema kwenye buku. Nimebahatisha kutafuta ripoti ya Kamati nikaipata hapa, namshukuru Mheshimiwa aliyenipa sitaki kumtaja jina. Hebu iangalieni programu hii Mhe. Waziri kwenye buku inaonesha milioni 19, ukurasa nitakwambia 28 nishaweka *points* fungua katika buku lako kubwa. Hebu tuambieni *which is which*. Kamati ya Ustawi wa Jamii imeidhinisha bilioni 21, nyinyi kwa nini mkenda kuomba milioni 19 kwenye

buku. Sasa nani hapo mtakayekuja kumlaumu, halafu utakuja kusema pesa kidogo, mnatengenezewa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, kama hapo hapatoshi, Kamati imeeleza kuwa imepunguza bajeti 2017/2018) zimetengwa bilioni moja katika mradi huo. Jengo la Mkemia Mkuu fedha hizi hazionekani kwenye buku, sizioni mimi humu ndani ya buku kubwa. Naomba maelezo kama mradi huu umetengewa fedha. Hichi ni kitengo muhimu cha Doctor Slimu.

Kwenye programu ndogo "Huduma za Matibabu", Kamati nimeisikiliza vizuri wamesema kuna bilioni 15 na zaidi zimetengwa. Nimetizama kwenye kasma kwenye buku kubwa limetengewa bilioni 21 ukurasa wa 30. Mhe. Waziri angalia ukurasa wa 30 siyo maneno yangu haya. Nauliza Kamati na Wizara nani yupo sahihi, kipi kumekubaliwa kwenye kamati naomba maelezo kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya msingi kutokana na mifano hiyo, nina wasi wasi wakati Kamati ilipokaa na Wizara imeidhinisha pesa nyengine na hapa Wizara imeleta pesa nyengine ambazo Kamati hawajazipitisha au Wizara imefanya marekebisho bila ya kuitaarifu Kamati, hili ni kosa. Sawa sawa na kuidharau Kamati, naomba tuwe na utaratibu wa kuyaheshimiwa yanayotolewa na kukubaliana kwenye Kamati. Kamati nyingi zimekuwa zinatawaliwa na Wizara, haya yameshanikuta kwenye Kamati yangu mimi upande wa Kamati ya Wanawake na Watoto. Naomba tuwe na utaratibu wa kuyaheshimu yanayotolewa kwenye Kamati. Wizara kama zina marekebisho zipewe taarifa, siyo Kamati inasema kitu chengine na huku Wizara inafanya kitu chengine.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, angalia kwenye buku hili haya mambo mnayoyafanya muyaangalie, mengine mnayoyafanya ni mambo ya dharau. Hebu niambie lile jenereta alilotoa mfadhili Mhe. Abdalla Maulid Diwani kazungumza ile ni dharau au sijui nitumie lugha gani au kusahau au uzembe. Leo jenereta watu wameshakwama mle ndani siku ngapi tunapiga kelele hapa, hii nidharau wizara. Watendaji mnamuangusha Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, jenereta kubwa lilokuwepo pale la kuendeshea hospitali ile, leo umeme mule ndani sehemu nyengine taa haziwaki. Mhe. Abdalla Maulid Diwani akazungumza linataka kama Dola elfu tano, kama milioni kumi na moja, kumi na mbili, milioni nne hazifiki au tatu zile kwenda kujenga sakafu ile na kifaa basi kama hatuna tuweke makuti ya viungo ya makumba, hii dharau tunafanyiana jenereta lipo limeletwa tunazungumza kwa uchungu sisi. Sasa kitu kama kile jenereta atoke Makamu wa Pili wa Rais akasimamie lipo miezi mitano ni sawa na riski

kuipiga teke. Lile jenereta ni jambo muhimu sana, hii ni dhararu. Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na tatizo la maji mule hospitali, huku Wizara inazungumza vyengine, huku watendaji wanazungumza vyengine limetokea mimi nimekwenda nikaliona siku ya Jumapili. Leo maji nobe nayo kuwasha *pump* kwa uzembe Wizara jitahidini maji ndio usafi wa hospitali vile vyoo ambavyo ukiingia ndani havitizamiki vyoo Hospitali ya Mnazi Mmoja, la pili Mhe. Waziri aandike.

Mhe. Mwenyekiti, la tatu aandike kibanda hapa nilipata sana Mhe. Waziri hili wewe umelikuta. Kama kuna mtu wa kumshukuru wewe mshukuru Mhe. Abdalla Ramadhan Shaaban na Mamlaka ya Mji Mkongwe hii kazi nimeifanya mimi ndani humu Mwenyezi Mungu shahidi. Kibanda kile hapa mniletee ile ramani mlionionesha sasa hivi, mimi ndio niliohangaika sio nyinyi Wizara. *Doctor* Jamala shahidi anasema kibali hatukipati kwenye Mamlaka ya Mji Mkongwe, nikahangaika kikapatika humu ndani, nilizuiwia bajeti ya Wizara ya Ardhi kipindi kilichopota. Nimshukuru sana Mkurugenzi Issa Makarani kwa kujali wananchi lakini Wizara hii ni dharau mnayofanya, kibanda kile miaka saba sasa hivi. Mnadhimu wangu wa Chama cha Mapinduzi Mhe. Ali Salum Haji shahidi wa hili alikuwa kwenye Kamati, michoro nirudishieni mwenyewe hapa, nitatafuta njia mimi ya kufanya, tena naomba sisikii lugha nyengine yoyote michoro munirudishie humu ndani. Hii dharau zenu zinashafika pahali zimeshavuka mpaka, michoro nimehanganika mimi nirudishie mwenyewe nitafuta njia ya kufanya pale, kama nyinyi mumeshindwa kusaidia nitakusaidieni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wananchi pale wanapata shida pale hampiki pilau wala biriani wala hamtoi sadaka, hebu nendeni alfajiri nyinyi Mawaziri hayakukuteni, ndiyo hayo niliyokwambieni mkikaa kwenye gari zenu mnafunga vioo hamuoni wale watu wanavyoumia wanaokwenda pale wavuvi na wakulima katika hospitali ile, wamekaa kwenye sakafu kwa uchungu wengine wanapata maradhi baada ya kwenda kutizama wagonjwa wao wanapata maradhi pale kwa kulala chini kwenye sakafu baridi kama hii na mvua kama hizi yakhe, tunawafanyia nini. Ndivyo Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ilivyotuelekeza hivi. Kile ni kimbilio mimi pengine leo nije niumwe nipelekwe pale pale, lazima tujenge mazingira wizara ile Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein amefanya kazi kubwa katika Wizara ile sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini haya ya jenereta kibanda kile nobe nirejesheeni ramani ya kibanda kile humu ndani kabla sijakupitishieni bajeti yenu, zimeletwa *ambulance* kama sikuiliza mimi suala humu ndani ndio zikagaiwa *ambulance*, mpaka nikauliza suala mimi zikagaiwa, kama kesho ninataka

kujibiwa swali langu siku tatu ndio zikatoka *ambulance* na Naibu Waziri juzi naye akaja akachemsha, nikamuheshimu. Mhe. Mwenyekiti, anasema pesa bima wamekata wao, bima za *ambulance* kakata Mbunge wa Makunduchi shilingi milioni mbili, lakini nikaona ahaa! mwezi wa Ramadhani huu mengine tusameheane.

Mhe. Mwenyekiti, hebu nielezeeni zile taka taka pale mtamsingizia nani zile zilizokuja kuwekwa pwani pale na sindano zile, mitandao yote imeandikwa aibu pale, mtamlaumu nani taka taka zile. Hebu niambieni tumlaumu nani takataka zile...

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa bado hapa itabidi nitumie kuweka kando Kanuni kwa leo hii wizara unipe ruhusa, maana yake mimi ndio natengeneza huko kote usije ukanipa lakini hapa natengeneza....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku naomba umalizie.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Haya tunatengeneza Mheshimiwa. Jengo kuvuja lile suala limekuwa na mashaka sana, kuna sehemu Mhe. Mwenyekiti, tulisema hapa wakati sheria ile inaletwa hapa waifanye hospitali yetu ya kujitegemea ipate fedha zake wenyewe tukaonekana wabaya. Leo mnakuja maelezo yale yale tuliyosema mkataba. Mimi namuomba Mhe. Waziri arekebishe yale aliyosema kwanza Hospitali ya Mnazi Mmoja ijitegemee bila ya kuwa na wakala, chombo kinachojitegemea kinakuwa *corporate* kama Muhimbili. Hii nakusaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, "Programu ya Matibabu", iangalie kwenye buku maana yake huku kuna mambo mengine hayakuelekea. Hoja yangu ipo hapa kuwa ushahidi niliokuja Mhe. Waziri "Uchunguzi wa Matibabu", fungu la H02 Hospitali ya Mnazi Mmoja *paragraph* 126 katika kitabu chako cha hotuba ya Waziri kimeeleza, "Huduma za matibabu katika kliniki maalum hospitali zimetarajia ikiwemo kliniki ya saratani. Hoja yangu kuhusu Kliniki ya Saratani, hakikuwa na maelezo ya kutosha kuhusu kliniki hiyo, hamna humu katika kitabu chako kwenye *paragraph* ya 126, haielezi fedha kiasi gani zimetengwa kwa kliniki ya saratani na miradi ya wafadhili. Niliuliza swali nambari 101 kwenye bajeti hii, nikaambiwa nitajibiwa kwa maandishi leo ya sita imeshapita, hakuna maandishi hata moja yaliyokuja. Najua huduma hizi zinatolewa lakini lengo la kliniki wanaoumia ni wanyonge, vitu vyake gharama zake ni kubwa.

Huduma za saratani ni ghali wagonjwa kutoka Zanzibar kufuata Dar es Salaam, ni *process* kubwa. Kiasi gani zimetengwa nataka kuelezwa katika kitengo cha saratani, fedha hizi zinapatikana kwenye bajeti za mwaka huu. Hii nataka kueleza hapa mpaka nipate maelezo ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, namalizia naomba uniruhusu dakika tatu kwa hisani yako Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuomba Mhe. Jaku kama unayo ya zaidi yaandike upeleke kwa maandishi ili tuwape nafasi wengine na muda wako umeisha nakuomba sana Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Namalizia dakika mbili nakuomba **k**ama kweli Hospitali ya Mnazi Mmoja inajitegemea, mbona fedha hizi zimetengwa katika bajeti ya wizara 9.8 billion zimetengwa baada wizara kuwa H01 wameandika kwenye H02. Huu ndio ukweli ulivyo....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku ahsante peleka mchango wako kwa maandishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, maelezo mengine nitaandika kwa maandishi nitampelekea Waziri na nakala kwa Makamu wa Pili wa Rais na mwenyewe kwa Mhe. Rais nyengine.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushurkuru sana Mhe. Jaku kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Mtumwa Suleiman Makame akifuatiwa na Mhe. Zulfa Mmaka Omar, Mhe. Hamad Abdalla Rashid ajitayarishe na Mhe. Simai Mohammed Said naye ajitayarishe.

Mhe. Mtumwa Suleiman Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika hapa tukiwa hali ya uzima na afya. Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kufika hadi leo kukamilisha nguzo ya nne ya Uislamu na ninamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuimalize kwa salama.(*Makofi*).

Hata hivyo pia narejea tena kumshukru Mwenyezi Mungu kwamba atujaalie wale wote tuliokuwa hatujakamilisha nguzo ya tano ya Uislamu tuikamilishe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kwa kumpongeza Mhe. Waziri. Kwa kweli nampongeza sana kwa utendaji wake na ni jembe, lakini sasa jembe hili linataka tupa. Mhe. Waziri kwa kweli ni jabari ni hodari na ni msikilivu wa watu, lakini haya tunayozungumza humu uyasikilize na uyafanyie kazi, ukiyafanyia kazi, jembe hilo litaweza kupata tupa na kung'oa visiki vilivyokuwemo ndani ya Wizara ya Afya.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, naingia katika Hospitali yetu ya Kivunge. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Rais kwa kutuwekea Hospitali ya Mkoa ya Kivunge pale ya Rufaa kuwa ni ya Mkoa. Lakini sasa kwenye mafanikio na matatizo yako Mhe. Mwenyekiti, hospitali yetu nzuri huduma zetu zinapatika pale lakini tuna matatizo aina tatu.

1. Tatizo la kwanza nyumba za wafanyakazi ni kidogo. Kwa hivyo tunaomba suala letu hilo au kilio chetu hicho cha watu wa Kaskazini kionekane na kiangaliwe vizuri.

2. Nguo yoyote huwa inataka kufuliwa na ile hospitali yetu pale ina huduma mle ndani mna eneo la bustani, lakini kwa bahati nzuri mfanyakazi wa bustani yupo lakini bahati mbya mpaka leo hajaariwa. Kwa hivyo naomba suala langu hilo, nitaunga mkono lakini uje unijibu suala hilo ni lini mfanyakazi yule ataajiriwa.

3. Tulikaa hapa nyuma mwanzo wa kuingia kwenye Baraza hili tukaletewa makaratasi mengi tuu tujaze fomu kwa ajili ya huduma ya bima, lakini bahati mbaya Hospitali ya Kivunge huduma ile mpaka leo hapana. Je, wale watu wa shamba waliokuwepo wanatumia hospitali ile pale, huduma ile wataipata wapi. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa na suala hilo la huduma ni lini itaanza katika Hospitali ya Kivunge anieleze.

Mhe. Mwenyekiti, naingia katika Hospitali yangu ya Kaani Masingini kwa sababu lugha hiyo ya Kaani Masingini Mhe. Waziri ilikuwa haijuwi. Sasa mimi nikiwa ni mtu wa pale Kaani Masingini nakwambiya ile si Chaani Masingini, ni kaani maskini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo nimepe Mhe. Waziri historia ndogo ya Kituo kile pale cha Afya, Kituo kile cha Afya tulijenga watu wa Chaani kwa ajili tunapata matatizo, kutoka Chaani kwenda Chaani kubwa Kikobweni na kutoka Chaani kwenda Kivunge, wanawaake wa pale tulikuwa tunapata matatizo, daladala hakuna na kwa bahati mbaya ile pesa ya daladala pia

mwanamke hana. Tukaenda tukabeba mawe sisi wanawake wa Chaani Matemwe tukajenga hospitali ile kipindi kile mimi Katibu wa Tawi la CCM tawi lile pale. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Waziri kwamba siku ya tarehe 11/06/2016 ulitembelea kituo kile pale na ukaona tatizo lililokuwepo pale. Mhe. Waziri alikubali kwamba tatizo lile utalifanyia kazi, lakini sasa nasikitika sana au tunasikitika watu wa Chaani kwamba hadi hii leo tatizo lile hujaliondoa. Kwa hivyo nakuomba hapo utakapokuja kujibu haya masuala uje kunijibu ni lini ukarabati ule utaufanyia kazi Hospitali ya Chaani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naondoka hapo usione nasema sana ni Kiswahili cha lugha ya kishamba hicho, kichukuwe hivyo hivyo. Mhe. Mwenyekiti, naingia katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kweli tunampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na wewe tunakupongeza. Lakini sasa hospitali yetu ina matatizo. Kuna baadhi ya wafanyakazi wale wanokaa pale mlangoni heshima zao fupi.(*Makofi*).

Mhe. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wale pale uwafahamishe au uwaelekeze, usiwaondoe waite tu uwalekeze kwa sababu bado hawajafahamu, ukiwazelekeza wanaweza wakafahamu. Wafanyakazi wale ukifika pale hayo maneno wanayokupa si mazuri. Hivi karibuni tulifika pale na Waheshimiwa wenzangu tunaingia mule ndani hospitali, kama si kuingilia Mhe. Abdalla Maulid Diwani tulikuwa tushuke ndani ya gari tumpige kibao yule mlinzi pale, kwa kauli alizotuweleza basi nakuomba uwaelekeze wafanyakazi wale.

Halafu Mhe. Mhe. Mwenyekiti, jengine tulitembelea ile hospitali na kufanya usafi lakini bahati nzuri kwenye jengo la wanawake kule juu ghorofa ya tatu hakusemeki. Sisi ikiwa ni wanawake tulipoingia kule machozi yalitutoka, kuyaeleza yaliyokuwemo ndani kwa hapa hayaelezeki, lakini nakuomba uwende ukaliangalie ujuwe tatizo lilokuwepo mule ndani.(*Makofi*).

Halafu jengine kuhusu habari ya huduma hiyo ya bima. Mhe. Waziri huduma hii ya bima pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, huu ni mwezi wa tatu hapana na kuna wanyonge wengi sana tunakimbilia hospitali ile pale. Kwa hivyo namuomba suala hilo ulifuatilie ile na sisi tuliokuwa hatwendi hospitali nyengine, tukenda pale huduma hizo tuzipate.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuhusu wale watu wanaokaa pale na wagonjwa wao. Kwa kweli wale wananchi wanaokaa pale wanapata tabu na wanadhalilika. Juzi nimekwenda hivi karibuni hata siku nne bado, nikalala pale chini alipopazungumza Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti,

ukienda pale machozi yatakutoka, hayo mengine siyasemi. Lakini tatizo kubwa pale palijengwa vile vikuta vya kukalia wale wananchi wanaowasubiri wagonjwa wao kule utujengee choo. Kwa sababu basi wakati inapokuwa saa za kuangalia wagonjwa hazijafika, wale wananchi waliokuwepo pale wanapata matatizo ya kujisaidia hawana pa kwenda, wakifika mlangoni, hao watoa huduma hao hayasemeki maneno wanayoeleza na kuna watu wengine wameshakuwa watu wazima.(*Makofi*).

Kwa hivyo ninalokuomba Mhe. Waziri sehemu ile pale uingalie vizuri utafute eneo lolote uwajengee choo wapate watu cha kujisaidia ili wastirike wale wanaotoka kule vijijini, watu wa mjini wakifika pale wanaweka mgonjwa mtu anaondoka kwa sababu wako karibu. Lakini kuna wengine wanatoka shamba akifika pale lazima anabaki pale.

Mhe. Mwenyekiti, jengine la mwisho hilo kwenye huduma hospitali hili huku jengo jipya. Lile jengo zuri, linakidhi lakini wafanyakazi kidogo. Ninalokuomba Mhe. Waziri hawa wafanyakazi watakaoajiriwa pale upaone, kwa sababu kule kuna huduma za watu wanaojifungua na wanawake ndiyo sisi, lakini tatizo lake wale wafanyakazi waliokuwepo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hili la mwisho lakini kuna jengine, hili ndio kubwa zaidi. Mhe. Waziri jana alitueleza kwamba huduma za uzazi wa mpango kwa sababu anayekwenda kutafuta huduma hizo lazima aende na mwanamme. Hili ni tatizo kubwa sana na wanaume wenyewe ndio nyinyi, wanawake wengi sana wanajiunga na huduma hizo waume za hawajui. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi unataka kusababisha talaka. Watu wanaokwenda kujiunga kwenye uzazi wa mpangilio nasema uhakika baadhi ya wanaume waliokuwepo humu ndani sio nje mwanamke anajiunga mumewe hataki, anakwenda kumpimisha mtoto kliniki huku anajiunga na uzazi ule. Leo unasema kwamba atakapokwenda kule ende na mumewe. Mhe. Waziri takala hiyo, ukae ukijua kwamba hii ni takala. Sasa basi pamoja na hayo hawa waliokuwa na waume watakwenda na waume zao. Je, Mhe. Waziri nataka uje kunijibu hapa wale waliokuwa wanataka kujiunga na huduma hizi waliokuwa hawana waume watafanya nini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango wangu mdogo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naunga mkono tisini na tano na tano zilizobaki anijibu. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mtumwa Suleiman. Sasa naomba nimwite Mhe. Zulfa Mmaka Omar akifuatiwa na Mhe. Hamad Abdalla Rashid na Mhe. Simai Mohammed Said ajitayarishe.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika Wizara hii nzito. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi zake zote anazozichukua katika Wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo pekee la kujisifia sisi Wazanzibari kutokana na Rais wetu, tunaona mafanikio mengi sana tuliyoyapata na tunaona jitihada za Mhe. Rais juu ya suala la afya.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tu Mhe. Rais alikwenda kutufungulia jengo letu la Hospitali ya Mkoani. Tunamshukuru sana wakaazi wote wa Pemba na tumefurahi na tunaomba Mwenyezi Mungu amjalie kila la kheri baba yetu yule katika maisha yake kwa imani zake anazotuonesha sisi wananchi wake wa Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nina michango miwili mitatu katika Wizara hii nzito ambayo naomba tu-share na Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, watu wanasema, "Mcheza kwao hutunzwa". Mimi Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze na kwetu Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana Wizara nimeona kwamba kuna marekebisho ambayo yamewekewa pesa katika Hospitali ya Chake Chake. Kwa kweli jengo lile la Chake Chake lilikuwa limeshakuwa aibu kubwa sana kwa sababu jengo linavuja na tunajua kwamba ile ni hospitali wanaotumia Pemba nzima, kwa sababu tunakuta kwamba watu wa Wete, Mkoani na Chake Chake wote wanatumia jengo lile.

Kwa kweli nimefurahi sana kuona kwamba kuna pesa ambazo zitafanyiwa marekebisho jengo lile. Lakini nimuombe tuu Mhe. Waziri hizi pesa ambazo zinakwenda kufanyiwa marekebisho tunakuta kwamba kuna Mawizara mengi sana yameingiziwa pesa wanakwenda kufanya marekebisho majengo, lakini mwisho wa siku majengo yale hata miezi sita hayafiki yanaanza kuvuja na kutoka pele. Kwa hivyo nikuombe sana katika ujenzi huu usimame mwenyewe kufuatilia, hili ni suala zito usimtume mtoto Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo katika Hospitali ya Chake Chake kuna mambo kidogo hayapo vizuri, naamini kwamba ni jitihada zako unataka mambo yote yawe sawa lakini naomba nianze katika Kitengo cha Macho.

Mhe. Mwenyekiti, katika Hospitali ya Chake Chake Kitengo cha Macho hakiridhishi. Kitengo kile hakina vifaa vya kutosha na tunajua kwamba macho ni kiungo kizito kwa binadamu. Kwa hivyo nikuombe sana. Tumeona hapa

kwamba kuna vifaa ambavyo mlipata mchango kutoka kwa madaktari lakini vifaa vile havikufika Pemba. Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri katika bajeti yako hii uweke pesa ijapo kidogo, utuwekee vifaa na sisi katika kile Kitengo cha Macho. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia unakuta kwamba kuna watoto ambao wana matatizo ya macho, kuna vijana, kuna watu wazima, kwa kweli wanasumbuka sana kupata huduma hii ya macho. Mhe. Mwenyekiti, tunafikia kipindi kwamba ukitaka matibabu mazuri ya macho ni lazima uje Unguja. Kwa hivyo nikuombe sana kitengo kile kiangalie kwa jicho la imani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika suala la saratani. Mheshimiwa tunaona kwamba hapa Unguja Hospitali ya Mnazi Mmoja tayari kimeshawekwa hiki kitengo, lakini kule Pemba hamna na tunajua kwamba watu wengi sana hawana uelewa juu ya matatizo haya. Kwa hivyo mtu akienda pale ukianza kushukiwa na tatizo kama lile ukiambiwa nenda Unguja, inakuwa ni ngumu sana. Mhe. Mwenyekiti, sisi hatutaki kitengo kikubwa ijapo kidogo tu utuwekee mtu akienda pale apate japo ile huduma ya mwanzo aangaliwe, apewe ushauri, afanye hivi basi itakuwa ni vizuri kuliko kwamba akienda pale anaambiwa nenda Unguja kwenda kupata matibabu. Kwa kweli Mheshimiwa tunakuomba kwa suala hilo utuwekee vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika suala la vipimo. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba sasa hivi matibabu ni bure na ukienda hospitali unaambiwa matibabu ni bure *alhamdulillah* tunaona, lakini mheshimiwa kuna hili suala la vipimo, kama kipimo cha *HB*, vipimo vya sukari, vipimo vya *typhoid.* Mhe. Mwenyekiti, vipimo vile mara nyingi sana unavipata mwanzo wa mwezi, ikifika kati kati ya mwezi unakwenda vipimo vile hamna, unaambiwa kwamba uende katika hospitali za *private*. Mhe. Mwenyekiti, hospitali za *private* kuna mambo yake na wale ni wananchi wetu. Kwa hivyo tunakuomba sana vipimo hivi.

Pia ukiangalia kipimo cha sukari ambacho mtu anatakiwa kupima asubuhi na jioni, hapa Unguja *alhamdulillah* vipimo vile wanavipata bure, lakini Mheshimiwa nikwambie kwamba Pemba kipimo hicho wanapima kwa shilingi 1000 mara moja. Kwa hivyo unakuta kwamba mgonjwa siwezi kujua kwamba vile vipimo ambavyo wanavitumia wale madaktari waliomo mle ni vya kwao au vipi na wanakubali kwa sababu wanataka wajue afya yao. Kwa hivyo nikuombe sana vitu hivi vinapelekwa lakini niseme sijui ni haba au vinatumiwa sivyo. Hivyo, nikuombe sana Mheshimiwa masuala ya vipimo kama haya yapelekwe ili wananchi waweze kutumia vizuri waondokane kwenda katika hospitali za *private*, kwa sababu hospitali za *private* ukienda kupima majibu

wengine wanakuwa hawaridhiki nayo. Kwa hivyo nikuombe sana kwa suala hili unisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika hospitali ya Chake-Chake sasa hivi kuna tatizo la *washing machine*. Tunajua kwamba *washing machine* ni kitu muhimu hasa hospitali, kuna ugumu mkubwa sana wa kuchukua shuka ambalo kalalia mgonjwa kwani kila mgonjwa na matatizo yake. Mhe. Mwenyekiti, ikikosekana ile *washing machine* itamlazimika mtu akoshe kwa mikono yake na akikosha kwa mikono yake kila mtu na matatizo yake, maradhi mengine yanaambukiza. Kwa hivyo nikuombe sana suala la *washing machine* lifanyie haraka iwezekanavyo ili na wao katika hospitali ya Chake-Chake suala hili waweze kulipata kwa muda muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo hapo kuna mashine za kusafishia picha za X-*ray*. Mheshimiwa hizi mashine hospitali ya Chake-Chake wanasafisha kwa mikono na ni jambo ambalo limepitwa na wakati. Kwa hivyo suala hili naomba pia uende kulitizama.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende katika walinzi. Mheshimiwa katika hospitali zote zina walinzi lakini na hospitali ya Chake-Chake walinzi uliotuwekea ni kiboko. Walinzi wajeuri, hawajui kazi zao sikwambii kwamba wafukuze, kama alivyosema Mhe. Mtumwa lakini nikuombe sana wale walinzi wapeni darasa kidogo au ikiwezekana tutafutie walinzi ambao wana sare tunajua kwamba huyu ni mlinzi amefahamu. Lakini sas ukienda pale mlinzi kama atakutolea jeuri wakati mwengine una mgonjwa wako yuko katika hali mbaya, tunaweza kuja kusababisha pale watu kuja kupigana kwa jambo ambalo halina maana. Kwa hivyo nikuombe sana ukae na hawa walinzi wako uwaeleze kwamba ile hospitali kila mtu anayekwenda hospitali anakuwa na akili zake. Kwa hivyo naamini kwamba wakishakufahamishwa hivyo bila ya kufukuzwa, mimi naomba wapewe onyo kwa mara nyengine ili na sisi tujue kwamba wale watu wanapewa onyo na wanabadilika na tabia zao.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika Hospitali ya Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, hospitali ya Mkoani ni nzuri, iko imara na ina vifaa ambavyo naweza kusema hapa kwa Zanzibar vifaa vile vinapatikana katika hospitali ile ya Mkoani. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nimuulize je, unafahamu kwamba mashine ya X-*ray* ya Mkoani haina *film* sasa hivi ni mwezi mzima. Kama hujui mimi nataka nikujuilishe hilo, ile ni mashine mpya imefungwa na pale wananchi wanakwenda wanajua kwamba tumefunguliwa hospitali nzuri wakienda pale wanakosa huduma hii.

Mhe. Mwenyekiti, pale pana *CT Scan. CT Scan* hii mwahali mote wanafanya kwa malipo kama Shs.150,000 hivi, lakini pale nashukuru kwamba inafanywa bure. Lakini mashine ile ya *CT Scan* ambayo ni mpya sasa hivi kuna mwezi mmoja na siku kidogo haina *film*. Kwa hivyo hili ni tatizo kwa sababu wananchi wanajua kwamba tukienda pale sisi tunakwenda kwa ajili ya huduma hii tutaipata. Kuna wananchi kutoka Unguja wanakwenda Pemba kwa ajili ya kufuata *CT Scan*, lakini wakifika pale jibu lao wanaambiwa kwamba hamna *film*. Kwa kweli kidogo ni mtihani, hivyo nikuombe sana Mheshimiwa suala hili uende kuliangalia naamini kwamba inawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, pia nije katika suala la hospitali ya Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, hospitali ya Mkoani imefunguliwa na kuna vifaa vingi sana, lakini la kusikitisha vifaa vile havitumiki na havitumiki kwa sababu hamna madaktari. Je, nimuulize Mhe. Waziri wakati inajengwa hospitali ile hukufahamu kwamba pale patatakiwa madaktari, kwa sababu kuna siku hapa Naibu Waziri alijibu kwamba madaktari wako wanasomeshwa kwa ajili ya kwenda kufanya kazi zile. Lakini sasa kwa kipindi hiki ambacho madaktari wale wanasomeshwa. Je, huoni kwamba ipo haja ya kuchukua madaktari ijapo Tanzania Bara na kuweza kuwaweka katika nafasi zile ili mashine zile waweze kuzitumia na wananchi wetu wapate kupata huduma zile za afya. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kusema kwamba mashine zile zikae tu mpaka tumalize kusomesha madaktari, kwa kweli kidogo ni mtihani na itakuwa tuna mvunja moyo hasa Mhe. Rais, kwa sababu yeye tayari ameshavinunua na ameshaviweka pale, matajirio yake kwamba vitumike na wananchi wafaidike. Lakini vitu vile mwisho wake vimekuwa kwamba ni pambo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika suala la usafi. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri sana katika hospitali zetu tunakuta kuna baadhi ya uchafu uchafu. Hebu nikuombe Mhe. Waziri katika bajeti hii panga pesa kidogo hebu ununue ma-*dustbins* uweke katika vyoo vya hospitali tuangalie, kwa sababu tukienda katika vyoo vya hospitali tunakuta kwamba kuna uchafu mwingi sana unaotupwa chini. Kwa kweli hili ni tatizo, hivyo nikuombe sana mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile niende katika zile ajira ambazo zimetangaziwa. Katika zile ajira mimi nipongeze kwamba kuna ajira ambayo unataka kuajiri, lakini nikuombe sana zile ambazo zimepelekwa Pemba ni kidogo, kwa sababu Pemba kuna *section* nyingi sana ambazo hazina watu. Kwa hivyo kwa kusema kwamba Pemba unapeleka nafasi kumi sijui kumi na mbili, kwa kweli kidogo ni mtihani. Nikuombe sana Mhe. Waziri hizi nafasi zipo mia na zaidi, hebu angalia na Pemba uwaongezee nafasi ili na wao waweze kupata madaktari wale

ambao wataajiriwa wafanye kazi katika hospitali zetu. Tukiangalia hospitali ya Mkoani hamna watu, tukiangalia hospitali ya Wete kumewekwa vifaa kibao vya kuzalia lakini hamna madaktari, hatujui kwamba vifaa hivi vinanunuliwa kwa ajili gani. Kwa hivyo niseme kwamba pesa zetu zinapotea kwa sababu vinanunuliwa vifaa baadae vifaa hivi vinakaa mapambo. Nikuombe sana Mhe. Waziri suala la vifaa vile watafutie madaktari ambao wataweza kwenda kuvitumia.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika lugha. Mheshimiwa bado wauguzi wetu wana lugha chafu, kama unavyomjua mtu akienda anaumwa na uchungu anakuwa na akili tofauti kidogo, ile ni hali nzito ambayo pale hata Mwenyezi Mungu mwenyewe kapasemea. Lakini Mheshimiwa tunakuta kwamba wale ambao wanazalisha bado wana lugha chafu. Kwa hivyo nikuombe sana hao ambao wanazalisha hebu wape tena darasa wawe na lugha nzuri, kwa sababu ile si hali ya kumtolea mtu jeuri, maneno mazuri sadaka. Kwa hivyo basi wafanye maneno mazuri, pale ni pahali pazito. Kwa kweli mimi naamini suala hili kwa wao wanaliweza.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuipongeza wizara hii kwa jitihada zao ambazo wanazifanya na naamini kwamba Mhe. Rais hakukosea kuingia katika sekta ya afya ila nimuombe tena Mhe. Waziri kwa mara ya mwisho. Mhe. Waziri tunajua kwamba ni mtu ambaye unapenda kufanya *research*, unapenda sana kutembelea sehemu mbali mbali. Kwa hivyo nikwambie kwamba madaktari wa hospitali ya Chake-Chake wanakuomba uende uwatembelee na wao, wana hamu ya kukaa na Waziri wao kukujua na kubadilishana mawazo mawili matatu. Kwa hivyo nikuombe sana madaktari wa hospitali ya Chake Chake wanakwambia uende ukakae nao kidogo mbadilishane mawili matatu.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia hapo naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kamili. Ahsante mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka Omar kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamad Abdalla Rashid akifuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajitayarishe.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze moja kwa moja kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi zake kubwa anazochukua katika kuimarisha sekta ya afya visiwani mwetu. Halikadhalika niwapongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote wa Wizara ya Afya kwa kutunga kitabu ambacho kinatupa mwamko

sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma sahihi na bora ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze moja kwa moja kwenye fani ya uuguzi kwa sababu na mimi ni fani yangu. Kwa hivyo sina budi niichangie ipasavyo. Kwanza ningependa Mhe. Mwenyekiti, tuelewe hasa hii maana ya uuguzi. Maana yake wananchi wetu wengi wanaelewa kila anayefanya kazi hospitali ni daktari, hapana. Madaktari wako mbali lakini na wauguzi wako mbali na muuguzi lazima awe ni mtu aliyesoma ile kozi ya uuguzi lakini isitoshe awe kafaulu na sikufaulu tu aruhusiwe na serikali yake kufanya kazi ile ya uuguzi, huyo ndiye anayeitwa muuguzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi huwa napata tabu sana na kitu kisichofichika na nashukuru Wajumbe wengi wa Baraza la Wawakilishi wameelewa kabisa kwamba kuna upungufu mkubwa wa fani hii ya uuguzi ambayo inasababisha udhoroteshaji na utoaji huduma bora za wagonjwa wetu katika mahospitali. Hili lipo na si la kujificha na ningeomba kabisa na kumshauri Waziri hii fani ya uuguzi atie kasi zaidi ya kuhakikisha wauguzi wengi wanaajiriwa. Kuna wauguzi wako tele nje lakini hawana ajira ni vijana ambao tayari wamemaliza fani ya uuguzi, lakini wanaranda randa, lakini Wizara bado haijakuwa tayari kuwaajiri. Sasa mimi ningependa kumshauri Mhe. Waziri fani hii ya uuguzi kwa sababu uuguzi bila ya wauguzi mahospitali yetu basi hakuna hospitali. Hakuna hospitali inayoweza kufanyiwa kazi na madaktari tu, wauguzi peke yao wanaweza kuendesha hospitali lakini madaktari peke yao hawawezi kuendesha hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, katika fani hii na si wauguzi tu mimi ningemuomba na kumshauri Mhe. Waziri hata wale tunaowaita ma-*orderly*, mara nyingi visiwani petu ma-*orderlies* wanaajiriwa lakini hawapati hata semina ya wiki moja kuhusu nini u-*orderly*. Wenzetu kule Tanzania Bara wao wanaitwa *nurse assistant*, lakini mimi nawashukuru kwa sababu wao wale *nurse assistant* wao wanawapa *short courses* za kutoka *nurse assistant* kwenda *nurse auxiliary* akitoka hapo anapata na kozi ya kwenda mpaka *TN* au *Trend Nurse*. Sisi ma-*orderlies* wetu wanafanya kazi mpaka wanakufa katika sehemu ya hospitali anabakia kuwa *orderly* tu, hii si nzuri. Ningemshauri Mhe. Waziri na watendaji wake waandae mkakati maalum wa kuhakikisha ma-*orderlies* nao kwa sababu miaka hii vijana wetu wote ni wasomi, ni kuanzia *form IV* kwenda mbele. Kwa hivyo wangepata na wao kozi za kutoka *orderly* ndani ya kazi yao baada ya mwaka mmoja au miwili wakenda kwenye *nurse assistant*, tukaweza kupata huduma nzuri katika mahospitali yetu. Lakini leo ndio inayosema hakuna ule mpangilio maalum wa kuweka mtu muhusika kwenye sehemu husika, yeye ni

proper person at a proper place, tunapata tabu. Matokeo yake ndio tunaona ma-*orderlies* wetu wanaachiwa kuchoma sindano, wanaachiwa kufunga vidonda, wanaachiwa kuwagaia wagonjwa chakula, fani ya uuguzi hairuhusu hivyo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, muuguzi ndiye anayestahiki kumpa mgonjwa chakula, muuguzi ndiye anayestahiki kufunga kidonda mgonjwa, muuguzi ndiye anayestahiki kumpa mgonjwa dawa, muuguzi ndiye anayestahiki kumzalisha mzazi, haruhusiwi *orderly* ni kozi ambayo anatakiwa asomee, tunaona rahisi sisi kufunga kidonda cha mgonjwa. Mhe. Mwenyekiti, katika *procedure* ngumu ya Wizara ya Afya, basi ni *procedure* ya *dressing* kumfunga mgonjwa kidonda. Huku nje unaona ni rahisi lakini katika *procedure* ngumu mimi nimesoma miaka minne pale Muhimbili, katika *procedure* ambayo nilikuwa naiogopa kwenye mtihani ni *procedure* ya kufanya *dressing*. Ni *procedure* ambayo inastahiki kidonda cha mgonjwa kisije kikaingia mdudu wowote kusababisha madhara.

Sasa leo Zanzibar au visiwani petu mimi nathubutu kusema na Mhe. Waziri ananisikia ni kawaida sasa hivi *orderly* kufunga kidonda, yeye ndio kazi anaachiwa ile afanye. Ni kawaida *orderly* kuachiliwa kumpa mgonjwa chakula, siyo wagonjwa kuna kila aina ya wagonjwa. Kuna wagonjwa hawali sukari, kuna wagonjwa hawali mafuta, kuna wagonjwa hawalio chumvi, kuna wagonjwa wanasubiri kufanyiwa operesheni, *orderly* hajui ni *nurse* pekee ndio anaruhusiwa kufanya zile kazi. Lakini leo *nurse* ni moja wagonjwa 70 au 150 kwenye wodi. Kweli Mhe. Mwenyekiti, atafanya kazi *nurse* yule. Hafanyi na matokeo yake itakuwa ni sisi kumlaumu, wananchi kumlaumu. Mimi ningemshauri Waziri hebu tupige hatua moja mbele, tukubaliane kwanza wauguzi waongezwe katika kufundishwa kozi, wauguzi waajiriwe kwa nguvu lakini na ma-*orderly* na sekta nyengine zote wakiingia tu hospitali basi apewe kozi japo fupi ya nini hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, tukifanya hivyo hata hilo zogo la walinzi kwamba wanakuwa na lugha chafu, wafanyakazi wengine wanakuwa wanatoa lugha chafu pale itaondoka kwa sababu watakuwa wamejua sasa kwamba kuna tofauti baina ya hospitali na marikiti ya kuuza samaki au kuuza nazi. Kwa sababu nazi ukitaka kununua unasema tu bei yako, kataka mteja atanunua, hataki ataondoka. Mgonjwa haiwezekani, mgonjwa lazima ujue anahitaji nini na anahitaji kupatiwa kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo katika ushauri wangu wa kupatikana hawa ma-*nurse* wengi, mimi ningeomba Mhe. Waziri na nashukuru safari hii elimu

ya juu imepatiwa Wizara ya Elimu washirikiane sasa, kuhakikisha Chuo cha Afya Mbweni kinapatiwa wanafunzi wa kutosha kwa sababu vijana tunao wanaofaulu masomo ya sayansi, wanazagaa mitaani, hawapati nafasi ya kwenda chuoni zinachukuliwa nafasi kidogo. Mhe. Mwenyekiti, ipanuliwe ili vijana wetu waliofaulu masomo ya sayansi waende wakasome uuguzi, tukifanya hivyo baada ya miaka michache tutaona kwamba huduma ya uuguzi kwenye nchi yetu inakwenda vizuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa ile niliyoisema "*proper person at a proper place"*. Kuna aina tofauti ya wauguzi. Maana yake tukiita wauguzi tusisikie kama ni uuguzi, wauguzi wako wa aina tofauti. Kuna muuguzi *special* wa watoto, kuna muuguzi anayeweza kuzalisha tu, kuna muuguzi anayejua *medication* na mambo ya dawa tu, lakini kuna wauguzi *special* kwa wagonjwa mahututi tu. Hizi zote ni fani za wauguzi ambazo zinahitaji kozi maalum. Namshukuru Waziri katika kitabu chake kaelezea kabisa na kuna tayari baadhi ya wauguzi wamepelekwa kusomea kozi hizo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, katika kusomea hizi kozi, mimi napata tabu sana huwa nasikitika muuguzi anakwenda kusoma *special* kuhudumia wagonjwa watoto wadogo. Lakini hatumpeleki pale tunampeleka kwenda kuhudumia wagonjwa wa akili, wakati kwenye ugonjwa wa akili kuna muuguzi tena wake *special, nurse psychiatric* ambaye anasoma ugonjwa ule, anaondolewa anakwenda kupelekwa kwenye wagonjwa wa kifua kikuu. (*Makofi*).

Mhe. Mewnyekiti, mimi ningeomba Mhe. Waziri na Wakurugenzi wake hebu tupitie tena huu utaratibu wa ugawaji hawa kufanya kazi hususan wauguzi, tujue hasa kwamba muuguzi huyu kasomea kuzalisha, huyu ni *nurse midlle wives* tumpeleke kwenye wodi ya kuzalisha, muuguzi huyu kasomea magonjwa ya akili *nurse psychiatric* tumpeleke kwenye wodi ya wagonjwa wa akili, *nurse* huyu kasomea ugonjwa wa kutibu wagonjwa mahututi, tumpelekeni *ICU,* tuondoe hii dhana kwamba muuguzi ni muuguzi, hapana ndio maana muuguzi baada ya kusoma anakwenda kuchukua kozi ya ku-*specialiaze* ile fani anayoitaka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa juhudi aliyoichukua katika kitabu chake kueleza kuna wauguzi wamepelekwa kwenda kusoma hizo kozi. Naomba sasa tuwapange katika sehemu husika. Mhe. Mwenyekiti, kuna wauguzi wamekwenda kusoma mambo ya ushauri nasaha wana *degree*, kwenye ushauri nasaha akawekwe *nurse* tu wa kawaida, yule mwenye *degree* anaambiwa wewe fanya kazi vizuri. Haiwezekani lazima tuangalie mantiki kwa

sababu kenda kusoma yule kwa faida ya nchi yetu kuhudumia wananchi wetu tumpe nafasi ile aliyokwenda kusoma.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa niende kwenye Chuo cha Afya Mbweni. Nilisema mwanzo hapa kama kiko kwenye elimu ya juu. Mheshimiwa kile chuo mimi nasema kina mantiki kubwa na mimi ningefurahi kweli kama kile chuo kingekuwa chini ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kinachojitegemea, nina sababu zangu. Mheshimiwa chuo kile ndio pahali ambapo wanafunzi wauguzi na kozi nyengine wanatoka, nchi yetu ni nchi ya visiwa, tunapata *disaster* nyingi hapa. Kwa mfano, tumeona meli zetu kuzama kutokana na upungufu wa wafanyakazi wetu ambao wako hospitali. Kama kile chuo kingekuwa kina nguvu na kipo pale na wanafunzi wote wanalala pale kwenye bweni, basi ilikuwa ni wakati mzuri wakati ule kwa sababu mwanafunzi akifika mwaka wa pili muuguzi tayari anaweza kuhudumia mgonjwa, tungeweza kuwachukua haraka haraka wakaja wakajiunga na wafanyakazi wa hospitali wakafanya kazi. Lakini leo inatokezea *disaster* tunakamatia kamatia tu, wauguzi wetu ni kidogo tunawaondoa pale wanapelekwa kwenye *disaster*, huku wagonjwa wetu wanaendelea kufa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemshauri Waziri wa Afya na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali hebu wakae pamoja tuone kile chuo tunakitunza, maana yake tukitunze kile ni chuo ambacho kina muamko, kinatupa vijana wetu wengi wenye fani za afya tukilee tuhakikishe kwamba tunapata mafanikio. Kwanza tuhakikishe wanafunzi wote wanakaa pale chuoni kwenye mabweni tuache ule mtiririko wa wanafunzi kwenda majumbani mwao tukimtaka hatumpati. Mimi nakumbuka kuna mwaka *boeing* ya Tanzania ilitekwa hapa kwa maboribo tu, hatukulala siku mbili, sisi wanafunzi tumepigiwa simu tunaambiwa kaeni tayari kuna *disaster* imetokea, kuna ndege imetekwa hatujui itatua vipi Dar es Salaam, mukae tayari kupokea wagonjwa mahatuti na majeruhi, tulifanya hivyo. Mimi namshauri Waziri wa Afya na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wajitahidi kufanya hivyo.(*Makofi*).

Mhe Mwenyekiti, niende pale kwenye elimu ya kada nyengine sasa kama nilivyosema kwamba ma-*orderlies* tunapowaajiri na namuomba Mhe. Waziri wa Afya *Allah, Allah,* kanidokeza kwamba safari hii wanataka kuchukua kampuni ya kuajiri hawa ma-*orderlies,* tuwe macho na haya makampuni. Naomba zile kampuni Mhe. Mwenyekiti, tuhakikishe angalau basi zina watu wa fani ya afya ambayo itawasomesha wale wafanyakazi *orderlies* pale kabla ya ajira, wawape kozi maalumu ambazo zitasaidia katika kupata lugha nzuri, kupata huduma nzuri kwa wagonjwa wetu, tuache kwenda kuchukua kampuni ambayo itakwenda kuchukua watu pembeni huko wavuta unga tukawapeleka

pale hospitali itakuja kuwa hatari kubwa, itakuwa hatari ambayo tutakuja kujuta.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hospitali kama nilivyosema wananchi wengi wanaona wanaofanyakazi hospitali ni madaktari tu si kweli. Hospitali kuna fundi karo, kuna fundi umeme, kuna mfagiaji, kuna wafyekaji majani, sio madaktari wala si wauguzi lakini wapo pale. Lakini tofauti ya mkata majani wa hospitali na mkata majani wa barabarani inakuja tofauti hapo ni kwamba yule wa hospitali apewe elimu inayohusu hospitali. Wawakilishi wengi wamesemea hili itaondoka hii dhana ya lawama na kumparamia Waziri na kumtwisha mzigo mzito, bila ya kuwapa elimu hawa hatumalizi suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika fungu la unyanyasaji na unyanyapaa. Mimi namshukuru Waziri katupa rungu kubwa, sisi kama Wawakilishi tuwe tunaweza kuhoji ndani ya mahospitali. Mimi namshukuru kwa jambo hili na Waheshimiwa mimi nasema kwamba tuhojina Mhe. Waziri kakubali. Katika kuhoji kwetu nashauri sasa, kuna mambo yana mipaka yake kwenye hospitali, Waheshimiwa Wawakilishi si vyema, haitokuwa vizuri kwa sababu una rungu la Waziri uhoji hospitali ukaenda ukavamia wodi ya wazazi mule ndani maskini wako vibaya ukaingia tu, haiwezekani wala haiyumkiniki, tuangalieni mipaka hii vizuri. Naipongeza Wizara ya Afya kuzuwia sasa wanaume kuangalia wodi za wazazi. Mhe. Mwenyekiti, napongeza sana kwa hili kwa sababu wazazi ni wazazi. Kuna wodi zao haiwezekani uingie tu, mimi nikifika naingia tu kwa sababu ni *staff* tuseme ule ukweli, ukweli haufichiki tuko pale pale tu. Mimi ni *staff* nitaingia haidhuru ni Mwakilishi lakini wewe mwenzangu Mwakilishi unavamia saa sita za usiku hospitali kwa sababu unakwenda kuchunguza tu, unaingia ndani ya wodi ya wazazi aah! haiwezekani. Naomba rungu la Mhe. Waziri tulitumie vizuri, tulitumie kwa vipimo, tuelewe kwamba hapa ndipo, hapa sipo, ikibidi hivyo tutakuwa tunafanya vibaya. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda upande wa Pemba na nataka nimwambie Waziri mwenzangu katangulia kusema hapa kwamba bado Pemba upungugu huu wa wafanyakazi ni mkubwa mno, yaani ni mkubwa wa kupindukia, na kule hasa ndipo iliko hii *proper person at a proper place* na yote inatokana na huu upungufu. Wafanyakazi wetu wa Pemba wanajitahidi viongozi wetu lakini tatizo hawako wafanyakazi hususan hii kada ya uuguzi, watafanya nini. Matokeo yake leo Hospitali yangu ya Vitongoji kuna *nurse* watatu *Cottage Hospital*, ina wodi ya akinamama, wodi ya wanaume, wodi ya wazazi, *nurse* watatu. Hata ile *roster* maskini hawawezi kupanga tena. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri sasa ile hospitali hebu aipe upendeleo maalumu wa

kuongeza wauguzi mpaka angalau na mimi nirudi, tujitahidi tushirikiane. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nije na uchakavu wa majengo. Mimi napenda Waziri nimpongeze kasema ukweli na kwenye changamoto zake kasema kabisa kwamba moja katika majengo machakavu ni lile la Hospitali ya Chake Chake. Mhe. Mwenyekiti, lile jengo hizi mvua zilizopita ni aibu na tatizo lake ni dogo sana ni kuvuja kwa paa, sio padogo jengo lote la hospitali, wodi zote. Mhe. Waziri mimi namuomba kwa nguvu zake zote na najua Rais wetu hawezi kumuangusha tumpelekee ombi maalumu la uezekaji wa paa la Hospitali ya Chake Chake, imekuwa sasa ni karaha, maana yake kuna balaa na karaha ile sasa karaha, sogea huko na mimi nisogee huku na wagonjwa wengi inakuwa tabu. Naomba tumpelekee Mhe. Rais ombi hili maalumu atusaidie.

Mhe. Mwenyekiti, kuna siku nakumbuka hapa niliulizia kuhusu Kituo cha Kibokoni. Tuna kituo kule Vitongoji kinaitwa kijiji cha Kibokoni kimejengwa huu zaidi ya mwaka wa kumi na mbili, kituo kile hakijapata vifaa wala wafanyakazi wa kufanya kazi. Mhe. Waziri namkumbusha kile kituo akija hapa aje anieleze vizuri ni lini kitapatiwa vifaa na wafanyakazi wa kutoa huduma ili kuwasaidia wale ndugu zetu wa Kibokoni pale wasipate adhabu ya kutembea masafa marefu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije Hospitali ya Wete. Kwa kipindi hichi Hospitali ya Wete ina mashine ya *X-ray* lakini tunaambiwa haijafungwa. Naipongeza kwanza Wizara kupeleka mashine mpya ya *X-ray* pale. Sasa naomba kwa kuwasaidia wale wananchi wetu wa Wete na viunga vyake, mashine ile ifungwe haraka ili wananchi wetu wapate huduma.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho Mhe. Waziri mimi rafiki yangu, tena rafiki yangu wa kweli kweli, namkumbusha tu katika ahadi yake ya tarehe 18 katika maswali na majibu hapo, alinijibu rasmi baada ya kumlalamikia kwamba wananchi wangu wa Vitongoji na viunga vya Wawi wanapata shida ya usafiri pale linapotokezea tatizo na yanatokezea kwa uhakika, aliniahidi kwamba kuna magari manne mapya mbele ya Baraza hili na *hansard* ninazo ya tarehe 18 aliahidi kwamba, katika yale magari manne basi moja atalipeleka Vitongoji na ninaamini hataniangusha, naamini kikwazo mimi na yeye kitakuwa hapa kwenye bajeti kama hajanihakikishia lini gari lile la Hospitali ya Vitongoji jipya litafika pale lianze kutoa huduma.

Nimemshawishi Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Vitongoji kakubali kushirikiana na mimi kuhakikisha gari lile litapata mafuta umri wake wote wa kuhudumia

wananchi katika majimbo yetu. Mimi na yeye ndio tutajitolea kuhakikisha gari lile linapata mafuta ya kuhudumia wananchi wetu mpaka kufa kwetu. *(Makofi)*

Baada ya hayo nirudie tena kumpongeza Mhe. Waziri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia 98 naacha mbili tu za ahadi ya gari langu hilo.

Baada ya hayo naunga mkono hoja ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamad Abdalla Rashid kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said akifuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti ahsante, awali ya yote na mimi nianze sasa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kuweza kutoa maoni yangu, mawazo yangu, kuishauri wizara husika. Lakini nichukue nafasi hii kwa kunipa nafasi pia kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu ambao wao pia mimi ni kama sauti yao, mtetezi wao katika Baraza hili. Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa usomaji wake wa hotuba yake ya bajeti ambayo aliisoma kwa umakini na kuweza kuikamilisha kwa mbwembwe kabisa na kwa kujiamini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningependa niseme mambo mawili au matatu, lakini moja ni kwamba Wajumbe ambao walionitangulia nawaunga mkono yote waliyoyasema na ningependa nisirudie kwa yale ambayo wao tayari wameshayazungumza, lakini mimi nitapenda nijikite katika maeneo ambayo nahisi yataweza kutusaidia.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Wizara ya Afya ni katika eneo moja muhimu sana kwa mwananchi wetu wa Zanzibar pia wageni ambao wanaishi hapa inawagusa katika kila siku ya maisha yao. Mimi mwenyewe jana usiku nina mgonjwa kutoka jimboni kwangu amelazwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini cha kushukuru ni kwamba alihitaji *pints* mbili za damu na ninamshukuru Mwenyezi Mungu ameweza kupatiwa wala bila ya kufika mwenyewe katika hospitali ni jambo la kujipongeza. Lakini mambo kama haya hutokana na juhudi na kelele ambazo mara nyingi ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili wanapoyasema na mengine yale ambayo wayoyafuatilia. Msemaji aliyepita alitoa ushauri mzuri juu ya jinsi Wajumbe wanapotaka kuwajua lakini naamini utaratibu utakuwa ni mzuri, kwa sababu kila mmoja ameingia katika mlango huu kwa kupitia maeneo matatu. Moja ikiwa ni Jimbo la Ikulu, Majimboni kwa kupitia uchaguzi na pia wananchi kwenye uchaguzi wa viti maalumu.

Sasa nataka niseme vitu viwili kwa mambo niliyoyaangalia. La kwanza ukiangalia kwenye bajeti mara hii ni ukweli usiojificha, bajeti ya Serikali ukiangalia mara hii ukiijumlisha na kuangalia kwa umakini Wizara ya Afya imepewa karibu asilimia 10 ya bajeti ya serikali yote, sawa na shilingi 83 bilioni. Mimi sijapata kuiona hii. Sasa ikiwa hizi fedha zilizotengwa na serikali, na Waziri ametusomea kwa hili jambo, kwa kweli mimi naipongeza sana serikali kwa juhudi kuangalia katika bajeti kuu ya serikali asilimia 10 yote bilioni 83 itaingia hapa.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika usomaji nimeona suala la kensa. Mara hii naona karibu shilingi bilioni moja inaelekezwa huko. Sasa hili isiwe ni kwamba tunasoma katika maandishi lakini najua suala hili la kensa shilingi bilioni moja haijawahi kutokezea humu ndani tukaisikia. Mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu naipongeza sana serikali kuhakikisha kwamba shilingi bilioni moja hii itakwenda kwenye suala la kensa. Nampongeza sana Mhe. Waziri kwa hili.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nataka nipongeze sehemu moja. Wizara ya Afya au na hizo hospitali zetu zote changamoto zipo lakini tangu historia ninayoijua mimi nilipolazwa mwaka 1982 kwa malaria pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, tangu wakati hospitali ile inaitwa *V.I. Lenin Hospital*, wakati wa Karimjee Jivanjee, ni kwa mara ya kwanza awamu hii ya Rais huyu tuliyekuwa naye sasa hivi Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa mara ya kwanza vitanda vimeongezeka kutoka 430 na sasa tumepata 230 vipya. Hili kwa kweli ni jambo kubwa sana kwa nchi yetu halijawahi kutokezea, ukijumlisha sasa tutakuwa tuna vitanda 450 na jengo jipya 230, fanya mahesabu karibia 680 kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja na majengo yote yale. Hili ni jambo la kheri. Sasa tuitakie kwamba na maeneo yote ambayo huduma zitakapoboreshwa hasa katika suala la macho pia kule tunajua kuna shilingi milioni 350 zimetengwa tuhakikishe jambo linafanyika. Sasa haya yote mimi naamini yatatusaidia.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimeangalia pia katika magonjwa ambayo yanahusiana na masuala ya damu ambayo wanaita *blood bloated disease*. Ukiangalia kwenye bajeti mwaka jana palikuwa pana shilingi 20 bilioni ambazo pia walisaidiwa na taasisi kutoka mambo ya nje lakini mwaka huu mashirika ya kimataifa pamoja na taasisi kutoka nchi za nje, naona bajeti imeongezeka kuwa shilingi 24 bilioni. Sasa kwa wale ambao wanaosema kwamba nchi za nchi za nje zimetununia, hawa hapa nataka kujua wanatokea wapi. Nani anayesema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haishirikiani na taasisi za kimataifa. Sasa mbona leo kuna ongezeka la shilingi 24 bilioni, mbona Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi humu ndani pia kenda

kushiriki katika Jumuiya za Madola na nchi 16 ambaye ndiye mimi. Sasa hizi siasa zinapikwa wapi, hizi shilingi 24 bilioni zimetokea wapi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa hawa watu wanakuwa wanapoteza wananchi, serikali iseme ukweli. Rais wetu anatambulika na tunashirikiana na nchi za kimataifa na jana hapa tumemuona Balozi wa Morocco alikuja na mimi kule nilipokuwa Afrika ya Kusini nimepewa pongezi nimwambie Rais anapongezwa sana na nchi tofauti kuhusiana na kwamba kuweza kuanzisha hii pensheni ya shilingi 20,000. Sasa kama taasisi za kimataifa zipo na sisi, hii siasa inayotaka kudanganya watu hebu tuachane nayo na serikali iwaambie wananchi ukweli. Sasa hizi shilingi 24 bilioni mimi naipongeza sana serikali na ni jambo la kheri kabisa.

Sasa nataka niulize suala la *cholera*. Mhe. Mwenyekiti, kila mwaka ukifika wakati wa mvua lazima kuwe na kuna *cholera* lakini hii *cholera* inatutia jina baya na maeneo ambayo yanatokana na hii *cholera* ni yale yale *traditional places,* utasikia Daraja Bovu, Mtopepo, Kinuni. Lakini tatizo kubwa linalokuja sio la Wizara ya Afya ni kutokana na makazi ya watu, kwa sababu haya maeneo pia yamevamiwa na watu, hizi ni *squatters*. Sasa juhudi lazima ifanyike na Wizara husika ya makaazi pia inayosimamia masuala ya maji ili waangalie jinsi gani watakuja na mkakati kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, kwa sababu suala la *cholera* haliwezi likaangukia Wizara ya Afya peke yake na kuondoka, lilikuwepo mwaka jana, litakuwepo mwaka huu na litakuwepo mwaka ujao. Haiwezekani mwananchi anaishi kwenye nyumba hana eneo la kujisaidia, wanaishia Misikitini, watu wanajisaidia nje, watu wanajisaidia kwenye mifuko ya plastiki. Sasa kama hatutabadilika huko na kuwasaidia wananchi wetu hili litaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana *cholera* ilidumu kwa muda wa miezi minane kwenye rikodi ya nchi hii. Tunaishukuru serikali kwa kuwa wawazi na kutoa hizi taarifa katika jamii na maeneo yote, lakini pia haituletei sifa nzuri. Mimi naomba sana mwaka huu wa bajeti hii inapokaa serikali, nione serikali wanakaa pamoja na Wizara husika kuja na mkakati maalumu ambao utakuwa una *short term* na *long term plan* kuweza kuwasaidia wananchi haya maeneo niliyoyataja na mwaka ujao angalau hili jambo lisitokezee wakati wa mvua.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nataka niulize swali alilouliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub, suala la michoro. Kwa kweli Mhe. Waziri angejitahidi juu ya suala hili kulimaliza kwa haraka, muda umekuwa mrefu.

Sasa nataka nigusie sala la takataka ambazo zimeonekana baharini na kukosekana kwenye *incinerator* kutotumika**.** Mwaka jana mwezi wa sita nilimhoji hapa na kumshauri Waziri na nikamuuliza hospitali zote ambazo ni za serikali pamoja na *private*, suala la *waste* wanazotumia zinaishia wapi. Mwaka 2016 nafikiri ilikuwa tarehe 20 na ukenda kwenye *hansard* ataikuta. Waziri akanijibu inakuwaje leo watu wanachoma sindano na *packet* za damu baharini, zimekwenda zimefika mpaka katika bahari ya *ATC* pale *Extelecom* na hili siku ile Jumapili nimekwenda nimeangalia mwenyewe, kwa kweli ilikuwa ni uchafu, uchafu, uchafu. Ni aibu tumeingia katika nchi yetu. Sijui Waziri wetu wa Utalii ameweza kujibu nini huko nje. Maana yake pale tuna hoteli mbili zenye daraja la juu, Wazungu wanakuwepo lakini pia vijana wetu wa Kizanzibari wanacheza mpira, watoto wanakwenda, tumeingia aibu vibaya sana. Mimi nataka kufahamu waliofanya tendo hili baya wamechukuliwa hatua gani za kinidhamu na kisheria ili jambo hili lisijirudie, isiwe tena mambo ya kujuana. Kwa hivyo Waziri atapokuja hapa atueleze yote walioyafanya haya wamechukua hatua gani.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Waziri amekuwa anapiga debe sana suala la *Telemedicine.* Naomba atakapokuja atueleze *issue* ya *Telemedicine* amefikia wapi na tunaendelea nao vipi. Lakini pia nataka nizungumze suala la hawa ma-*specialists* madaktari wetu juu ya mafao yao. Naomba kidogo Mhe. Waziri atuangalizie hili na atueleze pia kwenye mafao hawa ma-*specialists* wetu tulionao katika hospitali zetu tunahakikisha tunawalinda vipi.

Mhe. Mwenyekiti, katika nchi ambayo imepoteza sana madaktari wao ni nchi ya Zimbabwe, ukienda karibu nchi nyingi za Kiulaya, maeneo mengi utakuta Wazimbabwe wapo wanafanya kazi kutokana na kwamba kutothaminiwa na nchi yao. Kwa hivyo suala la mafao kwa ma- *specialists* wetu ni muhumu sana na ni jambo la msingi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze suala la Hospitali ya Binguni. Mhe. Waziri amelizungumza sana hili suala mwaka jana Hospitali ya Binguni. Lakini pia kwenye hotuba ya Mhe. Rais ambayo aliisoma hapa 5 Aprili, 2016 kwenye Baraza la Wawakilishi ukurasa namba 52 anasema, naomba kunukuu:-

"Kadhalika serikali itatekeleza mpango wake wa kujenga hospitali ya kisasa ya rufaa katika eneo la Binguni Unguja".

Mhe. Mwenyekiti, eneo la Binguni ni kweli lipo katika Jimbo la Tunguu ambalo mimi pia ni Mwakilishi wao. Lakini naamini Hospitali ya Binguni ni

kwa ajili ya wananchi wa Mkoa wa Kusini hata na wengine wanatoka mjini lakini na watu wa Kaskazini pia.

Sasa kwenye suala la Hospitali ya Binguni nataka nielewe pia Mhe. Waziri atakapokuja atueleze amefikia wapi kwenye Hospitali ya Binguni na maendeleo yake, kwa sababu kwa hali ilivyo kule Binguni ukipita huhisi kwamba tayari ujenzi unataka kuanza na ukiangalia kwenye Ilani yetu ilizungumzwa sana na muda unakwenda. Je, sasa hii imegeuka kuwa ni changamoto au mambo bado yako pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, suala la wajawazito nataka nizungumze. Ni kweli ukiangalia kwenye hotuba vifo vya wajawazito vimepungua, ametaja idadi Mhe. Waziri nimeiona kwenye hotuba aliyoisoma. Lakini kwa kweli hili tatizo bado lipo. Sasa sijui mimi sisi sio mtaalamu lakini Mhe. Waziri nitapenda utueleze unatumia mbinu gani kuhakikisha haya mambo yote juu ya vifo vya akinamama hasa wakati wa uzazi unalitokomeza.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie la mwisho nataka nizungumzie suala la *mortuary***.** Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar sasa tunapokea wageni wengi ambao wanaokuja kwa ajili ya matembezi lakini kwa mapumziko, pia kutembelea familia. Lakini pia Uwanja wetu wa *Airport* sasa tunaoutangaza kwamba Uwanja wa Kimataifa tunategemea utakuja kwisha katika miezi inayofuata. Lakini pia tunategemea hata michezo ya baharini na michezo pia wa kwenye anga itazidi kuongezeka kama *diving, water sport* pamoja na mambo ya *sky diving*.

Mhe. Mwenyekiti, ajali haina kinga. Mimi nilipokuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wakezaji Sekta ya Utalii niliulizwa swali moja siku moja tukafanya *scenario,* nikaambiwa Simai ukipigiwa simu saa sita za usiku, ukiambiwa basi linakwenda Kiwengwa limegongana na basi la abiria, unaambiwa kuwa kuna wazungu 35 wamefariki, 20 wako mahatuti utafanya nini. Nikawaambia mimi nitazima simu nitaingia chini mvungu wa kitanda. Nikaulizwa kwa nini, nikajibu sina cha kuwafanya maiti nitawapeleka wapi. Kwa sababu la kwanza maiti siwezi kuwachukua tukawapeleka katika mahoteli katika *cold room* zao ambazo wanahifadhi chakula itakuwa haipendezi na wengine hawatakubali. Sasa utafanyaje. Namwambia kumzika huwezi kwa sababu mzungu huna haki ya kuweza kumzika kwa sababu wenyewe watadai maiti yao wakamzike kwao, wengine wanataka kuchoma na wengine wanataka kuzika. Sasa utafanyaje, nikawambia hakuna pa kuwahifadhi itabidi tukawazike au twende Kama.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nashauri sana wakati umefika sasa serikali kuwa na *mortuary* ya kisasa ili kujipanga kwa mambo ya *disaster*. Na ni kweli nikiri

kwamba jambo hili ninapolizungumza hatuliombei lakini inabidi tujitayarishe. Matukio kama haya yametutokezea na sisi kama tunahitaji wageni wa nje wanaokuja hapa kututembelea lazima tuhakikishe pia linapotokea lolote tuweze kuwahifadhi maiti zao, hatuna haki sisi kwenda kumzika mzungu yeyote kwa sababu wenyewe wana mambo yao pia, sisi tuna Dini yetu na mila yetu na utaratibu wetu.(*Makofi*).

Kwa hiyo, mimi naomba sasa kama Zanzibar tunaingia katika *International Destination* basi tujitayarishe na *mortuary* ya kisasa. Najua jambo hili mtanisamehe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Waheshimiwa wenzangu pamoja na Mawaziri, lakini ni jambo la msingi kuwa na *mortuary* ya kisasa ili tuweze kuwahifadhi panapotokezea janga. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi baada ya hayo naomba kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu, naunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia juu wa Wizara hii kwa umuhimu na juhudi zilizochukuliwa na nakuhakikishia sitopiga buti yoyote na sio kawaida yangu, lakini kutokana na mambo ambayo yamejitokeza Wizara hii na *improvement* niliyoiona na hasa katika masuala ya bajeti kuona asilimai kumi, naunga hoja mkono asilimia mia juu ya mia.

Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidh akifuatiwa na Mhe. Bahati Khamis na Mhe. Salma Mussa Bilal ajitayarishe.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyeiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia wizara muhimu ambayo inaangalia afya zetu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba ku-*declare interests*. Mhe. Mwenyekiti, kiasi miaka miwili na nusu iliyopita mtoto wangu aliuliwa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja na nikaambiwa bahati mbaya kapita, mpaka leo nimeshindwa kufahamu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ulikuwa ni uzembe tu, yaani *I was there* nilikuwa naona ni uzembe uliofanyika hapa. Kwa hivyo naomba kwanza ku-*declare interest* Mhe. Mwenyekiti, ni uzembe hata kupoteza kijana wangu pale katika Hospitali ya Mnazi mmoja ni uzembe.

Mhe. Mwenyekiti, la pili baada ya ku-*declare interest* naomba kuchukua fursa hii ya kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kweli tumeona kila Rais aliyeongeza nchi hii alikuja na

agenda yake mfukoni. Lakini tumeona Mhe. Rais Ali Mohd Shein ana agenda ya kuendeleza huduma bora za afya Zanzibar, tumeona wote ni mashahidi. Lakini Rais Ali Mohamed Shein amekuja na ageda yake ya kuleta huduma bora ya afya Zanzibar, amejenga hospitali nzuri Pemba, amejenga lile jengo la akinamama na watoto pale lipo zuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nampongeza sana na asiyempongeza Rais na kumshukuru kwa ku- *improve health service* Zanzibar huyo tena atakuwa na lake na Mwenyezi Mungu amlaani. Lazima Rais tumpongeze kwa hili, tunampongeza kwa sababu anataka kuhakikisha huduma za afya Zanzibar zinakuwa-*improve*.

Mhe. Mwenyekiti, tuona bajeti ya Wizara ya Afya wanachokiomba wanapewa. Mhe. Mwenyekiti, tumeona Mhe. Waziri mwenyewe kakiri kwamba Wizara ya Afya wanachokiomba wamepewa karibu asilimia mia ya bajeti wanachokiomba. Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi mazuri yamefanywa.

Halikadhalika napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri anachukua jitihada kubwa ya kutaka mambo ya afya Zanzibar yawe mazuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema tena kwa kumshukuru tena Mhe. Waziri, nimetembelea pale *Mental Hospital* alhamdulillahi chakula wanacholishwa wale wagonjwa wa akili ni chakula kizuri. Naomba kumpongeza sana Mhe. Waziri Lakini ukweli usiofichika pale *Mental Hospital* wale watu wanaishi mazingira ya uchafu na uchafu umekithiri. Chakula wanalishwa kizuri mimi shahidi lakini uchafu umekithiri kiasi ambacho ukiingia mle utaona huruma na watu wa kufanyakazi wapo, lakini kazi hawafanywi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba kama hawataki kazi kawafukuze wote lakini wawasafishie wale watu uchafu umekithiri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, si siri hata kuna kuwa na nyoka mule mwiti umekuwa mkubwa, mabanda yao wanayolala kayatizame Mhe. Waziri utalia machozi, nenda ukatizame. Lakini mimi naomba kukiri na kusema kwamba kazi ya huduma ya afya, daktari na mwalimu ni kazi ya *charity*. *Mahatma Gandhi* kasema ni kazi ya wito, kazi ngumu wenzetu wanafanya, watizamwe kimaslahi. Nchi hii anayefanya kazi ngumu ni daktari lakini mshahara mzuri anaoupata mkurugenzi. Mhe. Mwenyekiti, tuwatizame watu hawa wanafanyakazi kubwa ngumu lakini mkurugenzi anapata mshahara mzuri na kazi anaifanya daktari na mwalimu.

Mhe. Mwenyekiti, bibi yangu ameniambia kuwa mjuu wangu unaposema sema "usiseme yote mengine ubakishe". Mhe. Mwenyekiti, leo nitasema lakini

mengine nitabakisha sitosema yote lakini nitasema. Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi Serikali ya Zanzibar inafanyakazi kubwa kuhakikisha huduma za afya zinakuwa *improve* zinaendelea. Lakini *wallah* Mhe. Mwenyekiti, pesa serikali inatoa nyingi. Jicho la serikali lote lipo katika Wizara ya Afya hasa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini nataka niseme katika jambo linaloitia mdomoni serikali yetu, katika jambo linaloifanya serikali yetu isemwe vibaya, katika jambo linaloifanya serikali yetu izungumzwe sana, hakuna kama Wizara ya Afya hasa Hospitali ya Mnazi Mmoja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, si siri inatuchafulia serikali, Hospitali ya Mnazi Mmoja inatuchafulia Chama cha Mapinduzi, inatuchafulia wapiga kura wetu, wanasema vibaya na wanayosema wananchi yote ni ya kweli. Wananchi walalamika sana Mhe. Mwenyekiti, walia machozi wananchi kwa sababu Hospitali ya Mnazi Mmoja huduma mbovu, serikali inachukua jitihada kubwa kutoa pesa, jicho la serikali liko pale lakini huduma yote mbovu, *almost* yote, natumia neno *almost* yote mbovu. Kwa sababu ukitaka ushahidi kama yote mbovu katizame malalamiko ya wananchi, kawachukuwe wananchi kumi uwaulize, wote wanalalamika na wote wanalia. Hiyo ni ushahidi Mhe. Mwenyekiti, kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja huduma inayotolewa *almost* yote mbovu ingawaje serikali inatumia nguvu nyingi, inatumia pesa nyingi inatumia nguvu nyingi katika kuwatafutia huduma bora wananchi wake. Lakini bado Mhe. Mwenyekiti, huduma za Hospitali Mnazi Mmoja *almost* zote mbovu. Tatizo ni nini, *management*, watu, kuna tatizo gani jamani Hopitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo liko Mnazi Mmoja ndio maana wananchi wanalalamika, ndio maana huduma sio nzuri, ndio maana huduma mbovu. Tatizo Mnazi Mmoja Mhe. Mwenyekiti, lipo *why*? Serikali inachukua jitihada kubwa na kila serikali inapochukua kubwa ndio huduma zinapozidi kudidimia kubwa mbovu Mhe. Mwenyekiti. Kama utakwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja mimi katika pahali ninapokwenda sana, asubuhi wa leo nilikuwepo, kila mwananchi analalamika. Naomba sasa nianze kuyatoa malalamiko ya wananchi Mhe. Mwenyekiti, na kila mtu ayasikie.

Mhe. Mwenyekiti, vifo vimekithiri Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mhe. Mwenyekiti, si siri mtoto wangu mimi pale nilisema nime-*declare interest* alikufa lakini aliuliwa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mohd Hassan mtoto wangu kwa uzembe hakuna chengine, wakaja kuniambia kapita, bahati mbaya, maneno haya nayatafutia maana yake sijayapata mpaka leo mpaka nitakufanya sipati maana yake maneo bahati mbaya, sijui kapita, sijui si riski. Nini maana ya maneno haya. Mimi sijayajua mpaka leo na sitoyajua mpaka nitakufa. Mhe.

Mwenyekiti, ukaniambie habati mbaya kifo cha mwanangu, umepata kuona neno hilo wewe, kwa uzembe ukaniambie bahati mbaya, *what you are talking about*. Mhe. Mwenyeki, uzembe umekithiri Hospitali ya Mnazi Mmoja. Lipo jambo Hospitali ya Mnazi Mmoja, wananchi wasingelalamika kama wanavyolalamika. Serikali inachukua jitihada kubwa lakini wananchi wanalalamika. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wawakilishi 27 tulikwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kuangalia hali ya usafi. Mhe. Mwenyekiti, hayasemeki tukiyoyakuta pale. Bajeti iliyopita nilimwambie Waziri ndege anazaa kwenye madirisha, akasema lete ushahidi, atwambie leo nilete ushahidi umejaa ushahidi tunao ushahidi, maana yake tuna kila kitu Mhe. Mwenyekiti, aseme leo kwa uchafu. Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja haisafishwi, vyoo Mhe. Mtumwa kasema hapa havisemeki. Chaa aibu na cha kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, tumekwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja Wawakilishi 27 jengo jipya lile mauwa bado yapo mlangoni ya kufunguliwa lile jengo jipya, wallah damu zipo kunako *flow* ya Mnazi Mmoja zimejaa na wenyewe watendaji baadhi yao walitokea pale wameona tunawaonesha jamani inakuwaje, jengo jipya maua bado yako katika milango ya kuonesha kwamba hii hospitali imefunguliwa juzi tu kishindo cha jana, basi damu zimejaa kwenye *flow* jengo jipya Mhe. Mwenyekiti. Hospital ya Mnazi Mmoja haisafishwi chafu mpaka inatia aibu, ukitaka kuumia wewe na kuzidi maradhi uende kunako hivyo vyoo utizame hayo mafeni Mhe. Mwenyekiti, uchafu umekithiri.

Baada ya *point* hiyo Mhe. Mwenyekiti, chengine cha kusikitisha nina mwanachi wangu katika kipindi kama cha mwezi mmoja na nusu ulizimwa umeme saa nane kajifungua, kitoto chake kimetiwa kwenye *incubator* basi wallah umeme ukazimwa saa nane kile kitoto saa 11:30 kikafariki. Mhe. Mwenyekiti, jenereta lipo chini pale tangu liletwe na picha tunazo kwenye simu tunapigiwa picha linashushwa, leo ni miezi 4 na siku 17 tangu liletwe niliwahi kumwambia mpaka Mhe. Waziri mtalifungua lini, akasema hana pesa. Lakini cha kushangaza kama alivyosema Mhe. Abdalla Maulid Diwani kila siku wako juu utafikiri ndege kwa kusafiri.

Lakini inashindikana milioni kumi ya kulifunga jenereta, mimi sijawahi kuona jambo hili na ni aibu kusema kuwa hakuna pesa. Serikali ya Mapinduzi Zanzibari ikashindwe na milioni kumi, serikali inayochukua jitihada kubwa ya kutaka huduma za afya ziendelee, leo milioni kumi. Mimi sikubaliani itakuwa lipo jambo Hospitali ya Mnazi Mmoja, mnatufanyia kusudi, mbona pesa za kusafiri mnapata, ikashindikane pesa ya kutoa milioni kumi kulifunga jenereta.

Mhe. Mwenyekiti, jenereta limebakisha miezi mitatu kumaliza *warrant* wenyewe wazungu aliotoa jenereta wanasema kwamba hawajawahi kuona kwamba jenereta limebakisha miezi mitatu kumaliza *warrant* wa kiwanda bado lipo chini halijafungwa, watu wanakufa, umeme unazimwa lakini jenereta tumeshagaiwa lakini lipo chini inashindikana milioni kumi. Mimi naona mnafanya kusudi Mhe. Mwenyekiti, wana Mapinduzi wanakuoneni hii ni kusudi haiwezekani mbona pesa za kusafiria zinapatikana mtatufanyia kusudi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, chengine juzi leo ni wiki ya pili mpaka Mhe. Waziri nimemwambiwa maji tumekwenda sisi watu 27 maji hayatoki, watu wote wana vidumu na juzi mimi mwenyewe nimemwambia Mhe. Waziri tumepandisha maji kwa madumu pale watu wanaumwa hawezi kukataa huyo hapo akatae. Hivyo kweli Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yanashindikana maji, hii ni kweli, hii si mnatufanyia kusudi. Serikali jitihada yote inayochukua ya kwamba *health improvement* ziwe nzuri lakini bado maji ni tatizo katika Hospitali ya Rufaa, hii inawezekana kweli.

Mimi sijapata kuona Mhe. Waziri hii mnatufanyia kusudi na hatukubali kwa sababu mnaitia mdomoni serikali yetu, mnaifanya serikali yetu inasemwa vibaya kwa sababu ya huduma ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na serikali itanajitahidi. Sasa lakini Mhe. Waziri Baraza hili la Tisa lazima lipate ufumbuzi, kwa sababu tunaisifu sana serikali, tunamsifu sana Rais, kazi anafanya kubwa lakini haifanani na huduma inayotolewa na Hospitali ya Mnazi Mmoja.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, chengine vipimo. Mhe. Mwenyekiti, imekuwa ni dawa unaambiwa nenda Hospitali ya Al-Rahma Kilimani, nenda Global ukapime aah! Hivyo mtu binafsi akatushinde serikali, vipimo kumbe vimo ndani vyote vimo hivyo lakini hupati Mhe. Mwenyekiti, unaambiwa Al-Rahma, Global basi, yaani hata hakutizami daktari uelekee Al-Rahma, ukienda Al-Rahma, Global elfu tisini utoe, unaipata wapi mnyonge mkulima na mkwezi si mnatufanyia kusudi na vipimo vyote Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, serikali inachukua jitihda kubwa ya kutaka kuendeleza huduma za afya, hii mnatufanyia kusudi. Sasa umefika wakati lazima kung'amuwe.

Mhe. Mwenyekiti, chengine juzi alipata mtu ajali kapelekwa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja saa saba na nusu za usiku na mimi nipo, kaumia mbavu kakatika ana-*internal bleeding*, tukatafuta *X-ray* tukaambiwa asubuhi heee! mimi sijapata kuona. Hospitali duniani vipimo vyote unavipata asubuhi kwani tumeambiwa ajali zinatokea asubuhi tu, katwambia nani maneno hayo kuwa

ajali zipo asubuhi. Vipimo vyote Hospitali ya Mnazi Mmoja unavipata asubuhi tena mwisho saa saba, tena kwa idadi ya watu. Mhe. Mwenyekiti, hatufanyiwi makusudi. Mtu yule kufika saa 11:30 kafa, hajapimwa vipimo kaambiwa asubuhi kafika asubuhi hakufika kafa. Sasa kamuua nani? wamemuua watu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ahadi yake ilikuwa bado kwa sababu angepimwa angejulikana yule mtu wapi ana tatizo angepata kutibiwa. Lakini vipimo usubiri watu wa asubuhi waingie mabwana wakubwa wanavyotaka saa sita saba, tena wanakuwambia tu bila ya tatizo watu 27 hao hao hata kama unataka kufa hawaongezi, tena wewe na Mungu wako. Mhe. Mwenyekiti, tumechoka mambo kama hayo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hospitali duniani vipimo vyote vinapatikana masaa 24, kama mtu ana *death threat* lazima akapimwe ajulikane kama ana tatizo gani, apate kutibiwa unasubiri saa saba, saa hiyo hafiki haya, kumi na moja yule kapelekwa saa 7:30, saa 11:20 juu ya alama kakata roho mimi nimepeleka gari tumeenda kuchukua tumekwenda kumzika, kamuua nani, Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, chengine ulinzi. Mhe. Mwenyekiti, mnaleta ulinzi wale watu tumechoka pale mkumbuke Mnani Mmoja ni sehemu inayotoa huduma kwa wananchi wanyonge, mnawaletea wale watu wanakuja kutulinda kumbe wanakuja kuwanyanyasa wananchi, kwa sababu wanapata pesa za kulipwa. Mhe. Mwenyekiti, wekeni watu wenye kujulikana kama vikosi wananyanasa watu.

Mhe. Mwenyekiti, wale watu wanawanyanyasa watu na tunawajua. Mtu hana mafunzo anachukuliwa mtaani, leo Juma kakosekana nenda wewe, akienda yeye anamwambia mwananchi, wee! mwananchi ondoka hapo anamtukana. Juzi Mheshimiwa mmoja kamtukana humu mpaka kalia machozi. Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba sana Mhe. Waziri watu wale uwaondoshe hatuwataki, kazi yao wanatunyanyasia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika hospitali binafsi. Mhe. Mwenyekiti, tunazo hospitali binafsi, hizi hospitali binafsi mnapozisajili basi mzitizame zimekuja kututibia wananchi au zimekuja kutaka kutuulia wananchi. Natoa mfano wa Hospitali ya Al Rahma. Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Al Rahma ukitaka kufa tu basi inaitwa *ambulance* unapelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwani wameambiwa na nani kama Hospitali ya Mnazi Mmoja ni hospitali ya kuulia. Ukianza kuumwa vibaya tu mbio lete *ambulance* unapelekwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, vifo vyote vinavyotangazwa vimetokea Hospitali ya Mnazi Mmoja, sio Hospitali ya Al Rahma.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nakuambia wamekwenda kumzalisha mtu ana miezi saba kumbe *incubator* hawana mtoto akafa wamemuuwa Al Rahma. Sasa nakuambia Mhe. Waziri, kama Hospitali ya Al Rahma sio hospitali basi ifungiwe Zanzibar isionekane hapa hatuitaki, kwa sababu sio hospitali ni chombo kimekuja kukusanya pesa za *NHIF*, pesa za *insurance* tu. Juzi wameshalipwa dola 880,000 za *insurance*, kazi yao kukusanya pesa za *insurance* lakini sio kazi yao kutibu. Chombo cha *private* kinachotoa matibabu lazima kiwe *up todate*, tukatizameni vyombo vya wenzetu, kile ni chombo gani kazi yake kukusanya *insurance*, wanajitia Uislamu, Uislamu wenyewe wa kubabaisha, halafu wanatibu watu, wale waongo tu Mhe. Mwenyekiti, wanakuja kuwadanganya watu tu hawana matibabu mamoja hatuwataki Hospitali ya Al Rahma hapa Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine nakupongeza sana, nampongeza sana Mhe. Waziri na Mhe. Rais. dawa Hospitali ya Mnazi Mmoja zipo *alhamdulillah*. Lakini sitaki kumtaja mtu na tarehe, lakini dawa Mhe. Mwenyekiti, hospitali ya Mnazi Mmoja huzipati mpaka kwa *c/o*. Tarehe fulani naihifadhi, kuna mgonjwa fulani alilazwa, alipolazwa akapewa ki-*note* kanunuwe dawa, hizi na hizi ni mgonjwa wa Mhe. Mhe. Waziri wale watu wanamtizama Mhe. Waziri wakasema dawa hizi zipo kwa kuamini kabisa. Akachukua kalamu akaandika ki-*note*, eeh! alipokwenda kule akaambiwa mgonjwa wa Mhe. Waziri huyu zile dawa zote akapewa, tena kuanzia hapo akaanza kutizamwa. Sasa kumbe dawa Hospitali ya Mnazi Mmoja zipo lakini mpaka ujulikane mgonjwa wa Waziri, mgonjwa wa Mheshimiwa, mgonjwa wa Rais, mgonjwa wa Spika, utatibiwa vizuri na dawa utapewa. Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kwenda, hii ni nchi ya kikwezi na kikulima ndio wenyewe, hii nchi ya wana mapinduzi, hii nchi yetu sote.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri hatuwezi kwenda namna hii. Leo nimesema jambo lipo Mnazi Mmoja. Kwa nini hospitali ya Mnazi Mmoja matibabu mazuri huyapati mpaka kwa *c/o* haiwezekani. Ndio maana watu wanawatoa wagonjwa wao wakawapeleka Fuoni kwa waganga kwa sababu akitoka anaambiwa dawa, akitoka anaambiwa kapime vipimo Al Rahma, kapime *Global*, mnyonge anaipata wapi, mkwezi na mkulima anaipata wapi, ndio wanapowapeleka watu wagonjwa wao halafu mkawalaumu kwa sababu ya uwezo. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba hili hatulitaki.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jengine wataalamu Zanzibar tunao wa kutosha wa mambo ya matibabu, lakini wote ni Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, wakubwa wa hiki. Hata mmoja juzi ananiambia mimi mheshimiwa kwa sababu Mkuu wa

Kitengo na Mkurugenzi, hata huko kutibu nimeshasahau, lakini huenda kujitolea mwenyewe pale Hospitali ya Mnazi Mmoja ili nisisahau ujuzi wangu. Mhe. Mwenyekiti, sio utaratibu. Katika nchi za wenzetu utendaji anapewa mtendaji aliyesomea *management* na kutibu apewa mtu anayejua kutibu, ndio mkuu wa *faculty* ya kutibu. Lakini hapa Wakurugenzi 14 wa Hospitali ya Mnazi Mmoja wote ni Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo wote ni madaktari *qualified* na wote ndio Wakuu wa Vitengo anatibu saa ngapi. Halafu tunasema tuna tatizo kwamba hatuna wataalamu madaktari, madaktari tunao lakini tumewapa wote Wakuu wa Vitengo, Wakurugenzi inakuwaje. Katika nchi za wenzetu *management* anapewa mtu aliyesomea *management*, daktari unampa Ukurugenzi inakuwaje, haiwezekani. Daktari unampa Ukuu wa Kitengo inakuaje haiwezekani atatibu nani. Mhe. Mwenyekiti, wale watu wanatakiwa wawepo hospitali wanafanya operesheni, wale watu wanatakiwa wawepo hospitali wanaangalia kufanya maabara, lakini wote leo wamekuwa wakubwa, asubuhi wanavaa suti na guo jeupe wameshalisahau hata linakuwaje. Mhe. Mwenyekiti, huu sio utaratibu, wataalamu wengi tunao lakini tunawakosa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais ametangaza nchi hii huduma za akinamama na watoto wapewa bure, lakini bado Hospitali ya Mnazi Mmoja huduma za akinamama zinatolewa sio bure na tena kwa matusi wanawatukana watu wetu, huyo Rais wenu aliyetangaza vitu viko wapi na kumbe vitu vipo mpaka upate kwa *c/o*. Mhe. Mwenyekiti, haya yote yapo Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa mfano sasa. Nataka kuliomba leo Baraza lako tukufu lije na kitu fulani. Mhe. Mwenyekiti, *in conclusion* naomba kusema yafuatayo. Swaziland walikuwa na tatizo kama letu, serikali inatoa pesa nyingi kupeleka Wizara ya Afya, lakini huduma zilikuwa mbovu. Mbunge mmoja wa Swaziland akapeleka hoja binafsi katika Bunge la Swaziland ili kuliomba Bunge tukufu liende likafanye utafiti kwa nini serikali inatumia pesa nyingi lakini huduma mbovu, ambalo ndio tatizo tulilokuwa nalo sisi, serikali inatumia pesa nyingi lakini kuna huduma mbovu.

Mhe. Mwenyekiti, UK serikali ya *Labour* ilikuja na hoja binafsi ya Bunge kwa nini serikali inatumia pesa nyingi lakini huduma mbovu. Mbunge wa *Labour* akaja na hoja binafsi. Mhe. Mwenyekiti, kilichotokezea ikaundwa *NHS* Mhe. Waziri unaijua. Leo ndio chombo kizuri kinachotoa huduma bora nchini Uingereza kwa hoja binafsi za Wabunge, na kwa kuunda Kamati Teule za kwenda kuchunguza kwa nini serikali inatoa pesa nyingi lakini huduma zinazopatikana ni mbovu. Tatizo tulilonalo Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, sio siri serikali alhamdulillah Mwenyezi Mungu aiwezeshe inatumia pesa nyingi Wizara ya Afya, lakini huduma tunazozipokea ni mbovu. Mhe. Mwenyekiti,

tatizo lipo tena kubwa tusifichane kwa sababu wananchi wasingekuwa wanalalamika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi Mwakilishi wa Jimbo la Welezo Hassan Khamis Hafidh, Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na wananchi wetu wanavyolalamika na wanavyoitia mdomoni Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na serikali tunaishukuru sana inajitahidi kadri ya uwezo wake kuipa pesa Wizara ya Afya ili mambo yawe mazuri, lakini bado mambo ni mabaya. Kwa hivyo, naliomba Baraza lako Tukufu leo kwenye mwezi huu wa Ramadhani. Swaziland na Uingereza walifanikiwa baada ya kuona kuna matatizo na pesa ni nyingi, waliunda Kamati Teule. Mhe. Mwenyekiti, tumezowea kuunda Kamati Teule humu ndani kwa kwenda kuchunguza pesa tu, lakini tuna huduma mbovu Hospitali ya Mnazi Mmoja tunazipata, zogo limekuwa jingi, hatari tupu, vifo vingi hata watu hawajali, ukishakufa unafungwa mfungo wa pipi wewe na Mungu wako, hata hawaogopi, kuogopa kule hawaogopi.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii ni kubwa. Naliomba Baraza lako tukufu leo Mhe. Mwenyekiti, kutumia Kanuni, tuwache kabisa kuunda Kamati Teule kwa kwenda kuchunguza pesa, tuunde Kamati Teule, naona unawasha taa, kwa kwenda kuchunguza kadhia ya huduma mbovu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuitumia Kanuni ya 111, mimi Mwakilishi wa Jimbo la Welezo Hassan Khamis Hafidh, bado huduma ni mbovu Hospitali ya Mnazi Mmoja ingawaje serikali inatumia pesa nyingi, tuunde Kamati Teule tukachunguze kadhia ya Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo inafanya serikali yetu isemwe vibaya, tujuwe tatizo ni nini. Kanuni inasema hivi, naomba uisoma:-

Kanuni ya 111

"Baraza linaweza kuunda Kamati Teule kwa ajili ya jambo fulani".

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 111 jambo fulani Hospitali ya Mnazi Mmoja lipo, wananchi wote wanalalamika. Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumika Katiba ya Chama cha Mapinduzi, ahadi za mwanachama wa Chama cha Mapinduzi tukiwe humu wengi ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi isipokuwa wawili tu ambao pia wanafuata sera za Chama cha Mapinduzi chama makini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema nitajitolea nafsi yangu kuondoa umaskini, ujinga, ugonjwa, maradhi na dhulma. Mhe. Mwenyekiti, maradhi tunayo mengi na

matibabu bora tunayakosa ingawaje serikali yetu inafanyakazi kubwa. Naomba sana Wajumbe wenzangu kwa heshima kubwa na taadhima kubwa, kwa kadhia tuliyonayo Hospitali ya Mnazi Mmoja na serikali yetu inajitahidi tuunde Kamati Teule tukachunguze jambo fulani pale Mnazi Mmoja. Nimechukua Katiba nyote mnaiona, nafikiria ndani ya nafsi yangu hakuna atakayelikataa hili. Tunapokuja kupiga kura tukubalini, hatwendi kuchunguza pesa, tunakwenda kuchunguza jambo fulani ili serikali yetu ipate *improvement*. Swaziland wamefanikiwa, Uingereza wamefanikiwa na sisi Mwenyezi Mungu atatujaalia tutafanikiwa na tutapata *solution* ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache naamini kwamba hakuna Mjumbe hata mmoja tutakapokwenda kwenye kura ya kuunda Kamati Teule hata hatonyoosha mkono wa ndio, na atakayenyoosha mkono wa sio, huyo tutamjua ni mpinga mapinduzi, mpinga maendeleo na huyo sio mtu aliyekuja humu kuwawakilisha wananchi, atakuwa amekuja humu kwa kuiwakilisha nafsi yake.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Bahati Khamis akifuatiwa na Mhe. Salma Mussa Bilal na Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na pili nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kutujengea hospitali mbali mbali zilizo nzuri ili tukuondoshea matatizo wananchi wake. Nampongeza sana Mhe. Rais kwa kutujengea Hospitali ya Abdalla Mzee iliopo Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wao kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba niende moja kwa moja katika ukurasa wa 38 unaosema, "Programu ndogo ya huduma za matibabu". Mhe. Mwenyekiti, tunaishukuru sana wizara huko nyuma imefanya kazi kubwa sana ya kuleta matibabu mbali mbali na kuondosha maradhi ambayo kuwa yalitusakili kwa muda mrefu sana, yakiwemo malaria, pepopunda na surua. Kwa hivi sasa tunamshukru Mwenyezi Mungu kwamba maradhi haya yamepungua kwa kiasi kikubwa sana.

Pia Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na Mhe. Mtumwa Suleiman kuhusiana na Hospitali ya Kivunge. Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Kivunge tunaipenda sana na ni nzuri lakini jambo la kusikitisha ni kwamba madaktari wengi wapo, lakini dawa zimekuwa ni kidogo mno. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aitembelee hospitali ya Kivunge na vile vile kama kuna ugawaji wa dawa ambao anagawa, basi tunamwambia kwamba hospitali ile dawa ni kidogo aongeze idadi ya dawa katika Hospitali ya Kivunge.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea vile vile katika ukurasa wa 46 kuhusu mradi wa kupandisha hadhi hospitali za wilaya na vijiji. Mhe. Mwenyekiti, katika hospitali ya Ukutini mwanzo wa kufunguliwa pale Mhe. Vuai Shamsi Nahodha aliipandisha daraja ile hospitali ya Ukutini. Lakini ni jambo la kusikitisha sana kwamba hospitali ile imeungana na Hospitali ya Mtangani, Chambani pamoja na Ukutini yenyewe, lakini hapana madaktari. Hivi sasa ninavyokwambia Mhe. Mwenyekiti, daktari aliopo ni mmoja tu daktari wa kike. Daktari huyo huyo atibu magonjwa, apime waja wazito, awapime watoto wadogo na matatizo mengine yakitokea pia, kwa kweli ni mtihani. Sasa sijui ni sababu gani Mhe. Mwenyekiti, hata Hospitali ya Ukutini pakawa na daktari yule mmoja tu wa kike na tukiangalia nyumba mbili zipo nzuri na za kuhamia madaktari na wakaweza kufanya kazi zao kwa ufanisi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kujibu hoja zetu basi anieleze ni sababu gani zilizopelekea Hospitali ya Ukutini pakawa na daktari mmoja tu wa kike.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende Chambani. Mhe. Mwenyekiti, Chambani pana daktari mmoja wa kike na mmoja wa kiume lakini ile hospitali yenyewe hasa haina thamani, ni hospitali ambayo kuwa ni ya zamani. Vile vile tukiangalia inahitaji kupatiwa nyumba, hapana nyumba ya madaktari. Wale waliopo mmoja anakaa Ngezi na mmoja anakaa Ukutini, hapajulikani wapi wakae. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri afanye juhudi zake za kina lakini katika Hospitali ya Chambani ipatikane nyumba na wafanyakazi wa kutosha, kwa sababu Chambani ni kubwa mno kwa madaktari wawili tu hawatoshi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika hospitali ya Wambaa. Katika hospitali hii ipo nyumba nzuri na madaktari wawili wapo, lakini nimwambie Mhe. Waziri ile nyumba haikaliwi. Sasa sijui ni kwa sababu gani hata madaktari nyumba ile ikawa hawakai. Nakuomba Mhe. Waziri utakapokuja unipe sababu ya kutokukaa madaktari katika nyumba ile.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, hospitali ile inahitaji wafanyakazi wa kutosha kwa sababu kule Wambaa ni eneo kubwa mno na wale madaktari pale ndio hawakai, ikitokea dharura ni tatizo, inabidi kukodi gari wananchi na kwenda

moja kwa moja katika Hospitali ya Mkoani. Hebu tuangalie mzazi atoke pale usiku Wambaa mpaka afike Mkoani, yuko katika hali gani. Mhe. Waziri naomba uliangalie kwa kina suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli katika hospitali zetu ambazo zinajitahidi sana hivi sasa ni hospitali ya Mkoani peke yake katika Wilaya yetu ya Mkoani. Katika vituo vidogo vidogo vyote Mhe. Mwenyekiti, vina matatizo. Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri avitembelee vituo vile ili kwenda kuyaona matatizo yaliopo na yaweze kutatuka, kwa sababu mimi naamini Mhe. Waziri wewe unapewa taarifa tu, lakini yale matatizo tuliyonayo kule huwezi kuyajua. Hebu acha yote lakini uondoke wewe pamoja na Wajumbe wako wa Baraza walio ndani ya majimbo yale, mwende mkazikague hospitali zile ili uweze kuona yale matatizo ambayo yapo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ukija katika hospitali ya Mtangani ni jambo la kushangaza sana kama daktari atoke Ukutini aende katika Jimbo la Kiwani kufanya kazi iliopo Hospitali ya Mtangani, lile ni tatizo na akiondoka daktari yule pale Ukutini, akienda Mtangani ni tatizo kwa sababu pale hapana daktari tena mwengine ambaye ataweza kushughulikia pale Ukutini. Sasa namuomba Mhe. Waziri madaktari wengi ambao anawapeleka Pemba, lakini madaktari wale wanaofaidika ni katika hospitali za mjini sio za mashamba, kwa sababu hawataki madaktari kukaa katika hospitali za shamba ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nirudie tena katika Hospitali ya Abdalla Mzee, pale kuna madaktari ambao wanakaa Chake Chake kutokana na usumbufu wa nyumba. Mhe. Mwenyekiti, tukizingatia kama kweli tunataka serikali isiingie hasara tumekodi gari aina ya *bus, bus* lile linawapeleka wafanyakazi asubuhi pengine wafanyakazi wawili au watatu linarudi na mchana linakwenda tena kuwachukua wafanyakazi wawili wanaoingia saa 8:00 na usiku wanachukuliwa tena wafanyakazi watatu kuingia saa 3:00.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka serikali isipate hasara au tunaiingizia hasara hasa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aje anijibu ni sababu gani zilizopelekea kwa nini tusichukuwe lile gari ndogo liliopo pale hospitali tukaweza kuwapeleka wale wafanyakazi wetu kwenda na kurudi na tukakodisha *bus* kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja katika huduma za uratibu wa wauguzi na wakunga. Mhe. Mwenyekiti, tunao wakunga ndani ya vijiji, wakunga wale ndio wanaotusaidia akinamama tulioko vijiji, kwa sababu baadhi ya vijiji vyengine kama tunavyoona hospitali zipo mbali na hali zao ni duni,

hawawezi kukodi magari wakapelekwa hospitali mpaka liwe tatizo limekuwa kubwa sana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba wale wakunga ambao wako vijijini wapewe taaluma za kutosha ili waweze kuvitumia vile vyombo ambavyo walivyopewa kwa ajili ya kuwazalishia akinamama. Ningemuomba sana Mhe. Waziri afanye bidii ya kuwapatia semina angalau kila baada ya miezi mitatu siku moja au mbili, ili waweze kupata maelekezo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi ya kueleza kwa sababu tayari wenzangu mengi tu wameshayaeleza. Lakini namuomba Mhe. Waziri ayasikilize sana na ayazingatie sana maneno aliyoyazungumza Mhe. Hassan Khamis Hafidh, kwa sababu tatizo la Hospitali ya Mnazi Mmoja limetugusa sote sio Mhe. Hassan peke yake. (*Makofi*).

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 75 nipewe jawabu nne ndio niweze kutimiza 25.

Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Bahati Khamis Kombo kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Salma Mussa Bilal, atafuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Khadija Omar Kibano ajitayarishe.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia fursa ya kuchangia hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi sina budi kumshuruku Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kunipa uzima mchana huu kuweza kuchangia hotuba hii.

Pia Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na kuweza kutuletea kitabu hichi na leo tukawa tunachangia katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nianze katika ukurasa wa 15 kipengele cha "huduma ya afya ya uzazi na mtoto". Mimi naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi zake za makusudi za kutaka kukuza sekta ya afya hapa kwetu Zanzibar. Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein alichukua juhudi za makusudi za kuwapunguzia mzigo akinamama katika hospitali au katika Wizara ya Afya, hali hii au hatua hii ni ya kupigiwa mfano kwa Rais wetu huyu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Mhe. Rais lakini bado kuna changamoto mbali mbali ambazo wenzangu wameshaieleza, lakini kwa kuwa na mimi nimeomba kuchangia nitazitilia nguvu. Nathubutu kusema kwamba pamoja na juhudi za Mhe. Rais kutaka kuondosha hilo tatizo la michango kwa akinamama lakini bado suala hilo lipo. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri suala hilo alifuatilie na liweze kuondoka na wale akinamama wetu wanyonge ambao wanakuja pale kutibiwa waweze kupata huduma hizo bure.

Mhe. Mwenyekiti, halafu jambo jengine ni kwamba limeshazungumzwa lakini na mimi nitalitilia mkazo, changamoto nyengine ambayo inatukabili katika hospitali zetu ni lugha chafu kwa baadhi ya watendaji wa hospiteli zote nathubutu kusema. Hali imekuwa mbaya mno. Nathubutu kusema kwamba inaonesha kama kwamba katika Vyuo vya Afya kuna *section* maalum ya kufundishwa wafanyakazi kusema maneno machafu kwa wagonjwa, nathubutu kusema hivyo kwa sababu hali kila siku inazidi. Hili tatizo tunalisemea sana lakini bado tatizo lipo. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri afanye juhudi za makusudi kulivalia njuga hasa tatizo hili liweze kupungua, kwa sababu mwananchi yeyote anapokwenda pale na tatizo anakuwa na shida, hatoki tu mtu akenda kutembea pale, anapokwenda pale anakuwa na tatizo lakini baada ya kupungua tatizo akifika pale anazidishwa tatizo mara mbili zaidi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala hili Mhe. Waziri aliekee mikakati.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika kipengele cha 35 ambacho kinaeleza hali ya uzazi. Katika hotuba yako Mhe. Waziri haioneshi watoto wafu na waliokufa baada ya uzazi. Ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika kitabu chako kwenye kiambatisho namba 4 umeeleza hapa taarifa ya hali ya uzazi katika hospitali na vituo vya afya vya Serikali kuanzia Julai, 2016 hadi March, 2017. Mhe. Mwenyekiti, ameeleza wazazi waliojifungua kawaida na upasuaji watoto walio hai, wanawake na wanaume na wazazi waliofariki, lakini hukueleza watoto nao wangapi wamefariki. Halafu pia hukueleza kwamba waliozaliwa wamefariki na waliozaliwa baada ya kufariki kipengele hicho hapa hakimo. Naomba Mhe. Waziri utakapokuja uje na taarifa hii ya hali ambayo niliyokueleza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapo hapo katika kipengele cha mwisho hapo umesema kamba wazazi waliofariki ni 27. Katika hotuba hiyo ulisema tatizo hili bado lipo lakini naomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majibu uje na taarifa rasmi labda tafiti gani mmefanya ili kuona kwamba hili tatizo bado linaongezeka. Mimi nafikiria tatizo moja si mtafiti lakini kuna tatizo mimi nahisi linachangia hili. Kule mwanzo nilisema kwamba hali ya majibu ya watendaji wako ni mbaya, mgonjwa anakuja hospitali ana matatizo

anaumwa, mjamzito anakuja pale ana matatizo anaumwa, anafika pale hapati kauli nzuri. Nafikiria inawezekana mmoja kati ya suala linalochangia vifo vya akinamama ni hilo, kwa sababu mtu anayekuja na matatizo, anafika pale anazidishwa tatizo, pengine wengine wana *pressure*, anafika pale *pressure* inapanda anafariki. Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba ukija uje na tafiti nzuri kuhusu hili.(*Makofi*).

Halafu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa pia amesema kipengele cha waliojifungua kwa upasuaji inaonekana idadi ni kubwa mno, wazazi wanaojifungua kwa upasuaji ni 1382. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri unazungumza na Mhe. Abdalla Maulid Diwani hunisikii, naomba pia ukija unipe sababu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Salma Mussa Bilali zungumza na kiti. Mhe. Waziri anakusikia lakini na mimi kwenye kiti pia nakusikia. Kwa hivyo nilikuwa naomba mweelekeo wako sana ueelekee kwenye kiti.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atakapokuja unieleze ni sababu zipi zinazosababisha wazazi wengi au idadi ya wazazi wanaozaa kwa upasuaji inaongezeka siku hadi siku, kila ukisikia fulani kazaa kapasuliwa tatizo siku nyengine linakuwa sio la upasuaji lakini anapasuliwa naomba uje na majibu mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba niende kwenye "Program ya Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala, program H0103 ukurasa wa 57". Mhe. Mwenyekiti, program hii ina lengo au ina malengo ya kukamilisha matayarisho ya mfuko wa bima ya afya na uanzishwaji wake. Suala hili limekuwa ni la siku nyingi mno, kila bajeti inayokuja suala hili limo lakini utekelezaji wake mpaka sasa hivi bado hatujajua umefikia wapi. Naomba sana suala hili ni zuri Serikali imeamua jambo zuri lakini mpaka sasa bado hatujajua ufumbuzi wake uko vipi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwanza nataka nijue ni maandalizi gani yamefikia, halafu ni hatua gani Wizara imefanya mpaka sasa hivi. Halafu nataka kujua ni hospitali gani mnatarajia kuzitumia kwa ajili ya huduma hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa kuna Wajumbe wamechangia kwamba kuna Wajumbe wana Bima lakini wanapokwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja wanakosa huduma, au wanaambiwa huduma hii haimo kwenye bima wanapata shida. Kuna Wajumbe hawa wamewakatia bima wazee wao vijijini katika *list* ya upatikanaji wa huduma hiyo Hospitali ya Mnazi Mmoja imo, Makunduchi imo lakini leo mwanamama anakwenda Hospitali ya Abdalla Mzee au Hospitali

ya Makunduchi hapati hiyo huduma kule anaambiwa huduma hiyo haipatikani. Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba tujue ni vituo gani ambavyo mmevipanga kwa ajili ya kutoa huduma hizo na mmejipangaje ili kuona kwamba hiyo huduma inakwenda kama ilivyopangwa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika hii huduma ya bima, mipango hii ipo siku nyingi sana. Kwa hivyo mimi nasisitiza kwamba Mhe. Waziri hili suala hebu lichukulie juhudi ya makusudi ili liweze kufanikiwa. Sisi Wajumbe wote hapa tulikuwa tunasubiri bima ya afya ya Zanzibar, lakini tumesubiri miaka mitano imepita na tumeingia miaka mitano hii bado hilo suala halikuwa tayari, tumekwenda kujiunga na bima nyengine za Tanzania Bara ina maana tunakosesha mapato katika Serikali yetu. Kwa hivyo Mhe. Waziri naomba sana hili suala lichukuliwe umuhimu wa aina yake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika "Program ya Tiba, PH0102 Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospitali za Vijijini kuwa za Wilaya na za Wilaya kuwa za Mkoa". Mhe. Mwenyekiti, Wizara ama Serikali katika program hii ilikuwa ina lengo zuri sana lakini hadi leo tunaona bado imekuwa hadithi ya vitabuni tu, tumeona mfano hospitali moja nadhani kwa usimamizi wake mwenyewe Mhe. Rais ni Hospitali ya Abdalla Mzee imetoka katika Hospitali ya Wilaya imekwenda ya Mkoa. Lakini kuna Hospitali ya Micheweni, kuna Hospitali ya Wete, kuna Hospitali ya Chake Chake bado hatujaona maendeleo yake yakoje.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nathubutu kusema kwamba Pemba angalau kuna hospitali za Wilaya, lakini hapa Zanzibar mpaka leo hospitali za vijiji bado hazijawa hospitali za Wilaya na wala hatuna hospitali ya Mkoa. Hili suala la upandishaji wa daraja, hili lilikuwa linakwenda sambamba na ujenzi wa Hospitali ya Binguni, lakini mpaka leo hatujui chochote kinachoendelea kuhusu hospitali ya Binguni. Mimi nina uchungu sana na hospitali ile kwa sababu mimi ni mmoja katika walioshiriki upatikanaji, upimaji na upatikanaji wa hati wa eneo lile, lakini naona mpaka leo bado hatua hazijachukuliwa, naona uchungu kwa sababu wanawake wa Mkoa wa Kusini wanapata tabu wengine wanazaa njiani, lakini itakaposogea huduma pale watafarijika na wao. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atakapokuja aniambie matayarisho gani yaliyofikiwa mpaka sasa hivi na nini hasa kikwazo cha kwamba mpaka leo ujenzi wa hospitali ile bado haujaanzishwa.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo nataka kumkumbusha Mhe. Waziri kwamba sioni raha anaongea na watu wengine sana hanisikii, sioni raha…

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwaombe sana tutumie hii Kanuni yetu ya 61 mazungumzao yamekuwa mengi hata mchangiaji anaposimama akachangia kwako Mhe. Waziri anahisi kama unampuuza huwi makini nae...

Mhe. Salma Mussa Bilali: Anadharau.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo nilikuwa naomba hii hoja ya Serikali ndio ipo mbele yetu hapa tunaijadili. Kwa hivyo kama Serikali na Waheshimiwa wote Wajumbe tunaotoa hizi hoja basi nawaomba sana tuwe makini, tusikilize ili yule mchangiaji Mhe. Waziri ajisikie raha maana mpaka anasema haoni raha kama humsikilizi.*(Makofi).*

Tuendelee Mhe. Mjumbe.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea nataka nimkumbushe Mhe. Waziri kwamba katika suala hili la upandishaji wa hadhi vituo katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 117 kipengele cha 102(c) kimeeleza hilo suala. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba uweke kipaumbele kutekeleza hii ilani ni siku nyingi suala hilo lipo lakini bado utekelezaji wake hatujauwona.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika suala la *cholera*.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa kwa sababu dakika zako zimeshakwenda.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Mwenyekiti nimekusikia namalizia mbio mbio.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri namuomba kwamba kila mwaka nadhani tumeona tatizo la maradhi haya ya *cholera* yanavyokuja, kumekuwa na vifo vingi, kumekuwa na matatizo mengi kila baada ya muda. Kwa hivyo naomba Wizara kulikuwa na tatizo la malaria limeundiwa mradi limeondoka, kumekuwa na tatizo la *UKIMWI* limeundiwa mradi limeondoka. Naomba Mhe. Waziri na hili tatizo la kipindupindu hebu liundiwe mradi, kwa sababu ni maradhi hatari na yanaua haraka haraka kushinda hata huo *UKIMWI*. Kwa hivyo naomba maradhi ya kipindupindu nayo yatafutiwe muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo na mimi nilitilie mkazo hili suala la *waiting shade* wananchi wanahangaika sana wanapokaa kusubiria wagonjwa wao,

wanapata tabu mvua hizi wanaroa wanahangaika. Kwa hivyo naomba na hili suala pia nalo alipe kipaumbele.

Halafu jengine la mwisho Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilizungumzia suala la *physiotherapy* nilitilie nguvu kwa sababu nataka tukumbuke kwamba sisi sote ni walemavu watarajiwa. Suala hili Mhe. Waziri bajeti zote za nyuma linatiliwa fedha haziingizwi, mara hii halikutajwa kabisa, ina maana hii inaonekana kamba kuna dharau fulani hapa imepita. Haiwezekani suala hili lisitiliwe fedha kwa sababu kuna mambo muhimu pale, sio tu watu wenye ulemavu, wengine wana ulemavu wa kuzaliwa wangine wanapata baadae kinasaidia kile kitengo. Kwa hivyo na mimi namuunga mkono Mhe. Mwantatu kusema kwamba hichi kitengo kiingiziwe fedha ikiwezekana Mhe. Waziri Kamati ya Bajeti Wizara ya Fedha itafute imegue huko popote lakini hichi kitengo kipatiwe fedha za kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri na mimi na wewe tuna uwezo wa kutoka hapa tukenda tukajitibu kwengine, kuna wananchi wanyonge wanatoka huko wanategemea hospitali yao ile. Kwa hivyo waende wapi, kitengo hakiingiziwi pesa, watendaji wanatakiwa wafuatilie, hamna pesa watapataje….

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Salma muda wako umekwisha.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Naunga mkono Mhe. Mwenyekiti. Baada ya kusema hayo mengine yaliyobakia nitayapeleka kwa maandishi, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono kwa asilimia tisini tu mpaka Mhe. Waziri atakaponijibu hoja zangu na hasa kipengele kile cha *physiotherapy* umegue popote lakini kile kipate pesa.

Mhe. Mwenyekiti ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Salma Mussa Bilali kwa mchango wako nina imani Mhe. Waziri amekusikia.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea kuwaita wachangiaji wanaofuata, kuna tangazo kidogo ambalo linahusu wageni wetu wa leo nao ni wageni wa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy wa Jimbo la Chaani. Wageni hao ni wawekezaji katika shughuli za utalii kutoka Turkey naomba tuwatambue.

1. Mgeni Alp Aksu
2. Thaylan Basarir
3 Baris Comurcu Oglu

Karibuni sana.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea tumebakiwa na saa moja ambayo tutakuwepo hapa lakini wachangiaji bado wengi, kuna wachangiaji nitawapa nafasi ambao wameomba dakika chache. Kwa hivyo wale ambao nitakuwa sikuwataja naomba wapeleke michango yao kwa maandishi.

Naanza na Mhe. Suleiman Makame Ali kwa dakika kumi ameniomba, atafuatiwa na Mhe. Khadija Omar Kibano dakika tano, Mhe. Masoud Abrahman Masoud, Mhe. Hamza Hassan Juma dakika kumi kumi kama muda utakuwepo.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Afya. Kwanza kabla ya kuchangia nitoe pongezi zangu niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa jitihada nzuri anazozichukua ili kuhakikisha suala la afya limefanikiwa Zanzibar. Kwa hivyo na mimi nimewaomba watendaji wote wa wizara musimuangushe Mhe. Rais, washirikiane wawe kitu kimoja ili kuhakikisha kwamba afya Zanzibar inaendelea na inapatikana kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya mchango wangu niende kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasema hapa katika ukurasa wa 168, "Kwa kutambua umuhimu wa afya kwa wananchi CCM inaendelea kusimamia utekelezaji wa lengo la kufikisha huduma za afya karibu na wananchi wote mijini na vijini, huduma za afya zinapatikana katika kila sehemu isiyozidi kilomita tano".

Mhe. Mwenyekiti, hilo ninalikubali na pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa sababu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kasema hapa kwamba, "Hoi hoi ni kilindo" ni kweli, tulikuwa tunapiga kelele siku nyingi kuhusu Kituo cha Afya cha Ndagoni kilichojengwa na wananchi wenyewe na ufadhili wa msamaria mwema na kwa kukifungua Mhe. Waziri ninakupongeza sana. Wananchi wa Ndagoni wanaondokana na usumbufu ule. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri alikwenda katika ufunguzi wa kituo kile ulishuhudia mwenyewe pale kwamba hakuna nyumba ya daktari pale.

Lakini vile vile katika Kituo cha Afya cha Ndagoni daktari aliyeopo ni mmoja na tena hatoki pale, anatoka Vitongoji. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri alihakikishe hili kwamba suala la daktari pale alifikirie ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma kwa wakati wowote. Kwa sababu daktari

ikiwa hayupo pale yupo Vitongoji ndipo anapokaa, wananchi itakuwa ndiyo yale yale na itakuwa hatujafanya kitu, itakuwa tumefunika tandu ukafunika nge. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri ahakikishe kwenye suala hili kwamba kile kituo cha afya cha Ndagoni wamepata madaktari wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala la malaria kwenye ukurasa wa 11. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara ya Afya kwa sekta hii ya malaria, kuhakikisha kwamba malaria Zanzibar inatokomezwa kabisa. Kusema la ukweli asilimia kubwa yamepungua kwa sababu miaka mingi ilikuwa tunazungumzia kuhusu suala la malaria, lakini sasa hivi malaria nadhani haizungumzwi sana, tunazungumza masuala mengine. Kwa hivyo nizidi kuomba wananchi wa Pemba hususan wa jimbo langu pamoja na Zanzibar kwa ujumla kuhakikisha kwamba wanatoa ushirikiano wanapokwenda wapigaji dawa na wanapopewa vile vyandarua wasivijengee michicha na vitu vyengine na kuvivulia ngogo kama kule kwetu Ndagoni, basi waweze kujifunikia ili kujikinga na hayo maradhi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika ukurasa wa 69, hapa anasema kwamba "Programu ya Huduma na Tiba". Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kulitia suala la *DNA* akaona kuwa ni muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninakubali kwa sababu suala la *DNA* Zanzibar imekuwa ni kikwazo. Kila siku tunalipigia kelele suala hili juu ya upatikanaji wa *DNA*. Kwa hivyo mara hii Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akaona umuhimu wa kuliweka, nadhani ni kipa umbele cha mara hii kwenye bajeti hii. Hivyo namuomba Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba hili nalo limepatikana kwa hali yoyote ile.(*Makofi*).

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 91. Kwenye kitabu hichi kinasema kwamba, "Orodha ya vituo vitakavyojengwa na vitakavyofanyiwa ukarabati kupitia mradi wa ORO". Mhe. Mwenyekiti, Naibu Waziri ni shahidi katika Jimbo langu la Ziwani kuna kituo cha afya cha Birikau kimejengwa ndani ya miaka kumi na mbili tena kituo kile, na Mhe. Naibu Waziri ni shahidi tulikwenda shirika. Wananchi wale wa Birikau wanateseka, ili kukamilisha ile Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba kilomita tano basi naomba kituo kile cha afya cha Birikau kwa hatua kilivyofikia, basi Mhe. Waziri nacho ingekuwa vyema angekiorodhesha humu. Kwa sababu wale wananchi wanateseka, wanapata tabu wanafuata huduma mbali. Mhe. Mwenyekiti, hivyo namuomba Mhe. Waziri alichukue hilo na alifanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Kitengo cha Ukimwi. Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Ukimwi kinaendeshwa kama kienyejienyeji, kama kirafiki-rafiki hivi. Kuna mafunzo pale ya semina hutokezea lakini yule anayekwenda leo na kesho ndiyo anayekwenda yule yule na keshokutwa yule yule. Yale ni mafunzo na lengo la mafunzo ni kupata taaluma. Sasa kumchukua mtu huyo huyo kila siku ukimpeleka, itakuwa kuna jambo hapa kwenye Kitengo cha Ukimwi. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri aweze kulisimamia hili na kuhakikisha kwamba linaondoka.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye masuala ya madawa katika vituo vya afya. Kuna siku moja nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri hapa kuhusu upatikanaji wa madawa kwenye vituo vya afya ndani ya Jimbo la Ziwani. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri akanijibu kwamba vituo vya afya vyote ndani ya jimbo langu vimepatiwa madawa ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza kikao nilikwenda Pemba ili kuhakikisha kwamba hizo dawa zilizopelekwa kwenye vile vituo vya afya vya Jimbo la Ziwani ni dawa gani. Nilipokwenda kule nilikuta *panadol* kopo moja moja kwa kila kituo. Kwa hivyo naomba kwa Mhe. Mwenyekiti, kwamba wanapotujibu majibu yao basi yawe na uhakika, kwa sababu sisi tunafuatilia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, pia vile vile Mhe. Naibu Waziri akaniambia kwamba ni tatizo la wenye dhamana hawakwenda kuchukua zile dawa wakati dawa zilikuwepo. Sasa mimi ninataka nijue hapa kuna utaratibu gani kwamba yeye mwenye dhamana ya kituo anapeleka maelezo kuwa mimi dawa zimenimalizikia kwenye kituo changu. Lakini sasa huku unaambiwa kwamba dawa mwenye dhamana ya kituo haendi kuchukua. Hapa itakuwa sifahamu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nikitaka majibu hapa Mhe. Waziri aje anipatie majibu kwenye kituo kile cha Birikau ambacho kimeshafikia hatua nzuri. Lakini vile vile kwenye kituo cha Ndagoni upatikanaji wa madaktari pamoja na nyumba ya daktari pale.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kutoa majumuisho yake anijibu ili niweze kupitisha bajeti hii bila ya tatizo lolote. La kama si hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninazuia shilingi mpaka Mhe. Waziri anipatie majibu ya masuala yangu niliyomuuliza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kukaa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame Ali. Sasa naomba nimwite Mhe. Khadija Omar Kibano. Mhe. Masoud Abrahman Masoud dakika

tano. Mhe. Hamza Hassan Juma dakika kumi ajitayarishe na Mhe. Rashid Makame Shamsi kama muda utaruhusu na yeye dakika tano pamoja na Mhe. Machano Othman Said dakika tano alizoomba. Mhe. Masoud tuendelee kwa sababu Mhe. Khadija hayupo ndiyo kwanza anaingia hivi sasa.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa kwenye kikao hichi adhimu. Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote kwa ujumla katika Wizara hii ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende moja kwa moja kwenye suala hili ambalo hivi sasa lipo katika mji wetu wa Zanzibar la kipindupindu. Mhe. Mwenyekiti, suala hili kila mwaka linajitokeza. Niombe sana Serikali inapokusudia kufanya lake inafanya na mimi ninaishi Bumbwisudi. Serikali ikiaamua kuwasaka wapika pombe huwa inatoa gari aina ya *defender* inakwenda maeneo yote inayopikwa pombe na watu wanakamatwa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, niombe sana wanaosababisha kupatikana kwa kupindupindu ni pamoja na wale wananchi waliokuwa hawapendi kuchimba vyoo, wanajisaidia maporini. Niombe Serikali kwa kupitia vikosi vyake vya SMZ na zile Kamati za Afya za Shehia zipite kwenye haya maeneo ambayo kila baada ya masika zinapata kipindupindu, waangaliwe wananchi waliokuwa hawachimbi vyoo ili watupunguzie hili janga kila mwaka kutokea.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo wenzangu wamelizungumza sana suala la mabanda ya kukaa kusubiri kuingia kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Wiki mmoja iliyopita niliona tabu sana, wananchi wanazuiwa nje wasiingie ndani na mvua zinanyesha watu wanaroa. Tumuombe sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri na wenzangu wamelizungumza sana tujengewe banda pale angalau wananchi wapate kujisaidia.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri mimi ni mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na wewe uliokuwepo kwenye kiti hicho. Tulipata nafasi za kutembelea kwa wenzetu Tanzania Bara. Mhe. Mwenyekiti, tumejiona jinsi ya wafanyakazi ya Wizara ya Afya au madaktari pamoja na manesi na wale wananchi waliopangwa kusafishwa katika hospitali zao. Hospitali ni nzuri zinapendeza, kila unapopita unaona wapo wasafishaji wasubiri kila baada ya saa moja au masaa mawili wanasafisha kwenye majengo yale.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri hospitali yetu kila aliyesimama hapa anaisema kwa uchafu. Sisi kama wana Kamati tunaona aibu. Nimuombe sana Mhe. Waziri suala hili la usafi katika hospitali zetu za Zanzibar lipewe kipewe kipa umbele kwenye wizara yake. Kwa sababu imekuwa aibu na sisi Waislamu suala la usafi ni jukumu letu. Nimuombe sana Mhe. Waziri ajitahidi kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine ambalo nilikusudia niliseme ni kumpongeza Mhe. Waziri na Mkurugenzi wa Bodi ya Chakula pamoja na Vipodozi, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Kipindi cha nyuma chote tulikuwa tukiona nyama zilikuwa zikipakiwa kwenye mabeiskeli, mavespa na magari zinang'ogwa na maizi. Lakini sasa hivi kwa bahati nzuri hali ipo vizuri, huioni ovyo ovyo mpaka uende dukani. Sasa Mhe. Mwenyekiti, waongeze juhudi ili tuhakikishe hilo tunaweza kufanikiwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya Afya kwa upatikanaji wa dawa. Sasa hivi upatikanaji wa dawa umekuwa mzuri. Lakini bado niseme tatizo lipo ukenda kwenye vituo vya afya unaambiwa dawa hakuna. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri pale ambapo zitakuwa zimepelekwa dawa, aunde Kamati Maalum ya kushughulikia au ufuatiliaji wa zile dawa zikifika huko hospitali wananchi wanyonge, maneno ya Shekhe Hassan Khamis Hafidh wakwezi na wakulima wanazipata hizo dawa. Kwa sababu kuna hali iliyokuwa siyo nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende moja kwa moja kwenye hawa madaktari ambao wamepelekwa kusomea. Madaktari ambao walioteuliwa Zanzibar kwenda kusoma, wanaporudi kuna tatizo ambalo linajitokeza, wanakaa muda mrefu bila ya kuajiriwa. Mhe. Mwenyekiti, wakikaa bila ya kuajiriwa wenzetu Tanzania Bara wakienda tu kwenye Halmashauri wanachukuliwa. Kwa hivyo huku kunabakia, muda ambao tumejipangia kuwaajiri wao tayari wameshaajiriwa Tanzania Bara. Hilo baadae linatu-*cost*, maana yake hata Waziri wa Elimu anapokusanya ile mikopo kwa watu ambao kawapa mikopo inashindikana. Kwa sababu inakuwa tayari wameshaajiriwa Tanzania Bara kwenye Mikoa mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nimuombe Mhe. Waziri na tena nimuombe sana katika kitabu chake cha mwaka jana cha 2016/2017, aliizungumzia Hospitali ya Mbuzini ambayo ni ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ahadi hii kwa kweli inasikitisha kidogo kwa sababu Rais wa nchi, yeye ndiye aliyekuteuwa wewe pamoja na Makatibu wako na Wakurugenzi. Lakini na sisi tumeteuliwa na wananchi waliotuchagua

na alitoa ahadi mbele yao kuwa hospitali ile itahakikishwa inafanywa kuwa ni Hospitali ya Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la kusikitisha sasa hivi hata kwenye kitabu haikuonekana. Nimuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja, naamini sasa hivi Mhe. Rais analiangalia Baraza hili Tukufu, yeye mwenyewe hajisikii vizuri, kuona amri yake mpaka leo haijatekelezwa. Nikuombe sana Mhe. Waziri utakapokuja angalau uniambie. Kipindi kilichopita uliniambia kwamba *Milele Foundation* wakitoka Pemba wanajenga hospitali nne, watakuja kujenga Hospitali ya Mbuzini. Lakini mara hii kwenye kitabu haionekani, wala haionekani popote. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa angalau uumpe yeye mwenyewe mwelekeo kuona ahadi yake inatekelezwa. Lakini na sisi wananchi tujue ahadi ya Hospitali ya Mbuzini inatekelezwa vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo mwaka jana kulikuwa na sakata la leseni ndogo kwa Hospitali ya *Global* pamoja na ya Hospitali ya Al-Rahma, shilingi mbili na laki moja na nusu leseni yake, kakwambia mwaka huu uhakikishe angalau leseni zao zinapanda juu kwa sababu kiduka kidogo chenye thamani ya milioni moja kinatolewa leseni ya shilingi laki mbili. Je, mradi ule mkubwa ambao ni wa kitaifa, lakini leseni yake inaonekana ni ndogo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja basi aniambie kuwa mara hii angalau leseni zao zimekuwa kua kua kidogo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo limezungumzwa na wenzangu sana kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja na huduma za kupima zile, kama *CT Scan* na mambo mengine. Niombe sana kama Hospitali ya Mnazi Mmoja uwezekano wa daktari kupatikana muda wowote haupo, hii huduma ipelekwe katika hospitali za kijeshi. Hospitali za KMKM-Kibweni na Bububu jeshini. Pale wakati wowote ule ukenda unapata huduma ili wananchi wetu wasipate usumbufu wa kumsubiri daktari mpaka saa tatu au saa nne amke ndiyo waje wapate huduma.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa dakika tano nimezitumia vizuri. Naunga mkono hoja ya Kamati yangu ya Ustawi wa Jamii kwa asilimia tisini, hizi tano (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Masoud. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi dakika kumi na atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Miraji Khamis Mussa utamalizia kama muda utaruhusu.

Lakini naomba Waheshimiwa ambao sijawataja wachangie kwa maandishi, lakini pia wale waliomba hizo dakika kumi, ziwe kumi kweli kweli au tano iwe tano maana isiwe unaomba dakika kumi kumbe unataka kuzungumza dakika ishirini. Kwa hivyo nawaomba sana muende hapo hapo ili tumalizie.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii nzuri sana ya Makaridio na Matumizi ya Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote hususan Naibu Waziri kwa utendaji wao, lakini vile vile niipongeze sana Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa ile hotuba yao nzuri, niwaunge mkono Wajumbe wote ambao wametangulia au wamenitangulia katika uchangiaji wa hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze sana Wizara ya Afya wana majukumu mazito wenzetu, wana majukumu wenzetu. Wizara ambayo ni ngumu sana, tunaitegemea lakini ina changamoto nyingi sana lakini wenzetu wanajitahidi sana kuchukua juhudi za kuweza kuona kwamba wanaimarisha huduma za afya katika visiwa vyetu na hususan nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi anazochukua katika kuifanya wizara hii kuweza kutoa huduma nzuri kwa wananchi wake.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nimsaidie tu Mhe. Waziri kwamba yeye ameweza kuainisha changamoto mbali mbali na kweli Wizara ya Afya ni moja kati ya wizara yenye changamoto nyingi. Lakini changamoto hizi zimegawika katika makundi mawili. Kuna changamoto ambazo zipo nje ya uwezo wa Wizara ya Afya na hususan mwenyewe Mhe. Waziri. Lakini kuna changamoto zilizomo ndani ya uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamezichanganua sana. Mhe. Mwenyekiti, nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba miongoni mwa changamoto ambazo zimo ndani ya uwezo wake kama wizara ni suala zima la maadili ya wafanyakazi. Hili naomba sana alitazame. Lakini kuna usimamizi mzuri ambao unakosekana, vile vile kuna tatizo la baadhi ya wafanyakazi kutowajibika vizuri kwenye nafasi zao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yanahitaji maneno tu na usimamizi. Kwa mfano suala kama la kubadilisha mashuka kwa wakati, hili halitaki fedha kwa sababu mashuka yapo na hususan katika jengo jipya. Lakini unaweza ukenda shuka mmoja linakaa wiki nzima halijabadilishwa. Sasa hili ni suala la

usimamizi, hayataki pesa. Lakini vile vile kuna nyumba za madaktari ambazo zimejengwa katika sehemu mbali mbali, huko vijijini lakini madaktari hawakai, wanakaa mijini. Kwa hivyo wanachelewa kufika kazini lakini vile vile wanaondoka mapema kazini kuja mjini. Hili ninafikiri halihitaji fedha kwa sababu Serikali imejitahidi kujenga nyumba hizi ili kuweza kuwarahisishia madaktari hawa wabaki katika sehemu zao za kazi kwa muda mrefu. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba awe mkali kidogo katika baadhi ya maeneo, kwa sababu haya mengine hayataki fedha, yanahitaji usimamizi na maelekezo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika jambo dogo sana katika Jimbo langu la Magomeni. Mhe. Mwenyekiti, pana Kituo cha Sebleni. Kituo hichi cha Sebleni kinawasaidia wakaazi wa Amani, Magomeni na maeneo ya jirani. Bahati nzuri kituo hichi cha afya kimo ndani ya eneo la makaazi ya wazee wetu pale Sebleni. Kina mlango ambao upo katika sehemu za viwanja huku.

Mhe. Mwenyekiti, ule mlango huwa umefungwa muda mwingi haufunguliwi. Kwa hivyo unawafanya baadhi ya wakaazi ya maeneo ya Sebleni na Magomeni au Nyerere hususan kupata tabu ya kuweza kuzunguruka mpaka mbele kule, wakati eneo lile lina mageti mawili. Mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, nishawahi kumwambia lakini ninasisitiza kwamba wananchi wetu wanapata tabu na hususan wale wajawazito wanaotaka kwenda mule kwa huduma. Hivyo afanye utafiti wa kukaa na Ustawi wa Jamii pale ili kuona kwamba geti lile linafunguliwa, ili wananchi wetu waweze kufika pale kwa urahisi na kuweza kupata huduma bila ya matatizo yoyote.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la ugatuzi. Wizara ya Afya ni moja katika ya wizara tatu ambazo zitakuwa zipo katika programu ya ugatuzi kuanzia Julai mwaka huu. Nimuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja aweze kutueleza kwa Wizara ya Afya ni majukumu yepi ambayo yatachukuliwa na Wizara yenyewe na majukumu yepi yatakuwa yanabebwa na Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa, ili sisi Wajumbe tuwe na uwelewa lakini vile vile na wananchi wetu wawe wanafahamu kwamba kuna huduma ambazo sasa zitakuwa zinasimamiwa na Tawala za Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wengi wameshazungumzia mengi nije katika suala zima la udhibiti wa kemikali, dawa, vifaa tiba, chakula na vipodozi kwenye ukurasa wa 35. Hivi karibuni wenzetu wa Tanzania Bara walizunguzia juu ya Kemikali Bashirifu kwa Kiingereza mimi siifahamu. Lakini Kemikali Bashirifu ni kemikali ambayo watafiti wanasema kwamba hivi sasa ni kemikali ambayo inatumika katika kutengenezea madawa ya kulevya ikiwemo *heroin* na

cocaine. Hivi jana kumetokea taarifa kwamba kuna kontena nzima ambayo ina Kemikali Bashirifu na kuna Kampuni ya *TECNO* ambayo hii inashutumiwa kwamba ndiyo inayoleta Kemikali Bashirifu kwa njia za udanganyifu na ina mahala Arusha, Bagamoyo na Dar-es-Salaam.

Sasa niiombe sana Wizara ya Afya kupitia kitengo hiki kuwa makini na kemikali hizi, kwa sababu unapozuia upande mmoja madawa ya kulevya wenzetu wanatumia upande mwengine. Kwa hivyo wanaleta kemikali kwa kutumia ngusha ya vitambulisho vyao na zinaweza zikaingia nchini na hatimaye madawa haya ya kulevya ya *cocaine* na *heroin* yakatengenezwa hapa hapa kwa kemikali hizi. Hivyo niiombe sana serikali kuwa macho na watu hawa ambao wanaleta kemikali hizi ili kuweza kuona kwamba hatupati janga jengine la madaya ya kulevya ambayo yanatengenezwa hapa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nije katika huduma za afya. Katika huduma za afya nimpongeza sana Mhe. Waziri na Wizara kwa huduma za afya ambazo anazitoa katika maskuli yetu. Maskuli 143 yameweza kupata huduma lakini zaidi ni ile huduma ya uchunguzi wa mazingira pamoja na kuwasilisha mada mbali mbali za kiafya. Lakini nipongeze sana kwa Wizara ya Afya kuweza kurusha vipindi mbali mbali kwa njia ya redio kwa njia za televisheni. Mimi ni mfuatiliaji sana wa vipindi hivyo, niwapongeze sana wenzetu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi niiombe sana na niishauri sana Wizara ya Afya ishirikiane na Wizara ya Elimu. Mhe. Mwenyekiti, sio kuweza kuwasilisha mada tu na hizi mada inawezekana zimewasilishwa katika baadhi ya skuli tu, lakini umefika wakati kwamba zile huduma ambazo zilizokuwa zinatolewa zamani, wakati huo tunasoma za kuweza kufanya uchunguzi wa afya za wanafunzi wetu, mimi nafikiri zingerudi. Kwa sababu ili mwanafunzi aweze kujifunza vizuri basi anatakiwa asiwe na vipingamizi vyengine vya afya. Mhe. Mwenyekiti, zamani tulikuwa tunapimwa macho, tunapimwa masikio. Sasa hivi vitu kama itakuwa mwanafunzi ana matatizo ya vitu hivi na kujifunza kwake kunakuwa kudogo. Vile vile mimba za utotoni zilikuwa ni kidogo sana. Kwa hivyo ningeomba sana Wizara ya Afya hili washirikiane na Wizara ya Elimu ili kuona kwamba huduma hizi sinatolewa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa dakika hizo chache na mimi niwaombe wenzangu Wizara hii ni ngumu sana. Wenzetu hawa tuwapitishie bajeti yao ili tuwapime wataweza sasa kujirekebisha vipi katika zile kasoro ambazo tumezisema.

Ahsante sana kwa kunisikiliza.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Rashid Shamsi. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma dakika 10 na Mhe. Miraji Khamis Mussa dakika 10.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia machache sana katika Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mimi nataka nianze kusema moja kwa moja kwamba katika bajeti hii asilimia karibu 80 sina tatizo nayo, lakini asilimia 20 hii kwa kweli Mhe. Waziri itabidi afanye kazi ya ziada aniridhishe ili niweze kukubali kupitisha bajeti hii. Nataka niseme Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake, nakusudia kuzuia fungu PH0102 ambayo katika kitabu hichi ipo ukurasa wa 28 ambayo inazungumzia suala la huduma za tiba. Hilo ni fungu kubwa lakini kifungu kidogo kitakuwa ni HH01020107 "Ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba".

Mhe. Mwenyekiti, pia katika Hospitali ya Mnazi Mmoja nitazuia fungu H02 kupata maelezo ya kina ili niweze kujiridhisha, kwa sababu hospitali hii asilimia 99.9 wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo ndiyo wanayoitegemea kama hospitali yao ya rufaa. Baada ya hayo nataka nianze kwanza kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya hiyo ambayo niliyoiunga mkono kwa asilimia karibu 80.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda wako nataka nianze kutoa maelezo yangu ili Mhe. Waziri ajue nini ninachokusudia kukizuia. Katika suala la Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hospitali ile tulipitisha Sheria hapa na baada ya kuonekana kwamba bado huduma za Hospitali ya Mnazi Mmoja zinasuasua. Mhe. Mwenyekiti, utakuwa shahidi siku ambayo tuliyokuwa tunapitisha Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja nilipiga kelele sana na nikasema hospitali ni lazima katika yale makusanyo ibakishiwe *retention* angalau asilimia 30. Lakini mwanzo nashukuru kidogo serikali ilihisi kama kukubali, lakini baadae sijui kilipita kitu gani wakaja wakakataa hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema vile kwa sababu gani. Nilikuwa nasema vile kwa sababu hospitali ni pahala pa *emergence*, pale hatwendi harusini au shughulini, unapokwenda shughulini dhifa ipo sawa haipo utakwenda zako. Lakini unapokwenda hospitali kile ambacho unachokihitaji kama hakipo, kwa kweli yale maradhi kama umekwenda na maradhi mamoja yanakuwa kumi na moja.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hoja yangu ipo hapa. Hospitali ya Mnazi Mmoja ambayo ni hospitali ya Rufaa. Lakini kama ni Hospitali ya Rufaa kitu ambacho kinachoniudhi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo na naamini na Wazanzibari wote, ni jambo la kwenda pale ukafanyiwa *postmortem* halafu ukaambiwa kipimo hiki nenda kapime Kilimani kinaniudhi kweli kweli.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kitu ambacho nilichokuwa nashangaa nimeangalia katika kitabu cha Mhe. Waziri kifungu cha 86 katika huduma ya upatikanaji wa dawa kuna fedha karibu bilioni 4 aliziomba na katika robo tatu kuna karibu bilioni mbili, milioni mia sita thalathini na sita na nyengine hizo hapo mbele ameweza kupatiwa. Lakini unapokwenda hospitali mara nyingi hivyo hivyo vifaa tiba vyenyewe unaambiwa *gloves* hakuna, kanunue, sijui bendeji kanunue, sijui vipimo nini kanunue, vyote hivyo hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, kuna siku nilitoka nikenda mpaka maabara, kwenda kule vile vifaa vipo vya kufanyia uchunguzi lakini wale watu wa *laboratory* wakaniambia hapa tukiziwasha hizi *AC* hazifanyi kazi. Leo tukienda Hospitali ya Mnazi Mmoja kama kuna *AC* mfano kama 10, basi karibu 7 hazifanyi kazi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hili ni ndiyo suala ambalo linaudhi. Kwa hivyo ina maana kama unakwenda hospitali hakuna vipimo, mimi nafikiri hiyo kusema hospitali ni ya rufaa bado haijawa sawa sawa. Halafu hichi ni kitu cha aibu kwa nini *private hospital* na hivi vihospitali vidogo wala havina kodi ya wananchi, leo ukenda pale vipimo vyote vinapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kutumia Kanuni ya 111 lakini nikaambiwa tayari kuna Mhe. Mjumbe Kanuni hiyo amekwisha kuijengea hoja na mimi kwa kweli naiunga mkono. Hoja yangu ipo hapa. Mhe. Mwenyekiti, ukiuliza serikalini kwenye hii Wizara ya Fedha, kwa sababu sisi tunapokwenda pale tukaona kuna matatizo, tunauliza tuna-*cross check* mpaka Wizara ya Fedha, wanasema wanachokitaka ndicho tunachowapa. Mhe. Mwenyekiti, lakini kama kinachotakiwa yaani fedha zinazopatikana, kwa nini pale vifaa vinakuwa pungufu, kama *reagent* hakuna.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hapa lazima twende tukafanye utafiti tujiridhishe hizi fedha kweli zinapelekwa na kama zinapelekwa zinatumika kama vile zinavyokusudiwa. Niliwahi kumuuliza mpaka mpaka huyu mtu ambaye anapeleka huyu supplier anayepeleka madawa. Kwa bahati nzuri katika utafiti wangu nikampigia simu mpaka yeye, nikamuuliza akasema napeleka kila kitu. Nikawauliza wale watu wa maabara pale, akauliza waulize kuwa

wakasema muulize analeta kila kitu *hundred percent* au analeta kila kitu kwa vile anavyotaka yeye. Mhe. Mwenyekiti, sio kama kusema kwamba mimi nimeleta vifaa, nimeleta madawa na vifaa vyengine pengine mwezi wa 7, lakini ulipeleka kwa asilimia ngapi. Mhe. Mwenyekiti inaonesha hapa kuna fedha zinapelekwa lakini yale mahitaji maalum yanayotakiwa pale hospitali hayapelekwi. Hapa lazima pakafanywe uhakiki ili tujiridhishe ili hospitali yetu ifanye kazi vizuri.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia katika kitabu hichi tulicholetewa na serikali katika changamoto walizonazo ni upungufu wa madaktari bingwa ambao wanahitaji watoe huduma kwa kiwango cha juu, mkusanyiko wa jamaa wagonjwa katika maeneo ya wodini bila ya kazi maalum.

Mhe. Mwenyekiti, wale sio kwamba wanakaa bila ya kazi maalum, mkusanyiko wa wale wahudumu wa wagonjwa, pale tunakwenda kuwahudumia jamaa zetu. Leo kama wagonjwa wetu wanaolazwa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuwaachia madaktari pamoja na ma-*orderly* pale, pale ungekwenda siku ya pili wananuka. Mhe. Mwenyekiti, wale jamaa wanaokwenda pale ndiyo wanasaidia ukiambiwa beba unabeba, peleka huku, unapeleka, peleka chooni wanapeleka. Mhe. Mwenyekiti, wale watendaji wetu kwa kuwabebesha wagonjwa kuwapeleka chooni na kurudi wallahi Mhe. Mwenyekiti, wewe mwenyewe ungekuwa shahidi hapa kama wale jamaa zetu wangekuwa hawendi pale tungekuta wagonjwa wetu wananuka na wengine wangekuwa wameshaoza.

Mhe. Mwenyekiti, hii changamoto tusiseme kwamba hawana kazi maalum. Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliwahi kuleta hoja pajengwe banda pale nje ili wale wananchi wetu wakae pale. Siku hizi kwa bahati nzuri mgonjwa hata akiwa taabani simu anapiga, nataka kwenda chooni anapiga simu, unatoka kwenye banda unakwenda unampeleka unarudi. Madaktri wetu na wao wafanye shughuli nyengine za matibabu lakini haya mambo mengine wananchi wetu wafanye. Huu ni utamaduni kila nchi ina utamaduni wake. Mimi tokea mdogo nakumbuka mama yangu ananichukua tunakwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja nawekwa pale nje, naambiwa wewe usende mtoto mdogo huruhusiwi kuingia hospitali. Mama yangu anakwenda kuangalia wagonjwa halafu tunarudi. Mhe. Mwenyekiti, sasa wale wazee wetu ambao wanakwenda pale hapa katika kitabu imeelezwa kwamba hawana kazi yoyote, kazi wanayo ya kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, ukosefu wa dawa na vifaa tiba, ukosefu wa taarifa sahihi kwa wagonjwa. Sasa kama huna vipimo taarifa sahihi za mgonjwa utazipata vipi, huwezi kuzipata. Haya ndiyo hayo tunayoyasema. Mimi namuomba Mhe.

Waziri inawezekana pengine hili lipo nje ya uwezo wake pesa hana, turejeshe tena Sheria ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, si vibaya sheria hata kama mwaka mmoja haijatimia lakini kama haitekelezeki irejeshwe sheria ile ili tuweze kuipitishia *retention,* yale makusanyo yanayokusanywa Hospitali ya Mnazi Mmoja asilimia 30 yabakie pale kwa ajili ya kutoa huduma zile nyengine ambazo si muhimu, mimi naamini tusingeambiwa kanunue bendeji, *gloves* wala tusingeambiwa kanunuwe dawa gani kule FAHUD au *pharmacy* nyengine mjini.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu hasa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, ni mambo ambayo kwa kweli yanaudhi sana. Nitazuia tena fungu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja fungu PH0201 "Huduma za Uchunguzi wa Matibabu na PH0202 Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja". Kama unavyojua siku hizi Mhe. Mwenyekiti, tukishakaa hapa tena kwenye mafungu mara tunaleta yale ya jumla kwa jumla, kwa hivyo nikikosa huku napiga huku.

Mhe. Mwenyekiti, jengine suala la usafi na ushughulikiaji wa jengo la Hospitli ya Mnazi Mmoja. Nina picha hizi hapa, dari mbovu, njoo umpelee Mhe. Mwenyekiti, bajeti tunapitisha mvua imenyesha, maji tele hospitali ndani. Sasa hii ndiyo Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ya Rufaa. Leo serikali yetu tunamshukuru sana Mhe. Rais katika Wizara inayopendwa, katika wizara inayobebwa ni Wizara ya Afya, serikali imesha-*invest* pesa nyingi, majengo mazuri ya kisasa. Sasa hivi kila mtu ana hamu azae, katoa takwimu Mhe. Waziri, watu wanazaa sana, mimi nawapongeza Wazanzibari, ukila samaki sana lazima utazaa sana.*(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, sasa jengo ni zuri, linapendeza lakini huduma zinaanza kuwa ndogo. Mimi nashauri, unajua hawa wenzetu wakati mwengine tunaweza tukawabebesha majukumu sio yao. Suala la usafi Hospitali ya Mnazi Mmoja itafutwe kampuni kwa ajili ya kufanya usafi tu. Hata sisi Baraza la Wawakilishi ilikuwa tunasafisha wenyewe hapa, wafanyakazi wanakuja kazini mtu taabani kachoka, fagio haliwezi. Baada ya kuajiri kampuni sasa hivi ukipita ukikanyaga hujaondoka msafishaji kasafisha.

Mhe. Mwenyekiti, leo kuna wakati mwengine unakwenda hospitali, ukenda kule chooni basi unaweza ukatapika ukaambiwa una kipindupindu. Kwa sababu ile kazi ilikuwa inatakiwa watu wa aina yake, sio kwamba wengine madaktari mabingwa, madaktari wakashughulikie mambo ya usafi. Mimi nashauri itafutwe kampuni ishughulikie masuala ya usafi. Lakini vile vile atafutwe meneja wa kushughulikia jengo. Leo ukenda ma-*air condition*, mimi

nilikwenda kuna siku nilikwenda kwenye huduma ya meno pale, daktari yule ananitibu kwanza anakwenda anajipepea kwa joto, ma-*AC* mabovu.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli katika eneo la Hospitali ya Mnazi Mmoja nafikiri nimeshatumia dakika zangu 5 kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, dakika zangu zilizobakia wacha nizungumze katika maeneo mengine waliyofanya vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza naomba umalizie, dakika sio tano unakaribia kumalizia, umebakiwa na dakika mbili tu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Aah! Mhe. Mwenyekiti! haya haya nimeshakubali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kama nilivyosema kuipongeza sana Wizara hasa katika suala zima la malaria na hii moto waliyokuja nayo sasa hivi ya kumaliza malaria, mimi kwa kweli niwashukuru sana. Hivi majuzi nilikuwepo Mexico, nilipojitangaza kwamba mimi nimetoka Zanzibar tayari kuna baadhi ya watu pale wakanifuata wakaniuliza kuna mbinu gani ambazo mlizozitumia kwa ajili ya kumaliza malaria. Nikawambia tunatumia *fumigation* katika majumba yetu na humu katika kitabu mumeeleza vizuri, katika zile nyumba ambazo bado wamegundua kuna maeneo kuna malaria wanakwenda wenye *field*. Mimi ninawapongeza sana kitengo hichi cha huduma za malaria, lakini kitu ninachokiomba serikali tusijibweteke. Hii kazi iliyofanyika ni kazi nzuri, ni lazima tuhakikishe kwamba kitengo hiki kinapatiwa fedha ili kuhakikisha kwamba wanatufuata katika maeneo yetu ili kutoa hizi huduma.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa wazo kwa Mhe. Waziri. Humu katika hotuba yako, tena nataka nikwambie katika mwaka ulioandika hotuba nzuri Mhe. Waziri mwaka huu umetuandikia kitabu kizuri kinajieleza, yaani *fantastic* tena umeeleza kila kitu. Changamoto iliyokuwemo kuna watu waliokuwa hawataki kwenda kupigiwa dawa majumbani. Mhe. Mwenyekiti, hawa tuwatangaze ni maadui namba moja wa Wazanzibari na tusikubali haiwezekani mwananchi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ukishazaliwa na mama yako, wewe unakuwa sio mtoto wake tena mtoto wa taifa, hawezi kukufanya chochote kukuondoa duniani unakuwa wewe ni mtoto wa taifa. Sasa na hawa ambao wanaokataa nyumba zao zisipigwe dawa za malaria, hawa ni maadui wala hawafai kuishi katika jamii. Naomba zichukuliwe hatua, nyumba zipigwe dawa kwa nguvu wakitaka wasitake.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana madaktari wa Hospitali yangu ya Jimbo la Kwamtipura wanafanya kazi nzuri. Lakini naomba Mhe. Waziri unaipenda sana hospitali yangu na umeshakwenda sana, ile hospitali kwa kuwa inatoa huduma sana kwa watu ng'ambu, hebu tuifanyeni sasa hivi ikawa inatoa huduma masaa ishirini na nne. Leo ukienda hospitali Mhe. Mwenyekiti, watu wamejaa hivi, madaktari wanaondoka wao wenyewe wanaona tabu wagonjwa tele inabidi waondoke....

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza waziri amekuelewa, muda wako umekwisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kishanielewa haya. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono asilimia thamanini na yale mengine tutakujakuelewana mimi na Waziri sina tatizo ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza kwa mchango wako. Sasa mchangiaji wa mwisho aliyebakia ni Mhe. Miraji Khamis Mussa, naomba utumie dakika kama ulivyoziomba ili tumalizane.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya, mimi siendi kwenye pongezi kwa sababu dakika zangu nilizopewa zenyewe kidogo.

Kwanza naomba niende tuu moja kwa moja kwenye "Programu ya Uchunguzi na Matibabu". Kwenye programu hii maelezo yale ya humu ndani ya kitabu sina tatizo nayo sana, kuna maeneo tu mawili matatu nataka kuyasemea, lakini mwanza naomba nimuulize tu Mhe. Waziri kupitia kauli ya Mhe. Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alitoa tamko karibuni kulingana na kadhia ya uwepo maradhi ya Ebola kwa nchi jirani za ukanda ambao tunapakana nao kama Uganda, Kenya wanaingia na kutoka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukizingatia na sisi kama Tanzania, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano pia tunaingia na kutoka Tanzania Bara. Kwa hivyo ule mwingiliano wa harakati hizi wapo wanaotoka kwetu kwenda kwao na wapo wanaotoka kwao kuja kwetu. Sasa kipindi kirefu kwa sababu tunasafiri safiri siku moja moja hata kwenda Bara au kwenda Pemba kwa kutumia ndege na kutumia bandari tulikuwa tunaona vile vipimo vya kupimia yale maradhi, lakini nasema kwa muda mrefu napita havipo kabisa. Sasa tamko hili ni athari mpaka kwetu na ni tahadhari mpaka kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri pamoja na ulikuwa nje ya nchi lakini suala la kipindupindu lile Kaimu Waziri alilitolea tamko, hatujaona *support* yoyote ya eneo hili na ni eneo moja baya sana katika kutengeneza tahadhari. Sasa sijui Wizara yako kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina utaratibu gani wa kuweza kutoa tamko, lakini kuweza kufanya vile vipimo kama utaratibu wa mwanzo ulivyo. Sasa mimi sitozuia fungu hili lakini ningependa hasa kwa faida ya watu wetu tupate kauli ya Serikali hasa kupitia Baraza hili kwa sababu ndio nishakuhoji itabidi uje ujibu, kwa hivyo tukizuia tu tutakuja kufanya utaratibu wa kuonekana, kama hukujibu maana utujibu wananchi wetu wasiishi kwa wasi wasi sana kunako eneo hili.

Lakini eneo jengine Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi niende kwenye hiyo Hospitali ya Mnazi Mmoja ambao wenzangu wameuzungumza sana. Katika programu ambazo hizi zote zina *support* Huduma za Tiba, Huduma za Vifaa Tiba, vinakwenda kwa asilimia kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, wako wenzangu wamempongeza Rais wa Zanzibar kwa kutilia nguvu pale na mimi naomba ni *support* hiyo, Makamu wa Pili wa Rais juhudi zao zinaonekana sana. Lakini lazima tukubali katika Wizara ambayo inapewa bajeti kwa asilimia kubwa sana ni Wizara ya Afya. Lakini matokeo ya utekelezaji hayaonekani, lazima tukiri mkono wa mtu upo sio bure, sio bure kabisa mkono wa mtu upo haiwezekani vifaa vipo, leo huyu ambiwe kifaa hiki kibovu cha *X-ray* lakini akiende mwengine nusu saa mbele fundi huyu hajaenda yeye anapewa huduma.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuna utaratibu pia hata hao wanaongoza hospitali hii wenyewe, kuna madaktari wanapangiwa zamu wanakwenda kuripoti tu pale, taarifa zipo wakisharudi kuripoti pale anaonekana tu kaingia basi huyo huyo masaa hayo hayo ambayo alitakiwa afanye kazi katika hospitali yetu unamkuta katika hospitali ya *private* pale kaenda kujiweka tu, daktari tunamlipa pesa zetu anakwenda kuripoti na kuondoka utaratibu gani huu, hatuwezi kwenda malalamiko yamekuwa mengi katika eneo hili.(*Makofi*).

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri sisi tunajua jitihada zako, Naibu Waziri tunajua jitihada zako na Katibu Mkuu tunazijua zake, lakini viongozi ambao wamechaguliwa kwa dhamana ya kwenda kushughulikia hospitali hii, ile *commitment* yao ni ndogo kweli. Malalamiko yamekuwa mengi, huduma zimekuwa ndogo. Juzi tu mvua imenyesha kwa masaa manne mpaka matano kadhia ile ya maji mpaka katokea mtu nje ya taasisi kenda kuchangia laki moja akanunua mipira ikenda kuzibuliwa, hii pia haipo ndani ya hospitali yetu ya Mnazi Mmoja, la kusikitisha sana. Kwa hivyo kila siku ikitokezea dharura watokezee wananchi wema wayaone maji kwenye mitandao, baadae yeye

ndiyo akatoe huduma, si utaratibu mzuri. Sasa yule ambaye tulimpa dhamana na mshahara wetu anakula yeye anafanya kazi gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana tukasema inafika pahala mikono ya watu ipo, si watu wote ambao wanaitakia mema hospitali ile, tuwachunguze kwa makini bajeti inakwenda kubwa lakini utaratibu huu wa kushughulikia na kutengeneza huduma hauko vizuri. Mimi ninaomba niungane na wenzangu kwenye jambo hili katika sura ya kuchunguza huduma mimi naunga mkono hoja, lazima tukachunguze, hatuchunguzi pesa, tunachunguza utaratibu wa utekelezaji wa huduma Hospitali ya Mnazi Mmoja. Leo kuna huduma moja imehamishiwa katika eneo la jirani pale, leo kupokea wagonjwa unakwenda katika hospitali mpya. Ni jambo zuri lakini ile miundombinu yule mgonjwa ambaye ameandikiwa kitanda anakuja katika jengo la zamani kutoka katika hiyo hospitali mpya mpaka jengo la zamani kile kitoroli kikibururwa yeye mwenyewe anaumia. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kweli hawa madaktari walisomea kweli na wakapasi au walikopea, maana ile huduma ambayo ya kumchukua yule mgonjwa tu na kufika katika utaratibu wa kawaida anabururwa anaumia miundombinu mibovu, toroli ile anaingizwa mpaka anafika katika wodi anayokwenda tunashangaa mpaka hospitali zetu za *cottage* zimejengewaa eneo zuri la kupitishia wagojwa wetu. Leo Hospitali ya Mnazi Mmoja, hospitali hii tunayosema tunaipeleka ibadilike kutoka utaratibu wa sasa iende katika utaratibu mpya, eneo hilo pia tunashinda kuliboresha.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini haitoshi mgonjwa huyu akishapokelewa akishapewa kicho kigari cha kuonekana wewe nenda katika wodi anaongozwa na yule ambaye kampeleka katoka naye kwake, ndio utaratibu wa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, ndio utaratibu wa hospitali huu unaotakiwa. Mhe. Waziri ukija twambie ndio maana tunataka kuchunguza huduma haiwezekani leo mgonjwa keshaandikiwa wodi ile mimi sijui namna na kumchukua mgonjwa aliyepata ajali, mgonjwa ambaye ana maradhi mengine ya kuambukiza, lakini wale ambao wamesomeshwa na utaratibu wao, wana uwezo wa kumbeba na kumpeleka, unapewa mwenyewe unakokotana naye unakwenda kule, hao tunaowalipa wako wapi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi niseme kwenye jambo hili la hii Hospitali ya Mnazi Mmoja na mimi hapana, naomba niungane na wenzangu wale walikuwa na nia nzuri ya kwenda kuchunguza huduma. Mimi sina tatizo labda la kuelekea kwenye ile *political responsibility* lakini nilikuwa na tatizo la kuelekea kwenye *leadership responsibility*, hao watendaji wote walikuwa

watupishe, tuweke watendaji wengine kwa muda kisha tuone, tunaweza tukenda au tukabaki wapi, haiwezekani naomba kunako eneo hili nichangia zaidi kwa maandishi nisije Mhe. Mwenyekiti, akaniwashia taa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini wenzangu walichangia *first track*, ukienda kule na mimi naomba niungane na wenzangu miundo mbinu mibovu, ile hadhi na ile huduma haipo, hatuelewi maana yake ile dhamira ya wenzetu ikoje, ndio maana nikasema ukichanganya vitu vyote unaweza ukaona ndio ukaenda huko katika *leadership responsibility*. Maana wao wenyewe wafikirie kwa umakini pesa tunawapa lakini kazi hazitendeki, kwa nini hawaachi tu tukisha tukaweka utaratibu mwengine kabla hiyo Kamati ya Mhe. Hassan Khamisi Hafidh kuundwa.(*Makofi*).

Lakini naomba niende katika eneo la mwisho kwa sasa kwa sababu huko kwengine nitapeleka kwa maandishi, kwa sababu nilikuwa na mengi na ndiyo nimepewa dakika chache za kumalizia. Katika eneo la Huduma ya Udhibiti na Kemikali, Dawa na Vifaa Tiba, Chakula na Vipodozi katika taasisi hii ya *ZFBA*. Kwanza niwapongeze sana na nimpongeze sana Mrajis au Mkurugenzi sijui kwa sasa cheo chake ambacho kimebadilika kwa hatua nzuri aliyoifanya, lakini jitihada zile zilipongezwa katika namna ya kubeba nyama, lakini naomba niende maeneo mawili haraka haraka kwa dakika mbili ambazo za kumalizia.

Mhe. Mwenyekiti, machinjio yetu ya Kisakasaka hayako salama. Wenzetu walizungumza sana lakini mimi naammini yule kazungumza labda analetewa picha lakini aende akatizame mazingira nyama ambayo inatoka kule, yale machinjio hayako rafiki. Mimi niunge jitihada zao mkono machinjio ambayo yalifungwa Mkoa wa Kaskazini, naamini wanatashirikiana na Mhe. Haji kupitia Halmashauri wayaboreshe ili huduma ile irudi.

Lakini pia kwenye jambo la mwisho soko letu la Darajani, mimi ni mdau mkubwa wa Baraza la Manispaa lakini ni soko ambalo ukienda katika eneo la kuuzia nyama mazingira yake si mazingira rafiki na kama hili Waziri unabisha, Mawaziri wawili wa Tawala la Mikoa na Waziri wa Afya tufuatane niende nikakununulieni nyama kilo mbili mkisha mkale bure katika eneo lile, hailiki mazingira machafu. Sasa hiyo miongozo tunawapa wengine lakini miongozo ya kuipa ile taasisi ya Serikali haipo. Leo kuna wageni wanakwenda mule wanapiga picha wanarusha katika sehemu mbali mbali, ndio soko la kuwapeleka watu kwenda kupiga picha lile, hebu tutengeneze utaratibu mzuri. Soko lipo pahala pazuri, wanakwenda watalii kila wakati basi mazingira yabadilike na ndio maana nikasema kama hili wanabisha asubuhi mapema tutapanga utaratibu, tukanunue nyama tu katika *butchery* zile lakini waingie

ndani wakaone mazingira kama wao wanaweza wakazila. Sasa wananchi wetu wanakwenda wakala.(*Makofi*).

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba kuonga mkono hoja kwa asilimia sabini, zilibakia nasubiri majibu ili tuone tunakwenda vizuri na Mhe. Waziri. Ahsante sana. (Makofi).

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti, 63.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekuelewa kuhusu utaratibu nakuomba ukae tumalize kwa sababu muda umekwisha lakini nishakuelewa.

Nimekuelewa Mhe. Hassan kuhusu utaratibu nimekuelewa na umesimama, lakini naomba kwa vile nimeshasimama na kwa kuwa naahirisha Baraza. Kwa hivyo kuhusu utaratibu nimekuona lakini tutafanya baadae.

Ahsante sana Mhe. Miraji na Waheshimiwa wote kwa michango yenu. Kabla ya kuahirisha Baraza naomba niwakumbushe kuwa kesho kuna Semina ya Wizara ya Afya. Semina hiyo itafanyika Hoteli ya *Ocean View* Kilimani.

Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue fursa hii kuwapongeza wachangiaji wote pamoja na Waziri lakini namuomba Mhe. Waziri, Jumatatu tukijaaliwa ndio siku yetu ya majumuisho na michangio ya Wajumbe umeisikia na nina imani na watendaji wako mtakaa pamoja mje mlete hapa jawabu sahihi zitakaziwaridhisha Wajumbe ili wapitishe bajeti hii.

Nawashukuru sana nimeahirisha kikao mpaka Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 8.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 5/06/2017saa 3:00 asubuhi)